

Kuandaliwa na Sarah Small,
Jon Paul Witt,
Alan Scantlebury
na Jo Kimball

Misingi 3:

# Maisha Huumba

DIGNITY

www.dignityonline.org.uk

# Misingi 3
# Maisha Huumba

*''Wapate kuitwa miti ya haki,*
*iliyopandwa na BWANA, ili atukuzwe.'*

*Isaya 61:3*

**Misingi 3: Maisha Huumba, Toleo la Kwanza, January 2020**
Haki miliki © Dignity 2020. Haki zote zimehifadhiwa.

**Wasiliana na Dignity**
Kwa Posta: 6 Barlow Moor Road, Didsbury, Manchester, M20 6TR, UK
Kwa Tovuti: hello@dignityonline.org.uk
Kwa Simu: +44 (0)7340 573 937

**Shukrani**
Dignity inamshukuru Yesu kwa maisha anayotoa kugundua ndani ya kitabu hiki. Dignity inamshukuru kila mtu na kumwamini kila aliyetoa mchango kwa kazi hii.

**Kazi ya Dignity**
Washiriki wa Dignity pamoja na wale wa kiunga kwenye jamii wanavuvia mabadiliko ya maisha na jumuiya kuleta uhuru kutoka kwenye umaskini kupitia mahusiano na Yesu. Tunayafikia haya kimsingi kupitia Vikundi vya Uzima, vikundi visivyo rasmi inayoongoza jumuia za Kikristo inayowaandaa watu kutembea karibu na Yesu na kuonyesha upendo kwa hao wanaowazunguka. Kupitia kazi yetu tuanawaona watu wakiishi maisha ya kushangaza na kuwa sehemu ya muujiza wa kila siku. Tafuta zaidi kwa: **www.dignityonline.org.uk**

**Kikundi nyuma ya Misingi**
Waandishi na wahariri: Sarah Small, Paul Witt, Alan Scantlebury na Jo Kimball
Wasomi wa Kitamaduni: Cornelius Chalwe, Gervas Chalwe na Dorothy Jikubi
Wasomi Wahakiki: Rachel Warner, Mark Vermes, na Elisabeth Cartwright
Mkalimani: Christopher John Mollel

**Dondoo za Biblia**
Biblia Habari Njema kwa Watu Wote (Yenye Vitabu vya Deuterokanoni): Tafsiri ya Ushirikiano wa Makanisa (BHN): Hakimiliki - 1995, 2001: kwa Chama cha Biblia cha Tanzania na Chama cha Biblia cha Kenya. Haki zote zimehifadhiwa.

**Taswira za Alama Zinazoongoza**
Taswira za Alama Zinazoongoza zimechorwa na Studio ya Metro Icon 5 iliyochapishwa na SyncFusion. Alama zimetumika kwa ruhusa.

# Misingi

**Misingi** ni mafundisho inayowasaidia watu kugundua na kukua ndani ya mahusiano yao na Mungu na kuwatia moyo kuhudumia jumuiya zao. Iliandikwa ili iweze kutoa vifaa vilivyo bora ambavyo vingeweza kutumika kwenye maeneo mengi ya kijiografia na kwenye vikundi vya kitamaduni duniani pote. **Misingi** ni mkusanyiko wa seti ya vitabu vine, na kila kimoja kinayo vipindi kumi na vitatu ya mafundisho kwenye vikundi.

**Misingi** imeandikwa na waandishi wageni waliojitolea toka duniani kote na kukusanywa na kuandaliwa na Dignity.

***Misingi 1: Maisha Yameanza*** inawalenga wale walio wapya au wasio na imani. Kwa mwanzo rahisi inawaongoza watu kwenye hatua hatua za mwanzo za imani na kumjua Mungu.

***Misingi 2: Maisha Hukua*** na kujenga msingi itakayowezesha imani kukua na kutoa ufahamu kwa baadhi ya maandiko yanayotumika ya Biblia na maombi.

***Misingi 3: Maisha Huumba*** umakini namna mitume walivyoishi ndani ya jumia walivyoleta mabadiliko kwa kila kilchowazunguka wao. Mkristo mwenye afya kwa kawaida huumba maisha waliyopewa kwenye jumuia zao na kwa watu wengine.

***Misingi 4: Maisha Hukomaa*** huonyesha jinsi Mkristo aliyekomaa anavyopaswa kuonekana. Kitabu hiki kinabeba mawazo wa mtiririko uliyobaki, ikizamisha na kupanua.

# Uandishi

***Misingi 3: Maisha Huumba*** iliandikwa na waandishi waliyojitolea toka duniani pote. Waandishi waliyochangia kwenye kitabu hiki wameorodheshwa kwa utaratibu wa alfabeti.



**Kate Dean** alifanya kazi kwenye elimu kwa zaidi ya miaka thelathini na kupenda kuwaona watoto wakistawi na kuwa jinsi Mungu alivyowaumba. Aliendelea kufanya kazi na shule na walimu wakuu na kutaka sana uangalizi mzuri kwa watoto na vijana. Hivi karibuni Kate amefanyika moja wa wadhamini wa Dignity na anaangalia mbele kwa nafasi yake hiyo ya kuwasaidia watu wenye shida.

*Kipindi 12*



**Anthony Delaney** amemwoa Zoe na anaongoza Kanisa la Ivy Manchester kule Uingereza. Anthony ni mwanzilishi wa Kanisa la KUFYATUA maongezeko na pia anaongoza ‘Kitu Kipya’ Ulaya magharibi. Ameandika vitabu kadhaa na kuonekana mara kwa mara kwenye radio ya BBC. Anapatikana pia kwenye anthonydelaney.com.

*Kipindi 2*



**Dennis Hardy** alimfanya Yesu kuwa Bwana wa maisha yake akiwa na miaka 16. Aliamini kuwa ni muhimu zaidi kwenda na kuwaambia watu badala ya kuwaambia waje na kufahamu. Pamoja na mkewe Jane na familia changa Dennis alitumia miaka 10 kule Bangkok. Kwa sasa wanaishi Manchester, Uingereza na wanajihusisha na hali ya kwenda na kuwaambia wengine.

*Kipindi 9*

**Michael Heng** amemuoa Mina na kwa pamoja wanao vijana 2. Wanaishi Kaskazini Mashariki ya pwani ya Uingereza mahali Michael anaendesha shughuli ndogo ya kufua na kupasi. Aliacha ujuzi wake wa upasuaji ili kutoa muda zaidi kwenye mahusiano yake na Kristo na familia yake.

*Kipindi 3*

**Mina Heng** alizaliwa Mauritius na akaja Liverpool kwa masomo yake. Akiwa huko alikutana na Michael na kwa sasa wameoana kwa muda wa miaka 18 na wanao vijana 2. Mina amefanyika kuwa Mkristo alipohudhuria kipindi cha kikundi cha vijana akiwa kijana. Mungu alimpa kusudi, sababu ya kuwa na anasema ghafla maisha yakawa na maana.

*Kipindi 6*



**Jo Kimball** amekuwa sehemu ya timu ya Dignity kuanzia 2008, akitembea mbali Zambia kufanya kazi na Vikundi vya Uzima na Kuvuvia Timu. Yeye ni muunganishaji na mtia moyo anayefurahia akiwaona wengine wakistawi na kujifunza nini maana ya kupendwa na Yesu.

*Kipindi 11*



**Reverend Peter Matthews** ni kiongozi kwenye kanisa la Anglikana kule Trafford ya Zamani, Manchester. Hivi karibuni alifundisha somo la fisikia kwenye shule tatu tofauti, akitumia kipaji chake cha kufundisha Afrika.

*Kipindi 7*



**Sarah Small** alilelewa na kukua Yorkshire halafu akasomea Dini na Theologia kule Manchester. Miaka 10 iliyofuata alifanya kazi kwenye kitengo cha kujitolea Uingereza na Afrika, sasa anajihusisha na umisheni maeneo ya vijijini kule Uingereza. Anashiriki uongozi wa kanisa, kazi ya kujitolea na ana familia ya watoto 2 na hivi karibuni amemaliza elimu ya MA kwenye Theologia ya Kingdom.

*Kipindi 4, 8 na 13*



**Richard Thompson** ni kiongozi wa Kituo cha Ndubaluba Nje, sehemu ya shule ya Chengelo, huko Mkushi, Zambia. Richard anayo hisia kali ya kuwaendeleza Wakristo kwenye kujifunza ugunduzi na kutumia mtiririko wa uvumbuzi na shughuli za nje kutoa changamoto kwa vijana kuhusiana na imani yao. Mwanzo kutokea ni Uingereza, na amefanya kazi Ndubaluba kwa miaka 23 na ameoa na ana watoto 2.

*Kipindi 5*



**Jon Paul Witt** ni mwanzilishi wa Dignity na amefanya kazi na makanisa ndani ya nchi nyingi. Ni mtu mwenye kufikiri, mwanzilishi, mwinjilisti na misionari. Jon amemuoa Judith na wanao watoto 3. Wanaishi kati ya Zambia na Uingereza. Hisia za Jon ni kuwaona watu kufikia kumjua Yesu na kwa hisia kali kuweza kubadilisha jumuia zao.

*Kipindi 1 na 10*

# Yaliyomo


Namna ya kutumia kitabu hiki ....................10

Kuhakikisha usalama wa watoto pale kwenye Vikundi vya Uzima ....................15

1: Mungu kama Jumuiya ....................16

2: Jumuiya ya Mungu - Kanisa....................26

3: Karama zangu ni Zipi? ....................34

4: Nitatumiaje Karama zangu? ....................44

5: Kuamini na Imani ....................52

6: Vita vya Kiroho ....................64

7: Kuombea Jumuia yetu....................78

8: Ushahidi - Kwa nini na Namna gani?....................86

9: Nenda Uwaambie Wengine ....................94

10: Haki .................... 106

11: Kuleta Mamlaka ya Kisheria .................... 116

12: Kuwasaidia Wengine Kukua .................... 126

13: Ufupisho wa Kipindi .................... 136

# Namna ya kutumia kitabu hiki

Kitabu hiki kimeandaliwa kutumika kwa mafundisho ya kikundi. Ni kiongozi anayeongoza kikao ndiye anahitajika kuwa na nakala ya kitabu hiki. Unapaswa kujaribu kukamilisha kila kikao kwa muda wa saa 1.5 – 2. Kama utaona unahitaji muda mrefu, siku zote utamaliza kikao 1 kwa muda muda wa wiki 2.

Inadhaniwa kuwa watu wanaojifunza kitabu hiki tayari wamekwisha jifunza ***Misingi 1: Maisha Huanza*** na ***Misingi 2: Maisha Hukua***. Hii ina maana kuwa baadhi ya mawazo hayajaelezwa tena kwenye kitabu huku. Ikiwa baadhi ya watu wanajiunga na kikundi chako ambao ni Wakristo wapya inawezekana ukarudia baadhi ya mawazo kwenye vitabu vilivyopita pamoja nao. Njia moja ya kufanya hivyo ni kuanza mafundisho ya kikundi kingine. Kitabu cha Dignity cha ***Panda*** kinaweza kukusaidia kwa jambo hili.

**Namna ya kuongoza kikao**

Ni muhimu kumhusisha kila mtu kwenye kikao. Siyo tu kwa wepesi kusoma kikao na kuwaambia watu jambo wanalopaswa kufanya. Tunaamini kuwa kila mtu anacho kitu cha kipekee cha kuchangia na Mungu hutufundisha kupitia hao wanaotuzunguka. Kwa ajili hiyo, vikao vimeandaliwa kwa namna ambayo kila mtu anapaswa kuhusika. Kuna vifungu vya kukumbuka, maswali, maigizo, hadithi na majadiliano yanayomhitaji kila mtu kuhusika.

Kama kiongozi wa Kikundi unapaswa kuhamasisha majadiliano na kusaidia yaendelee kwa njia iliyo sahihihi, lakini hupaswa kufanya kila jambo mwenyewe.

Unapaswa kuwatia moyo watu wenye aibu na wakimya kujaribu na kuongea wanapoweza. Unapaswa kuwatia watu moyo wenye kelele na wazungumzaji sana kuwapa wengine nafasi kushirikisha mawazo yao pia.

**Unachohitaji kwa kila kikao**

Vikao vimeandaliwa kuwa vyepesi na aihitaji vyanzo vingi. Utahitaji:

- Nakala ya kitabu hiki kwa mtu anayeongoza kikao
- Biblia (itasaidia ikiwa watu wachache kwenye kikundi kuleta Biblia pia, lakini siyo lazima)
- Kalamu na karatasi, ambavyo mara zote hutumika kwenye shughuli. Unapaswa kuwatia watu moyo kuleta vitu hivyo toka nyumbani.

Ikiwa kuna kitu kingine kitahitajika, hii inatakiwa kujulikana kikao kinapoanza na inahitajika kwa ajili gani. Unapaswa kuandaa vitu hivi mapema.

**Ishara za kukusaidia wewe**

Kukusaidia wewe kuongoza kikao tumejumlisha ishara kukjulisha wewe kila sehemu ni nini. Ishara zimeonyeshwa hapo chini na maana yake. Chukua muda kujua kila ishara ina maana gani na kutazazama baadhi ya vikao na kujua jinsi kila ishara inavyotumika. Hii itakurahisishia wewe wakati unaongoza kikao.



**Maandalizi**

Kuhakikisha kuwa kila kikao kinafanyika kwa urahisi hapa kuna vitu vyepesi unavyopaswa kufanya ili kuandaa. Hii inajumlisha wewe kuwa na uhakika kuwa na vitu vyote unavyovihitaji kwa ajili ya kikao tayari na kuandaa watu wa kujitolea kabla ya kukutana. Unapaswa kuangalia mambo haya siku chache kabla hujafanya kikao hivyo utakuwa na muda wa kufanya yale yanayopaswa kufanyika.



**Lengo**

Kila kikao huanza na lengo. Hii itakuongoza wewe kwa yale unayoyafundisha kikundi na kile ambacho kila mtu anapaswa kukielewa anapomaliza kikao. Unapaswa siku zote kutunza malengo haya kwenye fikira zako na kujiuliza kama unawasaidia watu kuyafikia. Ni wazo jema kuanza kushirikisha haya kwenye kikundi.

**Kifungu cha Kukumbuka**

Kila mmoja anapaswa kujifunza kifungu cha kukumbuka na kuweza kukariri mwisho wa kikao. Unapaswa kuwafundisha kwa kusoma kifungu cha kukumbuka na marejeo ya Biblia kwa sauti kwa kikundi. Soma tena lakini kwa wakati huu soma hatua kwa hatua, kwa sehemu ndogo, waambie kikundi kurudia kila sehemu baada yako. Rudia utaratibu huu, pole pole soma sehemu ndefu pamoja na kikundi ukirudia kila sehemu mpaka kila mtu aweze kukariri kifungu chote bila msaada wako. Watie moyo watu wengine wajaribu na kurudia wao wenyewe.

**Hadithi**

Hadithi ni njia nzuri sana ya kutambulisha somo na kujifunza kutoka kitu kinachojulikana. Kila mtu hufurahia hadithi na ni rahisi kukumbuka! Unapo hadithia kikundi, unapaswa kuwaleta kwenye maisha halisi kwa kutumia maigizo. Ikiwa kama kuna mtu kwenye kikundi chako ambaye ni mzuri kwenye kuhadithia itakuwa ni vizuri kuwaambaia wahadithie. Unapaswa kuwaambia mapema kabla ya kikao na kuwapa nafasi ya kujiandaa.

**Kujifunza Biblia**

Kila kikao walao inayo ukrasa 1 wa Biblia wa kusoma, na zingine inayo zaidi. Ikiwa kama kuna watu kwenye kikundi chako wasomaji wazuri unaweza kuwaambia kusoma hayo kwa niaba yako. Unapaswa kuwaambia mapema ili waweze kufanya mazoezi au wakuambie kuwa hawawezi kusoma. Kumbuka kuwa watu wengine hawajui kusoma hivyo unapowaambia kusoma mbele za watu wakati hawawezi kusema hapana ni kama kuwadhalilisha.

**Kuongea**

Hizi ni sehemu zinazopaswa kusomwa kwa sauti toka kwenye kitabu. Unapoyapitia haya unapaswa kuweka kituo mara kwa mara, hasa kwenye pointi za muhimu, na waulize watu kama wameelewa yale unayoyasema. Kama hawajakuelewa, unaweza kurudia sehemu au kujadili jambo kuwasaidia kuelewa.

**Maswali na Kujadili**

Kujibu maswali na kujadili mambo huwasaidia watu kujifunza na kuanzisha kitu wao wenyewe. Hii itawasaidia kukumbuka. Unapoona ishara ya swali ni muhimu kuuliza kikundi swali na kuwatia moyo baadhi ya watu tofauti kutoa majibu. Wakati mwingine maswali ni ya majadiliano kwenye vikundi vidogo. Kama kikao kikikuonyesha hivyo, unapaswa kugawanya watu kwenye vikundi vya 3 au 4 na kuwapa muda wa kujadili maswali. Kama kikundi chote wakija kwa pamoja unapaswa kutoa muda kwa kila kikundi kushirikisha moja au mbili ya pointi walizojadili.

Ikiwa kama kuna maswali mengi ama marejeo ya Biblia ambayo watu watakutaka wewe unaweza kumtia mtu moyo toka kila kikundi kupiga picha swali kutumia simu zao ama kuandaa kabla kwa kuandika nakala ya ziada ya maswali.

**Shughuli**

Watu hujifunza wakati wanapokuwa na vitu vya kuwafurahisha na kwa kufanya jambo fulani. Shughuli husaidia jambo hili kutokea. Unapaswa kumhusisha kila mtu kwenye shughuli na kuwatia moyo wawe na vitu vya kufurahisha wakati wanapofanya hivyo!

**Maombi**

Yale ambayo Mungu anasema moja kwa moja ni ya muhimu sana. Tunataka kutia moyo kikundi chako kuomba na kuombeana pale inapowezekana. Unapoona ishara hii unapaswa kuwaambia watu kuomba. Kuna namna tofauti ya kuomba ambayo imetumika kwenye kitabu hiki chote. Wakati mwingine kikundi inaweza kuambiwa kwa pamoja, wakati mwingine kwenye vikundi vidogo na wakati mwingine wawili wawili. Wakati mwingine watu wanaambiwa wapige kelele kwa Mungu na kwa wakati mwingine watu wanaambiwa kuomba kimya kimya. Ni muhimu kuwa unaacha muda wa kutosha kwa maombi na kuwatia watu moyo kusikiliza yale anayoyasema Mungu.

**Kufanya wiki hii**

Kila wiki kuna kazi ya nyumbani ya watu kufanya. Unapaswa kueleza kwa uangalifu kuwafanya watu kuelewa na uwatie watu moyo kufanya haya wakati wa wiki. Mwanzoni mwa kikao, unapaswa kuwaruhusu watu wakati mwingine kutoa mrejeo kama wamefanya kazi hiyo waliyopewa.

**Shahidi**

Ni muhimu kuwa tunaonyesha upendo wa Yesu kwa hao wanaotuzunguka. Tunaweza kufanya hivyo kwa njia nyingi tofauti. Kila kikao hutupatia wazo namna ya kufanya jambo lenyewe. Unapaswa kulieleza kwa uangalifu jambo hili kwenye kikundi na kumtia moyo kila mmoja kufanya shughuli hizi wakati wa wiki. Tunapoonyesha upendo wa Yesu kwa hao wanaotuzunguka tunaamini Yesu atabadilisha maisha ya hao wanaotuzunguka na kuleta uhuru. Itakuwa ni vizuri kuwatia moyo wanakikundi kutunza kumbukumbu ya watu waliyozungumza nao kama sehemu ya shughuli hizi na kuwatia moyo kuendelea kuwaombea watu hao.

5 Dakika

**Kuweka muda**

Kwenye maeneo mengine tumeweka pendekezo la urefu wa muda ambao shughuli ama majadiliano utachukua. Hii itakusaidia wewe kutunza muda uliyokubalika kwenye kikao.

**Kurasa sa Biblia na marejeo**

Unapoona jina na namba imepigwa mstari namna hii Zaburi 1:4-6 inakurejesha wewe kwenye ukrsa kwenye Biblia. Maana yah ii hasa unatakiwa kusoma kutoka kwenye kitabu cha Zaburi, mlango wa 1 mstari wa 4 na 6.

# Kuhakikisha usalama wa watoto pale kwenye Vikundi vya Uzima

Kwa pamoja tunaweza kuja na sheria nyepesi ili kuhakikisha watoto wetu wako salama ikiwa wapo nyumbani au pamoja nasi kwenye Kikundi cha Uzima. Sheria hizi ni vema kuzitumia kwenye maeneo ya maisha yetu pia. Ikiwa tunafanya kazi mashambani, kanisani au pamoja na marafiki, Mungu anataka sisi kuhakikisha kuwa watoto wetu wako salama.

Kila mmoja anayehudhuria kwenye kikundi ni lazima kuhakikisha kuwa watoto wao wako salama nyumbani na wanaangaliwa na mtu anayehusika au waje na watoto wao.

Viongozi wa vikundi wanapaswa kuwakumbusha wanakikundi kuhakikisha kuwa watoto wao wako salama nyumbani na wanaangaliwa na mtu anayehusika na pia kuwakaribisha watoto kwenye kikundi.

Mtu yeyote aliyeko kwenye kikundi na anashughulika na watoto ni lazima asifanye kazi mwenyewe afanye na mtu mmoja ama wawili zaidi. Ikiwa ni watu wawili, wasitoke familia moja. (Lazima wawe wa familia tofauti.)

Hao wanaoshughulika na watoto kwenye kikundi wawe ni watu ambao wamehudhuria kwenye kikundi kwa walao miezi mitatu bila kukosa.

Viongozi wa vikundi na wanachama ni lazima wasipige picha za watoto wakatiijihusisha na shughuli za Vikundi vya Uzima.

Ikiwa watoto watashiriki chakula kwenye mikutano ya vikundi, hakikisha ni salama wao kula.

Wanachama wa Vikundi wakati wana tembelea watu kwenye jumuia ni lazima watembee wawili, kwa mfano wanaume 2 kumtembelea mwanamume au wanawake 2 kumtembelea mwanamke.

1

# Mungu kama Jumuiya



'Sikiliza, ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja.'

Kumbukumbu la Torati 6:4

**Maandalizi**

Unachohitaji kwenye kipindi hiki:

- Chupa, iliyo wazi tupu, juisi uliyoongeza maji, maji ya kunywa na kikombe kwa kila mwanachama wa kikundi
- Kalamu na karatasi

Uwe na:

- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma Kifungu cha Biblia?

5 Dakika

**Karibu**

Mkaribishe kila moja kwenye kikundi na uwashukuru kwa kufika. Ikiwa kuna mtu yeyote mpya anayejiunga na kikundi unapaswa kuanza kwa kumwambia kila moja jina lako na kuwaambia kila moja aseme jina lake kwenye kikundi. Unapaswa kuwaeleza kitakachotokea kwenye kikundi.

Useme maombi, mafupi ya shukrani.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kufahamu kuwa Mungu yupo akipenda jumuia ndani yake. Ingawa yeye ni Mungu moja, amejidhihirisha mwenyewe kwa nafsi 3: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Wanashiriki asili moja, wakiishi na kufanya kazi pamoja kwa upendo, tunavyopaswa pia kufanya.

5 Dakika

**Kifungu cha Kukumbuka**

Soma kifungu cha kukumbuka na dondoo za Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Rudia tena kusoma na kuambia kikundi kurudia baada yako mpaka kila moja aweze kukariri kifungu chote. Watie moyo baadhi ya watu kujaribu na kurudia tena wenyewe.

*Sikiliza, ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja.*
*Kumbukumbu la Torati 6:4*

**Hadithi**

Wasomee hadithi inayofuata kikundi:

Faith anaishi kwenye Kisiwa Okavango Kaskazini mwa Botswana. Anaishi kwenye kijiji chenye mchanga, eneo lenye vumbi kwenye kasiwa. Kijiji chake kinafanana na vingine kwenye mkoa, mahali ambapo watu wengi kutoka mbali walisafiri kuishi eneo hilo. Eneo lina watalii wengi na watu hushindana kupata kazi kwenye nyumba za wageni na hifadhi.

Hii ina maana kuwa kijiji cha akina Faith haikuwa kama ilivyokuwa hapo mwanzo. Imekuwa kama ulimfahamu mtu kutoka kizazi hadi kizazi. Watu wanaweza kukaa mahali hapo kwa maisha yao yote. Kwa nyakati hizi haifanyiki hivyo. Watu wanaingia na kutoka kutegemeana na kazi zao, wengine hata wanazo nyumba maeneo mengine. Watu hawafahamiani na hawaishi pamoja kama ilivyokuwa mwanzo. Hii ina maana kuwa kama mtu anapambana, wakati mwingine watu hawajui juu ya hilo. Hakuna mtu wa kusaidia. Hakuna umoja tena au hali ya jumuia kama ilivyokuwa mwanzo.

Siku ya huzuni ilitokea kwenye kijiji. Brenda na Lewis walikuwa wameoana kwa miaka mingi. Kwa bahati mbaya, Lewis aligongwa basi dogo akielekea sokoni. Alikufa hapo, akimwacha mjane na watoto watano wakipambana wenyewe. Brenda alijawa na huzuni. Hakuweza kukabiliana na kumpoteza Lewis na changamoto zilizomtokea. Wakati ulipoendelea watoto waliacha kwenda shule, na kwa wakati mwingine hawakuweza kula na Brenda akawa haonekani.

Faith alitatizika na mambo hayo. Siku zote alikuwa Mkristo na kuelewa kuwa jumuia ilikuwa ni ya muhimu sana. Alikumbuka jinsi watu walivyomsaidia huko nyuma. Hata ingawa hakuelewa kamili kuwa ni kwa nini, alijua kuwa jumuia ni ilikuwa ni ya muhimu kwa Mungu. Ilikuwa sawa kusimama na kusaidiana. Akilifikiri hilo kwenye mawazo yake Faith aliamua kusaidia.

Alianza kumtembelea kila mtu aliyemfahamu kwenye kijiji hicho na kuongea nao namna vitu vilivyobadilika na namna Brenda alivyohitaji msaada. Kila moja aliyezungumza naye alikubali kuwa watatenda zaidi kwa pamoja na kuwa ni muhimu kusaidia inavyowezekana. Ingawa Faith hakuweza kufanya vingi mwenyewe, kila moja kwa pamoja walianza kuhakikisha kuwa Brenda na wanawe wameweza kuhudumiwa. Walimtembelea, wakachangia ada ya shule na kumuunganisha kwenye maisha yao. Watoto wake wakaanza kutabasamu tena, wakawa na furaha na maisha ya baadaye. Brenda akaanza kuonekana kijijini na kujisikia sehemu jumuia. Haya yote yalifanyika kwa Faith na moyo wake kwa jumuia.

Uliza kikundi ni nini kingeweza kutokea kama Faith hakufanya jambo lolote?

**Kujifunza Biblia**

Kifungu cha kukumbuka ni cha muhimu sana kwetu sisi kufikiri juu ya Mungu ndani ya jumuia na ina maana gani kwetu sisi kama Wakristo. Unaweza kuuliza, "Kifungu kuhusu Mungu kama mtu moja inaweza kufanya nini kwenye jumuia?"

Kifungu hiki toka kitabu cha Kumbukumbu la Torati ni kifungu kinachojulikana kwenye imani ya Wayahudi, imani ambaya Wakristo wamechukua mizizi yake. Ni kelele, tamko kwa taifa la zamani la Israeli kuhusu Mungu ni nani. Ndiyo sababu maneno ya mwanzo ya kifungu yalikuwa 'Sikia, Ee Israel'. Sehemu nyingine ya kifungu ni mahali panapofurahisha.

'Bwana Mungu wetu' inamaanisha hasa kinachosema. Jina la Wayahudi la Mungu lilikuwa Yahweh na ina mizizi ndani ya jina la Mungu mwenyewe 'Niko' (Kutoka 3:14). Kifungu cha kukumbuka leo kinasema Yahweh ni Mungu, Mungu moja, Mungu wetu wa pekee.

Kwa hiyo haya yana nini cha kufanya na jumuia? Sehemu nyingine ya kifungu inatuambia haya.

‘Bwana ni moja.’ Neno ‘moja’ kwenye kifungu hiki haisemi na wala haina maana ya mtu mojo. Ni neno ambalo ni lazima liwe na maana ya zaidi ya mtu moja. Neno ‘moja’ ni tafsiri ya neno la Kiebrania ‘echad’, ikiwa na maana ya kusudi la umoja, kiakili au makubaliano. Kwa mfano, itakuwa kama watu wote kwenye kijiji chako au jumuia kukubaliana kwa pamoja kwa jambo Fulani na kusema, ‘Tu wamoja’.

Kifungu chetu cha kukumbuka kina maana kuwa, ‘Sikia, Ee Israel, Bwana Mungu wako ni Mungu moja, Bwana Mungu wako anaishi kwenye jumuia ya zaidi ya mtu moja’.

Hiyo inaweza kuwa jambo zuri gumu kulielewa. Inawezekana umesikia juu ya Utatu – Mungu ambaye ni Baba, Mwana na Roho Mtakatifu – pengine mapema kwenye ***Misingi***, au sehemu nyingine. Hivi ndivyo inavyofanya kazi. Mungu anaishi kwenye jumuia ya Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Inapendeza namna gani kwamba anatualika kuwa sehemu ya jumuia yake. Kama watu wake tunayo sehemu kwenye jumuia ya Mungu na tumealikwa kuwa moja pamoja naye. Tunapokubali maisha yake mapya na kujiunga na jumuia hii, maisha haya ndani yetu halafu kazi kuunda nafasi hata kwa watu zaidi kujiunga pia.

**Shughuli**

5 Dakika

Kwenye shughuli hii utahitaji kitu kitupu, tazama kupitia chupa, juisi kiasi ambayo utachanganya na maji kiasi ya kunywa.

Shughuli hii itawasaidia watu kuelewa jinsi jumuia ya Mungu ilivyo karibu.

- Chukua chupa tupu na juisi kiasi. Mbele ya kila mtu mimina juisi kiasi ndani ya chupa. (Mimina ndani juisi ya kutosha ili wakati imechanganywa na maji itakuwa ni nzuri ya kunywa.)
- Waulize wote kama wanaweza kuona hiyo juisi.
- Sasa jaza chupa yote na maji. Tingisha chupa hiyo mbele ya kila mtu ili waweze kujua kuwa maji na juisi zimechanganywa.
- Pitisha chupa mbele ya kikundi chote, ukiwauliza kama wanaweza kuona mahali maji yamesimamia mwishoni, na mahali juisi ilipo. (Jibu ni kuwa hawawezi kuliona hili.)
- Mmiminie kila mtu kinywaji cha juisi iliyochanganywa na kumuuliza kila mtu namna ilivyo anapoonja. Wanaweza kusema kitu kama, ‘tamu’, ‘nzuri’ au ‘nzuri sana’.
- Waeleze kuwa wakati watu wako kwenye jumuia na wamekaribiana kiasi cha kwamba huwezi kuona mwanzo wala mwisho, sasa kionjo hicho ni kizuri kwa kila mtu.

Hivyo ndivyo jumuia ya Mungu ilivyo. Jumuia yetu inapaswa kuwa hivyo. Tutaenda kusoma baadhi ya vifungu vya Biblia inayotueleza jambo hili.

Soma Warumi 12:4-5 na Matendo 2:42-47 kwenye kikundi:

> [4]*Kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja tuna viungo vingi,*
> *wala viungo vyote havitendi kazi moja;* [5]*vivyo hivyo na sisi*
> *tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo, kila*
> *mmoja kwa mwenzake.*
>
> *Warumi 12:4-5*

> [42]*Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika*
> *ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.* [43]*Kila*
> *mtu akaingiwa na hofu; ajabu nyingi na ishara zikafanywa*
> *na mitume.* [44]*Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja,*
> *na kuwa na vitu vyote kishirika,* [45]*wakiuza mali zao, na vitu*
> *vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote*

*kulingana na haja ya kila mmoja. [46]Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe, [47]wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.*

*Matendo 2:42-47*

?

15 Dakika

**Maswali**

Maswali haya yametengenezwa kutusaidia sisi kuelewa vifungu na maana yake kwenye jumuia yetu. Wagawanye kwenye vikundi cha watu 3 au 4 ili waweze kujadili maswali na marejesho kwa kila moja. Unaweza kutaka kila kikundi kuwa na swali la tofauti.

- Ni ukaribu gani unaweza kuwa kwa mtu ambaye watu huko nje ya uhusiano huo wanaweza kukuita 'moja'? Hiyo ina maana gani kwenye jumuia yetu?
- Tunawezaje kuishi kwa pamoja kama moja?
- Nini inawazuia watu kuishi kwenye jumuia? Tunawezaje kushinda hilo?
- Ni nani huyo wa muhimu kwenye jumuia?
- Kwa nini tusihusishe kila mtu ndani ya jumuia yetu ya watu wa Mungu?

Ruhusu muda kwa kila kikundi kushuhudia mawazo yao kwa kila mtu. Hili ni swali la muhimu sana la kujadili. Waambie wote waje pamoja. Somo Matendo 2:46-47 tena na mjadili maswali haya na kikundi chote:

- Unafikiri tunaweza kuwahusisha hao wasioamini au hata wako kinyume na Mungu ndani ya jumuia yatu?
- Kwa nini unafikiri juu ya hili?

Tutalitaza swali hili kwa njia tofauti kwenye kitabu hiki chote.

**Maombi**

15 Dakika

Tumetazama ukweli kuwa Mungu ni moja, si kama mtu wa pekee, lakini kama Baba wa jumuia, Mwana na Roho Mtakatifu. Tumejifunza kuwa jumuia yetu ya kanisa imekusudiwa kufanana.

Kwa kila moja kwenye kikundi, anza kwa kumsifu Mungu kuwa ametuunganisha na na jumuia yake. Mwabudu yeye kwa kuwa ametuokoa na sasa tunasimama naye na wengine kwenye ufalme wake. Sisitiza kuwa siyo jambo kufanya kwa uwezo wetu. Mnaweza kuimba wimbo kwa pamoja au kutoa shukrani kwa Mungu kwa pamoja.

Sasa tunaenda kuomba tukitambua kuwa siku zote hatuishi kwa njia ambayo Mungu ametuundia sisi au kutenda sawa na namna anavyotaka sisi kufanya. Tunapotazama kanisa letu na makanisa mengine yanayotuzunguka, mara nyingi tunaona mgawanyiko na mabishano. Mgawanyiko unaweza kuwa wa watu binafsi, familia, ama kanisa lote. Kama familia ya Mungu, hatuishi ndani ya jumuia.

Kiambie kikundi chako kusimama na kushikana mikono nje mbele yao. Omba maombi mepesi kumwomba Mungu kuleta ndani ya fikra zao mgawanyiko wowote ndani ya jumuia yake kanisa analotaka kuponya. Ruhusu muda fulani wa utulivu kwa watu kusubiri na kumsikiliza Mungu.

Waambie watu kurudi kwenye vikundi vyao vidogo na kushirikisha yale ambayo Mungu amewaambia kama wanajisikia vizuri kufanya hivyo. Uwe na muda wa kuombea hiyoa hali Mungu aliyoleta kwenye fikra. Unaweza kumwomba Mungu msamaha. Unaweza kuomba kwa ajili ya uponyaji, msamaha na umoja.

Kilete kikundi pamoja na kumaliza kwa kurudia kifungu cha kukumbuka cha leo kwa pamoja na kumshukuru Mungu kwa kuwa ni Mungu wa jumuia.

**Kufanya wiki hii**

Kila wiki kuna kazi ya nyumbani sisi kufanya. Wiki hii, hakikisha kuwa unakuwa na muda na wanachama wengine wa kikundi chako kuendelea kuomba na kuchukua hatua kujenga umoja na jumuia kwenye familia ya Mungu.

Wakati mnapokutana, mkumbushe kila moja hali mliyoombea hivi punde. Ombeni tena kwa pamoja. Halafu mjadili ni hatua gani unayotaka kuchukua au kuwa na ushirika kwa maombi hayo. Je kuna mtu yeyote unapaswa kumomba msamaha? Je kuna mtu yeyote ambaye unapaswa kumsamehe? Kuna kanisa lingine ambalo unapaswa kuacha kuwa kinyume nalo na anza kufanya kazi nao?

Ombeni kwa pamoja na kujitoa kufanya matendo hayo pengine wewe pekee au pamoja, kwa namna itakavyokuwa sawa.

**Shahidi**

Ushuhuda wetu wiki hii itakuwa kuchukua hatua kuponya mgawanyiko kwenye familia ya Mungu. Chochote kile ambacho umekuwa ukikiombea na kupanga kwenye vikundi vyenu, endelea mbele na kufanya vile vitu ulivyojitoa kufanya. Kumbuka kuomba unavyoenda, kuongea kwa upendo na huruma na kutazama namna Mungu alivyo jumuia na kutukaribisha sisi kuwa ndani ya jumuia yake pamoja na hao wanaotuzunguka.

# Kumbukumbu

2

# Jumuiya ya Mungu - Kanisa



'Hata walipokwisha kuziegesha mashua zao pwani, wakaacha vyote wakamfuata.'
Luka 5:11

**Maandalizi**

Unachohitaji kwenye kipindi hiki:

- Neti, bakuli au beseni, karatasi na kalamu au penseli.

Uwe na:

- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma Kifungu cha Biblia?

**Wakaribishe na Mrejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila mtu kwa kufika kwenye kikundi.
- Anza kwa maombi, mepesi mafupi.
- Waulize wanakikundi kama wamefanya 'Kufanya wiki hii' na 'Kushuhudia' kazi toka toka wiki iliyopita.
- Wakaribishe washirikieshe chochote walichokijifunza ama kupata ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kujifunza zaidi kuhusu jumuia ya watu wa Mungu, inayoitwa kanisa. Kanisa, (wakati mwingine inaitwa Mwili wa Kristo) ni jumuia inayopendwa iliyoandaliwa kudhihirisha kweli ya Mungu, upendo na huruma kwa dunia inayotuzunguka.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na dondoo za Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Rudia tena kusoma na kuambia kikundi kurudia baada yako mpaka kila moja aweze kukariri kifungu chote. Watie moyo baadhi ya watu kujaribu na kurudia tena wenyewe.

> *Hata walipokwisha kuziegesha mashua zao pwani, wakaacha vyote wakamfuata.*
>
> *Luka 5:11*

**Hadithi**

Wasomee hadithi inayofuata kikundi:

Jani alikuwa na huzuni na mpweke aliyepambana na afya yake, familia yake na wale aliokuwa na uhusiano nao. Alikuwa na kazi lakini bosi wake alikuwa mkali na hakuelewa kuwa hawezi kufanya kazi kwa haraka kwa sababu ya afya yake dhifu. Mwishowe Jani aliishia kupoteza ile kazi na akaanza kukopa fedha ili aweze kuishi.

Maisha yakaanza kukosa mwelekeo zaidi na zaidi kwa Jani. Kwa wakati huo hata hivyo, alitambua kuwa kulikuwa na kikundi cha watu waliokutana kwenye holi la jumuia karibu na nyumbani kwao siku ya Jumapili. Waliweza kumpungia mkono na kumwonyesha tabasamu walipomwona jambo lililo mwuinua.

Siku moja, mtu moja aliyekuwa akiingia kwenye mkutano alikutana na Jani na akamuuliza kama angeweza kuingia ndani na kushiriki chakula pamoja nao. Jani alikuwa na njaa hivyo akaona ya kuwa wazo hilo ni zuri. Alikula pamoja na kikundi na wakaanza kumshirikisha kuwa wao ni sehemu ya kanisa la mahali. Walikuja pamoja kushirikiana chakula, historia kuhusu Mungu anafanya nini katika maisha yao na kuombeana na kuombea majirani.

Jani akaanza kuhudhuria mikutanao zaidi. Aligundua kuwa kikundi kilifahamu watu ambao wangeweza kumsaidia kwa madeni yake yanayoongezeka, wangeweza kumsaidia kutafuta kazi na la muhimu zaidi walionekana kumjali zaidi, na kutaka kumjua zaidi. Walikuwa na muda wa kujadiliana naye na kuwa na urafiki, kitu ambacho hakuwa na ujuzi nao huko nyuma. Moja ya kikundi alieleza kuwa wote walikutana wakashirikishana maisha pamoja kwa sababu wamepata maisha mapya toka kwa Mungu na walipenda kushirikisha tumaini hili kwa marafiki zao na majirani. Baadaye Jani alimpa Mungu maisha yake na kujiunga na kanisa; alianza kupata ujuzi kwa Mungu kufanya mabadiliko ya maisha yake yeye mwenyewe. Mara zotehaikuwarahisi tabia za zamani na watu aliyowafahamu kuendelea kumsababishia matatizo– lakini maisha yalibadilishwa kidogo kidigo na Mungu, akifanya kazi kupitia jumuia yake, ambalo ni Kanisa.

**Kujifunza Biblia**

Soma Matayo 4:18-22 kwa kikundi:

> *18 Naye alipokuwa akitembea kando ya bahari ya Galilaya,
> aliona ndugu wawili, Simoni aitwaye Petro, na Andrea
> nduguye, wakitupa jarife baharini; kwa maana walikuwa
> wavuvi. 19 Akawaambia, Nifuateni, nami nitawafanya kuwa
> wavuvi wa watu. 20 Mara wakaziacha nyavu zao,
> wakamfuata.*
>
> *21 Alipoendelea, akaona ndugu wengine wawili, Yakobo wa
> Zebedayo, na Yohana nduguye, ambao walikuwa katika
> mashua pamoja na Zebedayo baba yao, wakizitengeneza
> nyavu zao; akawaita. 22 Mara wakaiacha mashua na baba
> yao, wakamfuata.*

Ni changamoto kubwa wafuasi wa Yesu wa mwanzo waliweza kukuta nayo! Aliwaambia waache kila kitu na kumfuata yeye. Alienda kwa vikundi hivi vidogo vya familia na marafiki na kusema, ‘Sasa mtaenda kunitumikia mimi. Lakini hamtaweza kunitumikia na ninyi kujitumikia ninyi wenyewe tena. Mnapaswa kuniweka mimi na wito wangu mbele kwanza.’ Hii ingekuwa dhabihu kubwa, kuachilia mbali maisha yao yaliyopita. Mara nyingine Yesu anawaita watu kufanya hivyo, kwa kuachana na yale aliyokuwa anafanya na kumfuata yeye. Wakati mwingine anatuambia kwa urahisi kumtanguliza yeye kwa yale ambayo tayari tunayafanya, akitutumia sisi kumheshimu na kumtumikia yeye mahali tulipo.

Yesu alichukua jambo la kila siku walilolijua (namna ya kutega samaki) na kutumia kuwafundisha wao kile alichotaka wao kufanya. Alisema, ‘Nitatumia mbinu na karama ambazo tayari unazo, lakini badala ya kuvua samaki, nataka mfanye kazi kwa pamoja kunivulia watu mimi.’ Anawatumia hao ambao

wamekuwa na ujuzi wa maisha yake mapya kuwafikia na kueneza maisha hayo mapya kwa wengine.

Yesu hakuanza tu kwa kujenga makanisa. Hakuanza pia kwa kujenga majengo. Alianza kwa kuita na kuwafanya wanafunzi (wafuasi), akiwajenga pamoja kwenye jumuia, akiwafundisha kuwafanya wanafunzi wengine zaidi na jumuia nyingi yeye akiwa katikati yao. Hili ni kanisa ambalo Jani, kwenye historia yetu hapo juu, alikutana nayo. Walimwalika kwenye jumuia yao wakamshuhudia maisha mapya waliopokea toka kwa Mungu.

Wakati neno ‘kanisa’ inatumika ndani ya Biblia haikuwahi kumaanishwa kuwa ni jengo lakini inazungumzia juu ya kikundi cha watu wanaokuja pamoja kwenye umisheni, Yesu akiwa katikati ya hayo yote. Hilo ndilo kanisa. **Ukiwafanya wanafunzi (wafuasi) mwisho wa yote utafikia tu kanisa. Lakini ukijenga jengo la kanisa, siyo lazima uwapate uwapate wafuasi wa Yesu.**

Huu mkusanyiko wa watu wanaoanza kumfuata Yesu kwa pamoja wanaweza kuwa wachache, wastani au wengi; Kikundi cha Uzima kinaweza hata kuwa kielelezo cha kanisa. Idadi siyo kitu cha muhimu. Kinachojalisha kwa Mungu ni, ‘Nyavu hizi nzuri za kunasa watu zaidi, kuwaleta kwenye ufalme wangu?’ Kwa kadri tunavyofanyika nyavu za kuwafikia wengine, vikundi hivi vya watu vinajifunza kuwa Mungu ni nani: wanamwabudu kwa pamoja; wanashuhudiana kuinuka na kushuka kwenye maisha kwa pamoja na kusaidiana moja kwa mwingine. Wamekuwa ni jumuia yenye kuvutia, kila mara wakiunda nafasi ya kuwakaribisha wanachama wapya na wakitoa muda wao na nguvu kwa uzuri wa moja kwa mwingine.

Wavuvi wote walikuwa wamechoka na kujisikia kuwa hawawezi tena kufanya kazi waliokusudiwa kufanya. Lakini walipomwambia Yesu, ‘Kwa kuwa umesema hivyo, basi tutafanya,’ wakaona muujiza! Inawezekana hilo ndilo lililowasaidia kumfuata yeye. Siyo jambo rahisi kumtanguliza Mungu na kumwamini, lakini hilo ndilo wanafunzi wa kwanza walipewa changamoto kulifanya ili waweze

kuwa sehemu ya jumuia mpya ya Yesu. Waliishi kwa ukaribu ndani ya jumuia kila moja kwa mwingine kwa muda wa miaka mitatu, mchana na usiku. Waliona jinsi Yesu alivyofanya kila kitu na kujifunza kumnakili yeye, na kuiga namna alivyoishi na kupenda.

Unaweza kuwa umeacha kila kitu nyuma – au kumchukua tu samaki sokoni na kubakia pale ulipokuwepo?

Baadaye walpomwona yeye akifa, akawa hai tena na kwenda mbinguni, walikumboka somo la uvuvi alilowaonyesha wao, na wakatoka nje kuwavua watu.

Soma Matendo 2 (tulisoma sehemu ya hii wiki iliyopita) kuona Petro yule aliyepata hilo hakuweza kushika samaki yeyote kwa nguvu zake mwenyewe, 'kumshika' zaidi ya watu 3,000 walikuja na kumfuata Yesu wakati alipoubiri ujumbe wake wa kwanza!

Kuwasaidia watu wengi kupata njia ya kurudia upendo wa Mungu wa milele lazima imemfanya yeye kuwa na furaha zaidi ya siku ile nyavu zao lilijaa na zilikuwa karibu kukatika.

15 Dakika

**Maswali**

Kwenye kikundi cha 3 au 4 mjadili maswali yafuatayo:

- Kuna kitu chochote ulichonacho au iko kwenye njia ya wito wako ya kumfuata Yesu kwa karibu zaidi?
- Wewe ni sehemu ya kanisa? Inafananaje?
- Unadhani unahitaji jingo ili iwe ni kanisa 'kamili'?
- Unafikiri nini kwa kusema Yesu ni kiongozi wa kanisa? Unafikiri kuwa viongozi wa kanisa wanafanana na Yesu?

Rudisha kikundi tena pamoja na uhakikishe kuwa kila moja anayo nafasi ya kushirikisha majibu yao.

**Shughuli**

Kila mtu atahitaji kalamu na karatasi kiasi.

10 Dakika

Waeleze kuwa tunaenda kufikiri juu ya watu tunaowafahamu wasiomwamini Yesu bado au wapo nje ya jumuia ya kanisa.

Mwambie kila mtu achore, kata au teng'eneza mfano wa sura ya samaki juu ya karatasi. Kwa kila sura ya samaki watakayo fanya, waambie watu wachore au kuandika majina ya marafiki, wana familia au watu kwenye jumuia ambao hawamjui Yesu na bado siyo sehemu ya jumuia ya Mungu. Kumbuka kufikiri juu ya watu unaowaona kuwa ni wakiwa au walio nje ya jumuia, au wametengwa na jumuia.

**Maombi**

10 Dakika

Weka wavu, bakuli au chupa na katikati ya chumba.

Waambie wote wasimame kwenye mduara kuzunguka wavu, bakuli na chupa.

Waalike watu waje moja moja na kuweka samaki waliotengeneza ndani ya wavu, bakuli na chupa. Wanapomweka kila samaki kwenye wavu, bakuli na chupa na wao kusema jina mtu anayewakilishwa. Wakati haya yanafanyika, watie moyo kikundi chote kuomba kwa sauti ili kila jina la mtu liliwakilishwa litafikia kumjua Yesu na kuwa sehemu ya jumuia ya Mungu.

**Kufanya wiki hii**

Wiki hii mwombe Mungu nafasi kueleza historia ya muujiza wa kunasa samaki kwa mtu ambaye hamjui Yesu bado. Mwombe Mungu akupe ujasiri kufanya hili. Wakati unapoeleza juu ya historia hii mwombe Mungu aumbe maisha mapya uliyojifunza kwa hao unaoshiriki nao.


**Shahidi**

Jumuia ya Mungu imepanuka kutujumlisha sisi ndani ya kanisa lake, jumuia ya hao wanaompenda yeye. Tunapaswa kufanya hivyo kupanua jumuia yetu tukiwajumlisha wale wasiomjua Mungu. Ilimaanishwa wajumlishwe. Ni rafiki zetu ni hao

tunaokuaga nao. Ni hao wanaokuaga wapweke au wanaoteng'wa kwenye jumuia. Tusipowakaribisha kwenye jumuia ya Mungu, watajua vipi upendo na jumuia ya Mungu?

Wiki hii, tafuta njia ya kuwaunganisha hao ambao kwa sasa wako nje ya jumuia ya Mungu. Watembelee, wabariki, kula chakula nao, cheka au lia nao! Matendo yako ni mwanzo wa kuwakaribisha kwenye jumuia ya Mungu.

Fanyeni haya kwa pamoja.



3

# Karama zangu ni Zipi?

'Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana.'
1 Wakorintho 12:7

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma Kifungu cha Biblia?

**Wakaribishe na Mrejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila mtu kwa kufika kwenye kikundi.
- Anza kwa maombi, mepesi mafupi.
- Waulize wanakikundi kama wamefanya 'Kufanya wiki hii' na 'Kushuhudia' kazi toka toka wiki iliyopita.
- Wakaribishe washirikieshe chochote walichokijifunza ama kupata ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kufahamu kuwa kama ishara ya maisha yetu mapya ndani ya Mungu Roho Mtakatifu humpatia kila moja wetu karama. Ni vya dhamani kwa afya ya kanisa lote na kwa dunia inaotuzunguka. Biblia inataja idadi ya vipawa hivyo, na tutatazama njia yaw ewe kugundua unacho kipawa gani.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na dondoo za Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Rudia tena kusoma na kuambia kikundi kurudia baada yako mpaka kila moja aweze kukariri kifungu chote. Watie moyo baadhi ya watu kujaribu na kurudia tena wenyewe.

*Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana.*

*1 Wakorintho 12:7*

**Hadithi**

Imeandikwa na Maiko ambaye, yeye na familia yake, wanahudhuria kanisa la watu karibu 100 wa miaka yote kwenye mji mdogo kaskazini mwa Uingereza.

Kama mwaka moja uliopita tulisikia kuwa Mungu alituambia kama kanisa kutazama juu ya karama za rohoni. Tulijifunza karama hizo kwa pamoja kwenye ujumbe wetu wa shule ya Jumapili, na kwenye vikundi vingine vya mafundisho ya Biblia vilivyokutana majumbani katikati ya wiki.

Tumekuta inasaidia kutukumbusha sisi wenyewe, au kujifunza kwa mara ya kwanza, vipawa hivyo ni vipi (hekima, akili, imani, uponyaji, kunena kwa lugha, unabii, kupambanua roho, na nguvu ya miujiza), kusudi la kupokea hivi ni (kutumikia kanisa najumuia pana), yale ambayo karama hizi hufanya, na namna tunavyovitumia kwa udhabiti.

Tunachukua muda kutambua ni kipawa gani kila moja anayo. Tumefanya haya kwa mtazamo binafsi na pia kwa kuwauliza hao walio karibu nasi kutuambia ni kipawa gani wanaweza kuona ndani yetu. Tulizungumzia pia juu ya vipawa vilivyo ndani yetu ambavyo ni vipaji, na karama isiogunduliwa au kujifunzwa. Kila moja alimwomba Mungu kutuonyesha karama ambazo tayari tunazo na kutupa karama yeyote nyingine aliyonayo kwa ajili yetu. Kwa miezi kadhaa iliyopita tulianza kuvikuza vipawa hivi ndani ya kanisa.

Kama matokeo, binti moja aliyekuwa akifanya kazi kwenye shule na kuongoza kikundi chetu cha kuabudu alitiwa moyo kukuza kipawa chake cha kuhubiri na kufundisha. Kwa sasa kila mara na kwa nguvu anatufundisha neno la Mungu. Mtu mwingine aliyekuwa na kipawa cha uimbaji ambacho hakua akikitumia amejiunga na kikundi cha kuabudu na akamalizia kwa kuongoza kwa namna mpya yenye nguvu. Wote kwa kweli wamelibariki kanisa.

Binti mwingine aliyekuwa anajisikia kuchoka na kutovuviwa kama sehemu ya kikundi cha kuabudu alishuka chini ili kuanza kikundi kingine kipya cha kujifunza Biblia. Hii imewafikia watu wengi, mume na mke, familia ambazo hazikujisikia kuunganishwa kamili na kanisa na kuwarejesha mara kwenye mwili wa kanisa. Hivyo

tunaweza kuona matumizi ya karama za rohoni ikibariki wale walioko ndani ya kanisa na hao pia walio nje.

Kugundua na kutumia kwa ubora vipawa vyetu vya roho mtakatifu kwa Mungu, tunapaswa kuwa ni watu wa kupenda, waaminifu, wenye kujitoa sadaka na kupenda kujitoa sisi wenyewe kwenye huduma ya Mungu kwa faida ya mwili wake, na kwa jumuia pana.

**Kujifunza Biblia**

Soma 1 Wakorintho 12:1-11 kwenye kikundi:

> *1 Basi, ndugu zangu, kuhusu karama za roho, sitaki mkose*
> *kufahamu. 2 Mwajua ya kuwa mlipokuwa watu wa Mataifa,*
> *mlichukuliwa kufuata sanamu zisizonena, kama*
> *mlivyoongozwa. 3 Kwa hiyo nawaarifu, ya kwamba hakuna*
> *mtu anenaye katika Roho wa Mungu, kusema, Yesu*
> *amelaaniwa; wala hawezi mtu kusema, Yesu ni Bwana,*
> *isipokuwa katika Roho Mtakatifu.*
>
> *4 Basi kuna karama tofauti; bali Roho ni yeye yule. 5 Tena*
> *kuna huduma tofauti, na Bwana ni yeye yule. 6 Kisha kuna*
> *uwezo tofauti wa kutenda kazi, bali Mungu ni yeye yule*
> *azitendaye kazi zote katika wote.*
>
> *7 Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana.*
> *8 Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na*
> *mwingine neno la maarifa, apendavyo Roho yeye yule;*
> *9 mwingine imani katika Roho yeye yule; na mwingine*
> *karama za kuponya katika Roho yule mmoja; 10 na mwingine*
> *matendo ya miujiza; na mwingine unabii; na mwingine*
> *kupambanua roho; mwingine aina za lugha; na mwingine*
> *fasiri za lugha; 11 lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo*
> *mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama*
> *apendavyo yeye.*

Wote tumeumbwa na kupendwa na Mungu, kila moja akiwa na seti ya tabia ya kipekee, vipaji na uwezo. Vipaji na uwezo ni karama ambazo kwa kawaida vinatuongoza sisi kufuata vitu tunavyovipenda na nafasi. Pamoja na karama hizi za asili, Mungu pia huzidisha baadhi ya uwezo wetu au hata kutupa uwezo mpya, kwa njia ya muujiza; hivi ndivyo tunavyovielewa kama karama za rohoni.

Karama za rohoni hutolewa na Roho Mtakatifu. Zingine ni za kudumu na zitakuwa ndani yao; na zingine ni za muda maalum. Roho Mtakatifu anataka karama zitumike kuwaelekeza watu kwa Yesu, kutusaidia tufanane zaidi na Yesu, kuujenga mwili wa Kristo, na kubariki dunia tunayoishi. Hazipo tu kwa ajili ya mahitaji yetu binafsi. Matumizi ya karama za rohoni ni ushahidi wa Mungu kuishi ndani yetu. Maisha ya Mungu ndani yetu mara zote hutafuta kuumba maisha zaidi kwenye mahusiano yetu na jumuia.

Leo tunaenda kuangalia kwa undani zaidi juu ya karama zilivyo, na namna tunavyogundua ni ipi tuliyonayo na namna ya kupokea zile tunazozitamani. Wiki ijayo tutatazama namna ya kuzilea na kutumia karama hizi.

**Karama za rohoni ni nini?**
Kwenye kifungu cha Biblia cha leo idadi tofauti za karama za rohoni zimeorodheshwa. Hivi ni:

- Hekima: Kutumia hekima ya Mungu katika mazingira maalum.
- Akili: Uwezo wa kuleta kweli kwa mtu, kikundi au mazingira kupitia kuona mweleko wa Mungu au kupitia mtazamo wa Biblia.
- Imani: Uwezo wa kumwamini Mungu na kutenda kwenye ahadi zake kwa uhakika na bila kuwa na imani ya kupepesuka kwenye uwezo wake kutimiza ahadi zake.
- Uponyaji: Uwezo wa kufanyika sababu ya Mungu kuwarejesha watu kimwili, kihisia na kiroho.

- Nguvu ya Miujiza: Uwezo wa kufanya miujiza ya ajabu.
- Unabii: Uwezo wa kufunua kweli na kuizungumza kwa wakati na kuhusu tabia ya uelewa, marekebisho, toba, au kutia moyo.
- Kupambanua kati ya roho (utambuzi): Uwezo wa kupambanua kati ya kweli na makosa, lililo sawa na lisilo sawa, na ni roho zipi zilizo nzuri na zipi chafu.
- Kunena kwa lugha za ndimi tofauti: Uwezo wa kunena lugha mpya ya maombi, ama ya dunia au ya mbinguni.
- Tafsiri za lugha: Uwezo wa kufanya ujumbe kueleweka wa mtu anayenena kwa lugha.[1]

Hii tu ni moja ya idadi ya karama za rohoni tunayopata ndani ya Biblia. Tutatazama baadhi ya maeneo mengine inayozungumzia juu ya karama za kiroho kwenye vikundi vidogo sasa.

?

15
Dakika

**Maswali**

Gawanya vikundi vya watu 3 au 4 na uangalie vifungu hivi 1 au 2 hapo chini kwa kila kikundi. Hakikisha kila kifungu kinaangaliwa na hata kikundi 1.

Uliza kila kikundi kuangalia kifungu au vifungu waliyopewa na kutafuta karama za kiroho iliyojumlishwa ndani yao. Karama za kiroho zimejumlishwa kwenye mabano hapa kukusaidia wewe wakati watu wanatoa mrejesho.

- 1 Wakorintho 12:28 (Mitume, manabii, waalimu, wasaidizi, watawala)
- Warumi 12:6-8 (Kutia moyo, kutoa, uongozi, huruma)
- Waefeso 4:11 (Uinjilisti, kuchunga)
- 1 Petro 4:9-10 (Ukarimu)
- Kutoka 31:3-5 (Fundi stadi)
- 1 Timoteo 2:1-2 (Kuombea)

[1] Maelezo iliyosimamia juu ya Bugbee, Bruce & Cousins, Don (2005) *Kusudi la Karama Zondervan*, ukrasa 44-51

- Zaburi 150:3-5 (Kuunda mawasilianao)

Mpe kila moja dakika 5 kufanya hili na kurudi kuwa pamoja kama kikundi na uambie kila kikundi kidogo kuwaambia wengine ni karama zipi za kiroho wamepata kwenye vifungu.

- Uliza kama kuna mtu ameshangazwa au amefurahishwa na karama yeyote waliyopata kwenye vifungu vya Biblia.

**Tunatambuaje karama ambazo tayari tumeshapewa?**

Mtupe Paulo anatuambia 'takeni sana karama za kiroho.' Kwa hiyo, kama watu tumepokea maisha mapya kutoka kwa Mungu, tunapaswa kuwa waangalifu na karama na kumuuliza Mungu karama anayotaka tutumie kwa kazi yake.

Ili kutambua karama ambazo tayari tunazo na kutambua zile tunazozitaka, inawezekana kufuata mtiririko wa hatua:

- **Hatua 1:** Omba na kumuuliza Mungu kukufunulia karama ulizonazo au wewe kuwa nazo. Yeye ndiye mwenye kutoa karama na anakujua zaidi ya mtu yeyote.
- **Hatua ya 2:** Kwako mwenyewe, fikiri juu ya karama za kiroho zilizo tofauti tulizozisoma leo. Je unatambua yeyote kwenye karama hizi ambazo tayari umekwisha zielewa na kuzitumia? Je unatambua karama ambayo unajua kuwa unayo lakini bado hujatumia? Je unadhani kuwa unaweza kuwa na karama fulani, lakini huna uhakika?
- **Hatua 3:** Zungumza na mtu anayekufahamu vizuri kama moja wa familia, Kikundi cha Uzima au kiongozi wa kanisa. Waulze kama wanaweza kuona karama maalum ndani yako, au kutambua neno maalum toka kwa Mungu kwa ajili yako, inayohusu karama yako.

Wakati unapochukua hatua hizi, ni vizuri kukumbuka kama kipawa kinatosha na hali uliyonayo na tabia. Kumbuka kuwa ingawa karama za kiroho 'zinaweza kutosha', hizi ni karama za miujiza na

siyo matokeo ya uwezo wetu wa kibinaadamu. Mungu ndiye mwenye kutoa, siyo kwa faida yetu bali kwa faida pana kwa hao wanaotuzunguka.

Biblia inazo historia isiyoweza kuhesabiwa ya wanaume na wanawake walioweza kutumia karama zilizoonyesha nguvu ya miujiza ya Mungu. Hii iliendelea kupatikana kwa wailioamini kwa sasa ili kurejesha mpango wa Mungu na kusudi juu ya dunia na kuwavuta watu kwake.

20
Dakika

**Shughuli**

Wagawenye tena kwenye kikundi cha 3 au 4 na upitie hatua zile ambazo tayari tumekwisha jifunza. Hii itakusaidia kutambua karama za kiroho kwa hao walioko kwenye kikundi.

Kwenye kila kikundi, muwe na muda wa kuomba, na kufikiri na kuzungumzia juu ya karama za kiroho kwa kila moja kwenye hicho kikundi.

10
Dakika

**Maombi**

Biblia inatuambia kuwa karama za kiroho inatolewa kwa kuwekewa mikono (ona 1 Timoteo 4:14).

Kwenye vikundi vya 3 au 4 muombeane, na kumwekea mikono mtu anayeombewa na kuomba kwamba Mungu awajaze tena kwa Roho Mtakatifu na kuwapa karama za kiroho kwa utukufu wake. Mshukuru Mungu kwa karama ambayo tayari mtu anayo na kuomba kuwa atawawezesha kukua kwa matumizi ya karama hizo.

**Kufanya wiki hii**

Kila wiki kuna kazi ya nyumbani sisi kufanya. Wiki hii, weka listi ya karama za kiroho zilizojadiliwa mapema kwenye mafundisho kwa muda wa majadiliano. Endelea kuomba na kutafakari juu ya listi hiyo, na kumwomba Mungu kuweka wazi kwako karama alizokupa wewe na hizo anazotaka kukongezea.

Omba juu ya namna ya kukuza karama hizi mbele. Mwombe Mungu namna, wapi na lini anataka wewe utumie karama hizi.

**Shahidi**

Wiki hii, chagua moja ya karama ambazo zimetambulikana kuwa unazo. Chukua muda kufanya mazoezi matumizi ya karama.

Unapojifunza karama uliyonayo, tumia moja kumbariki mtu fulani ambaye ni sehemu ya familia ya Mungu tayari. Hii inaweza kuwa mtu mwingine kwenye Kikundi cha Uzima chako, mtu fulani kanisani kwako au toka kanisa lingine.

Omba kwa ajili ya nafasi na kuwa jasiri na utumie karama ulizopewa.

**Ufupisho wa listi za karama za kiroho kutoka vifungu tulivyosoma leo**

- Neno la hekima
- Neno la maarifa
- Imani
- Uponyaji
- Nguvu ya miujiza
- Unabii
- Kupambanua roho
- Kunena kwa lugha
- Kutafsiri lugha
- Utume
- Mafundisho
- Kusaidia
- Utawala
- Kutia moyo
- Kutoa
- Uongozi
- Huruma
- Uinjilisti
- Uchungaji
- Ukarimu
- Ubunifu
- Maombezi
- Kuunda Mawasiliano

# Kumbukumbu



4

# Nitatumiaje Karama zangu?

'Ufuatilieni upendo, na kutaka sana karama za rohoni, lakini zaidi kwamba mpate kutoa unabii.'
1 Wakorintho 14:1

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma Kifungu cha Biblia?

**Wakaribishe na Mrejesho**

5
Dakika

- Mshukuru kila mtu kwa kufika kwenye kikundi.
- Anza kwa maombi, mepesi mafupi.
- Waulize wanakikundi kama wamefanya 'Kufanya wiki hii' na 'Kushuhudia' kazi toka toka wiki iliyopita.
- Wakaribishe washirikieshe chochote walichokijifunza ama kupata ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kujifunza namna ya kutumia karama za kiroho tulizozitambua wiki iliyopita. Tunapojifunza namna ya kufanyia mazoezi karama hizi, ndipo Mungu anaweza kututumia sisi kuumba maisha zaidi kwenye jumuia inayotuzunguka.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5
Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na marejeo ya Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Soma tena kwenye vifungu vidogo, ukiachia kikundi kurudia kila kifungu baada yako. Poleploe soma kwenye vifungu virefu kikundi kikirudia kila kipande mpaka kila mtu aweze kukariri kifungu chote. Watie baadhi ya watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

> *Ufuatilieni upendo, na kutaka sana karama za rohoni, lakini zaidi kwamba mpate kutoa unabii.*
>
> *1 Wakorintho 14:1*

**Hadithi**

Wasomee hadithi inayofuata kikundi:

Hana alisafiri kwenda maeneo ya shaba Nyekundu ya Zambia na timu toka kanisani kwake Uingereza, ili aweze kutumia muda kufanya kazi pamoja na timu ya wajenzi na watu wabunifu kujenga klinik ya matibabu kwa eneo hilo. Hana hakuwa zaidi mjenzi; ingawa aliendа lakuni hakuwa na msaada sana kwa wana kijiji waliokuwa wakifanya kazi kubwa tayari.

Walipokaribia mwisho wa kukaa kwao hapo kijijini, Hana na kikundi chake waliambiwa kushuhudia kwenye huduma ya sherehe kumshukuru Mungu kwa kazi iliyofanyika kijijini. Baadhi ya wanachama wa timu walishuhudia maneno ya kutia moyo toka ndani ya Biblia, wengine wiliimba nyimbo na wengine wakawa na muda wa kuombea washirika wa jumuia.

Wakati wa maombi binti moja wa kijiji aliyekuwa akisaidia kumwangalia Hana na timu yake akaja moja kwa moja kwa Hana akiomba maombi ya uponyaji kwa maumivu aliyokuwa nayo aliyoyapata kufuatilia kuzaliwa kwa watoto wake. Hana ghafla alijawa na hofu: atamwombeaje sawa dada huyu? Itakuwaje ikiwa mama huyo hatapona – hii itazungumzia nini kuhusu Hana na Mungu anayemtumikia?

Pamoja na uoga wake, Hana alimjali mama huyo na hakutaka kumrudisha hivyo aliamua kumwombea. Aliweka mkono wake juu ya bega la mama huyo na kumwomba Mungu, akimwomba kuleta uponyaji ambao pekee angeweza, kwenye maeneo ambayo pekee angeelewa.

Siku chache baada ya kuomba maombi yale Hana na timu yake wakatoa kwaheri yao ya mwisho kwa marafiki wao wapya ndani ya kijiji. Hana hakuwaza zaidi juu ya maombi yake ya uponyaji mpaka yule dada alipomfikia tena akiwa na tabasamu la furaha juu ya uso wake akimwambia kuwa maumivu yake yaliondoka na anajisikia vizuri tena. Aliponywa na Mungu kupitia maombi ya Hana ya uoga – Yesu asifiwe!

**Kujifunza Biblia**

Soma Warumi 12:3-11 kwenye kikundi:

*[3]Kwa maana kwa neema niliyopewa namwambia kila mtu*
*aliyeko kwenu asinuie makuu kupita ilivyompasa kunuia; bali*
*awe na nia ya kiasi, kama Mungu alivyomgawia kila mtu*
*kiasi cha imani. [4]Kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja*
*tuna viungo vingi, wala viungo vyote havitendi kazi moja;*
*[5]vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo,*
*na viungo, kila mmoja kwa mwenzake. [6]Basi kwa kuwa tuna*
*karama zilizo mbalimbali, kwa kadiri ya neema tuliyopewa;*
*ikiwa ni unabii, tutoe unabii kwa kadiri ya imani; [7]ikiwa ni*
*huduma, tuwemo katika huduma yetu; mwenye kufundisha,*
*katika kufundisha kwake; [8]mwenye kuonya, katika kuonya*
*kwake; mwenye kukirimu, kwa moyo mweupe; msimamizi,*
*na asimamie kwa bidii; anayerehemu, na arehemu kwa*
*furaha. [9]Pendo na lisiwe na unafiki lichukieni lililo ovu,*
*mkilishika lililo jema. [10]Kwa pendo la udugu, mpendane ninyi*
*kwa ninyi; kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu; [11]kwa*
*bidii, bila kulegea; mkiwa na juhudi katika roho zenu;*
*mkimtumikia Bwana.*

**Shughuli – Habari Njema**

5 Dakika

Wiki iliyopita tulianza kutazama karama za rohoni kwenye Biblia. Je unaweza kuchukua muda kukumbuka nini tofauti ya karama za rohoni? Jaribu na kuweka listi ya karama nyingi ambayo Roho Mtakatifu anawapa watu wake. Fanyeni kazi kwa pamoja kwenye vikundi vidogo na baadaye pale mwishoni angalia kama kuna yeyote ambayo ulisahau.

(Kumbuka: Kuna listi mwishoni mwa kipindi cha wiki iliyopita kwa marejeo.)

**Karama za rohoni ni za nini?**

Kama kifungu chetu cha Biblia leo kinavyosema, karama za rohoni hupewa kila Moja kwa kipimo tofauti. Inatukumbusha kuwa sisi sote ni sehemu ya mwili moja na karama zetu za tofauti zimetengenezwa na kupewa sifa kwa moja kwa mwingine kwa faida ya mwili wote. Ikiwa tutatumia karama zetu kwa matamanio yetu binafsi, na tukikataa kutumia kabisa, ikiwa tutaiinua karama moja zaidi ya zingine, basi tutakuwa hatutimizi mapenzi ya Mungu kwa kutoa karama mahali pale pa kwanza. Kifungu chetu cha kukumbuka pia kinatukumbusha kutumia karama zetu kwa upendo. Mtazamo wa unyenyekevu na upendo ni jambo la muhimu wakati tukitafuta kuwatumikia hao wanaotuzunguka, ama tunajikuta tunahatarisha na kusababisha ghadhabu na makosa na kweli hatuwakilishi habari njema za Yesu tunazozibeba. Afadhali kutokuwa na kipawa na kupenda, zaidi ya kuwa na vipawa vingi na kujisifu na kuwa mbinafsi.

**Tunatumiaje karama zetu za kiroho?**

Kwanza tunatakiwa kufahamu karama tulizonazo ni zipi, au ni karama ipi tungependa kupokea. Wiki iliyopita tulitazama baadhi ya njia ya kugundua karama zetu, na njia ambazo tutaomba karama. Mara tunapotambua kwamba ni zipi basi tunapaswa kuanza kuzitumia. Hii inaweza kuchukua nguvu kiasi na mazoezi kidogo. Hapa kuna historia nyingine kutoka kwa Hana (tuliyoisikia juu yake mapema):

> Nilijifunza juu ya karama ya kunena kwa lugha mpya ndani ya kanisa na siku zote ilichanganya namna inavyofanya kazi. Niliamua kumwomba Mungu kunipa karama ya kunena kwa lugha ili niweze kutumia lugha hiyo kumwomba Yeye wakati maneno yangu hayatoshi, na pia kama ishara ya Roho Mtakatifu akifanya kazi ndani yangu.
>
> Kwa muda baada ya kuomba hakuna hasa kilichotokea. Niliamua kuomba tena na kusikia Mungu akiniambia, 'Tayari unayo kipawa – unatakiwa tu kutumia!' Mara ya

kwanza nilipo nena kwa lugha kidogo nilikuwa naogopa; nilisikia kuwa na fahamu binafsi kidogo, kwamba inawezekana ninafanya na kufikiria vitu. Hata hivyo, wakati wa kuabudu ndani ya kanisa siku moja niliomba, nilifungua kinywa changu, nikaanza kujaribu kuongea. Kilichotoka nje ni maneno ambayo sikuyajua, na sikujifunza. Nilistaajabu! Kwa sasa ninayo maombi ya lugha ambayo naweza kutumia wakati wowote na katika mazingira yeyote na siyo tu kwamba inanisogeza karibu na Mungu lakini pia inanikumbusha kuwa yeye ni mtoaji wa karama nzuri na anataka kutubariki sisi. Wakati mwingine nanena kwa lugha mara kwa mara kwa undani, wakati mwingine sasa hivi na baadaye. Lakini mara zote najua kipawa kipo hapo: napaswa tu kuchagua wakati wa kukitumia.

30 Dakika

**Shughuli – Habari Njema**

Kifungu chetu cha kukumbuka wiki hii inapendekeza kuwa tutake sana karama ya unabii. Tunaenda kufanya mazoezi itakayotusaidia sisi kuzifahamu hizi karama na kujifunza namna tunavyoweza kuanza kutumia.

Unabii kwa lugha nyepesi ni kusikia kutoka kwa Mungu. Hii inaweza kuwa moja kwa moja toka kwenye neno lake Biblia; inaweza kuhusisha baadhi ya ufunuo juu ya mambo yajayo, kutiwa moyo au hata change moto. Jambo lililo la muhimu ni kuwa linatoka kwa Mungu na linalingana na neno lake (Biblia) na tunachojua kuhusu asili yake.

Utahitaji karatasi na kalamu kwa zoezi hili.

Kila mtu kwenye kikundi achore mzunguko wa mkono wake kwenye kipande karatasi na kuandika majina yao au chora alama utakayotambua juu ya karatasi.

Weka vipande hivi vya karatasi kuzunguka mahali mnapokutana, halafu ulete kikundi pamoja kuomba. Mwombe Mungu

amwezesha kila moja wenu kupokea neno la kinabii kwa moja au watu zaidi kwenye kikundi.

Baada ya kuomba, acha kikundi kigawanyike, msikilize Mungu, halafu nenda na uandike au uchore picha juu ya mkono wa mtu ambayo Mungu ameweka kwenye akili zao. Andika au chora kile unachokihisi kuwa anasema. Inatakiwa tu kuwa neno 1-2, kifungu cha maandiko au picha nyepesi ya kitu fulani. Lenga kufanya hili walao nusu ya wakati uliyonayo leo kuhakikisha kuwa kila moja ana vitu vichache vilivyoandikwa kwenye makaratasi ya mikono yao.

Baada ya kumaliza, kila moja akusanye alichokichora mwenyewe na kusoma kile kilichoandikwa hapo.

Waambie watu washirikishe kitu chochote kinachozungumza nao au kuwatia moyo kwenye zoezi hili.

**Ni wapi nitatumia karama yangu?**

Unaweza kutumia karama yako mahali popote. Kuna watu wagonjwa ndani na nje ya kanisa na kuna watu wanaotaka kusikiliza toka kwa Mungu mahali pote. Jamii zetu zinahitaji viongozi wa ki Mungu, biashara zetu zinahitaji wafanyakazi wanyenyekevu na waaminifu, nyumba zetu zinahitaji wazazi wenye upendo na kuhudumia. Karama za Rohoni hazijaelekezwa kutumika ndani ya kanisa peke yake, hata hivyo wenye akili nzuri na mawazo ya uangalifu hutumika wakati wa kuamua ni wakati gani na ni wapi pa kutumia hizo karama. Wakati wote uwe na muda wa kuomba Mungu moyoni mwako wakati unapohisi inawezekana anakuambia kutumia karama yako kwenye maisha yako ya kila siku. Mwombe pengine kuumba au kuondoa nafasi na kufuata uongozi wake.

Karama za rohoni ni vifaa visivyoaminika kuonyesha nguvu ya Mungu na uwepo wake kwa hao wasiomjua bado. Itahitaji nguvu kiasi kutumia karama hizi ulizopewa, lakini unapochukua hatua

ndogo utamwona Mungu akifanya kazi kupitia wewe na kuwafikia hao wanaokuzunguka na maisha yake.

**Maombi**

15 Dakika

Kwenye kikundi cha watu 3 au 4, tumia muda kiasi pamoja mkimshukuru Mungu kuzungumza na wewe kupitia shughuli mapema kwenye kipindi hiki. Watie wanakikundi moyo kushirikisha maneno yeyote au picha walizopokea ambazo zilikuwa sahihi au kwa wakati kwao. Pia waombee hao walioona mazoezi haya kuwa magumu. Omba kuwa Mungu ataendelea kuwasaidia wao kukua kwenye karama zao.

**Kufanya wiki hii**

Bado kuna ya zaidi sana ambayo tunaweza kujifunza juu ya karama za rohoni. Wiki hii tumia muda pengine wewe mwenyewe au kwenye kikundi kidogo ukijifunza vifungu juu ya karama za rohoni kuendelea. Endelea kumwomba Mungu kufunua vipawa ambazo tayari unazo na pia omba akupe wewe vipawa zaidi unazohitaji. Pia ombeni kwa pamoja kwamba Mungu akupe nguvu kutumia kipawa chochote ambacho tayari unazo.

**Shahidi**


Kama tulivyotaja, vipawa vyetu vinaweza kutumika mahali popote na kuhudumia kama ushahidi wa nguvu na uwepo wa Mungu. Wiki hii mwombe Mungu akupe nafasi kutoka kwa imani na kutumia kipawa alichokupa kumbariki mtu mwingine ambaye bado hamjui yeye.

Omba kila asubuhi, chukua muda kumsikiliza Mungu na uwe tayari kujibu wakati Mungu akikupa nafasi. Pengine akakupa neno la kutia moyo au akili kwa mtu mwingine, au anaweza kukuambia umwombee mtu mwingine kwa ajili ya uponyaji au anaweza kukupa nafasi kuonyesha ukarimu kwa mtu.

Ikiwa unayo wasiwasi, usiogope. Kwa wepesi mwombe Mungu akupe ujasiri!

5

# Kuamini na Imani



'Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote,
wala usizitegemee akili zako mwenyewe;
Katika njia zako zote mkiri yeye,
naye atayanyosha mapito yako.'
Mithali 3:5-6

## Maandalizi

Uwe na:

- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma Kifungu cha Biblia?

## Wakaribishe na Mrejesho

5 Dakika

- Mshukuru kila mtu kwa kufika kwenye kikundi.
- Anza kwa maombi, mepesi mafupi.
- Waulize wanakikundi kama wamefanya 'Kufanya wiki hii' na 'Kushuhudia' kazi toka toka wiki iliyopita.
- Wakaribishe washirikieshe chochote walichokijifunza ama kupata ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

## Lengo

Lengo la kipindi wiki hii ni kuelewa kuwa uzima Mungu aliyotupa inatutegemea sisi kumwamini na kuweka imani kwake, siyo kwenye uwezo wetu.

Kama Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu hawana mashaka kuaminiana na kuwa na imani kila moja kwa mwingine, hivyo tunapaswa kumwamini Mungu kutukuza ndani yake, na kututumia sisi kupitia karama zetu kuleta tofauti kwenye dunia yetu.

## Kifungu cha Kukumbuka

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na marejeo ya Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Soma tena kwenye vifungu vidogo, ukiachia kikundi kurudia kila kifungu baada yako.

Polepole soma kwenye vifungu virefu kikundi kikirudia kila kipande mpaka kila mtu aweze kukariri kifungu chote. Watie baadhi ya watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

> [5]*Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote,*
> *wala usizitegemee akili zako mwenyewe;*

*[6]Katika njia zako zote mkiri yeye,*
*naye atayanyosha mapito yako.*

*Mithali 3:5-6*

**Hadithi**

Soma historia inayofuata juu ya hofu na kuamini kwenye Mlima Mumpu kule Mkushi, Zambia kwenye kikundi. Historia iliandikwa na moja wa waalimu kwenye shule maalum.

Kuna mlima kule Mkushi – moja ya mlima mrefu kule Zambia – na kila mwaka kikundi cha wanafunzi kwenye shule ya karibu ya Kikristo ya Chengelo hupanda kwa pamoja. Jina la mlima ni 'Mumpu Welume', ambao kwenye lugha maalum ya Lala ina maana: 'Mlima wa Shetani'. Ina pango kubwa lenye sura ya mdomo uliyogeuka kwenye jabali upande wa mangaribi. (Mwonyeshe kila mtu picha mwanzoni mwa kipindi.) Mwonekano wa pango hili linainua jina lake na pia kwenye historia nyingi juu ya mlima. Watu maalum wa pale hawapandi kamwe mlima huo na wanaamini kuwa kuna 'roho' ya Mumpu ambayo inahitaji kuridhishwa kwa zawadi ya chumvi, mlo wa mialie na tumbaku kama wataenda kuwinda au kuhamia maeneo.

Ili kikundi chetu kipande Mlima Mumpu wanapaswa kwenda moja kwa moja kwenye pango, kupitia mdomo wa shetani! Kuzunguka kambi ya moto wakati wa usiku kabla ya kutoka, kikundi chetu cha vijana husikiliza kwa makini historia ya Mlima Mumpu. Macho yao hupanuka ninapowaeleza juu ya roho ya milimani inayoishi ndani ya pango. Wakati historia yote imekamilika utakachosikia ni upepo ukivuma kupitia juu ya miti na miali ikiwaka na kusambaa ndani ya matawi inayozunguka ya moto.

Ni kwa wakati huu ndiyo nimewauliza wao, 'Unaweka imani yako kwa nani?' Ghafla ikawa ni hali halisi, mazingira halisi. Kikundi kikajaa hofu ya wazi yam lima, ya giza, bado walijua kuwa Yesu Kristo alisema yeye ni nuru ya ulimwengu. Wangeweka imani yao kwa nani? Mazingira yangeweza kuwalazimisha vijana hawa kuogopa au kuweka imani yao kwa mababu na maroho, lakini

kuamini na imani ndani ya Mungu inaenda zaidi ya mazingira na hofu. Wakati tumeketi kuzunguka kambi ya moto, tulifanya uamuzi wa pamoja kwamba hata katika mazingira haya yasiyo ya kawaida; tunaweka imani yetu kwa Mungu. Tuliomba ulinzi wake tukijua kuwa ni mwenye enzi.

Mwaka moja kikundi cha wanafunzi walichukua mvuko mpana kupitia kwenye pango na kwenye kilele cha Mlima Mumpu. Walipanda kwenye kilele cha mlima kwa sababu pamoja na jina lake, Mlima Mumpu ni mlima wa Mungu kama vilivyo vitu vingine vyote duniani. Ni mlima wake na hatupaswi kuogopa tunapoupanda! Kikundi hicho cha vijana walipenda matukio ya kuona juu ya miteremko ya miamba, wakigombania kupita ndani ya pango na msisimko wa kilele, kama inavyokuwa tunapomwamini yeye kwenye matukio haya ya maisha.

**Kujifunza Biblia**

Soma Matayo 14:22-33 kwenye kikundi:

> *[22]Mara akawalazimisha wanafunzi wake wapande katika
> mashua na kutangulia mbele yake kwenda ng'ambo, wakati
> yeye alipokuwa akiwaaga mkutano. [23]Naye alipokwisha
> kuwaaga makutano, alipanda mlimani faraghani, kwenda
> kuomba. Na kulipokuwa jioni, alikuwako huko peke yake.
> [24]Na ile mashua imekwisha kufika katikati ya bahari,
> inapigwa sana na mawimbi; maana upepo ulikuwa
> unawakabili.*
>
> *[25]Hata wakati wa zamu ya nne ya usiku Yesu akawaendea,
> akienda kwa miguu juu ya bahari. [26]Wanafunzi
> walipomwona akitembea juu ya bahari, wakafadhaika,
> wakisema, ni mzimu; wakapiga yowe kwa hofu.*
>
> *[27]Mara Yesu alinena, akawaambia, Jipeni moyo, ni mimi;
> msiogope. [28]Petro akamjibu, akasema, Bwana, ikiwa ni
> wewe, niamuru nije kwako juu ya maji.*

*29Akasema, njoo.*

*Petro akashuka katika mashua, akatembea juu ya maji, ili kumwendea Yesu. 30Lakini alipouona upepo, akaogopa; akaanza kuzama, akapiga yowe, akisema, Bwana, niokoe.*

*31Mara Yesu akanyosha mkono wake, akamshika, akamwambia, Ewe mwenye imani haba, mbona uliona shaka?*

*32Nao walipopanda katika mashua, upepo ulikoma. 33Nao waliokuwamo ndani ya mashua wakamsujudia, wakisema, Hakika wewe u Mwana wa Mungu.*

Kwenye kifungu hiki tunamwona Petro, msukumo ukijianzia kwa Petro, akiitikia mwito wa Yesu. Yesu kwa muujiza aliwalisha watu zaidi ya 5,000 na aliwatuma wanafunzi kwenye na boti wakati alipolitawanyisha kundi. Baadaye alichukua muda kidogo tena na Baba yake Mungu kwenye maombi upande wa mlima. (Hii ni kwa sababu binamu wake Yohana Mbatizaji hivi karibuni aliuwawa na alikuwa kwenye huzuni.)

Ilianza kuwa giza na boti ilikuwa mbali kwenye ziwa wakati Yesu akitembea juu ya maji kuwaendea wanafunzi wake. Wanafunzi walitishwa na hiyo sura iliyotembea juu ya mawimbi ikiwaendea. Fikiri mwenyewe ukiwa kwenye hali hiyo: unaweza kuogopa pia?

Yesu aliwapa uhakika akiwaambia wasiogope maana ni yeye. Petro mara moja akajibu, akiwa amejaa imani na kumwamini: 'Ukisema nije, nitakuja!' Tunaweza kuwa na msukumo kama huo, imani ya Petro ni kama ya mtoto maana bila kuarajiwa alishuka upande mwingine wa boti kukutana na Yesu juu ya maji?

Bado mwanzo huo mzuri mapema ulififia baada ya Petro kuona mashaka ya hali, mawimbi na upepo, akaanza kuzama. Sisi pia tunafanana na hao wafuasi wa Yesu! **Ni mara ngapi tumeitikia wito wa Yesu na imani kubwa na uhakika, na kujikuta**

**tunatazama hali pekee inayotutatiza, tunakuwa tumechoka na changamoto, na kuanza kuzama?**

Petro alifanya kitu ambacho kila moja wetu angeweza kufanya wakati vichwa vyetu vikianza kuzama ndani ya maji ya majaribu ndani ya maisha yetu: alimlilia Yesu. Yesu alimfikia na kumvuta nje. Yesu bado akampa Petro changamoto (kifungu 31) akimuuliza kwa nini aliona shaka, swali hilo hutuuliza sisi tunapokua kwenye hali hiyo. Kwa nini tunaona mashaka?

Sidhani kuwa Petro kwa wakati huo alipoteza imani yake. Yesu hakuwaza hilo pia; alianza tu kuona mashaka. Kwenye Marko 9:24 tunasoma habari ya baba moja ambaye mtoto wake alikonda na kupagawa na mapepo na amekuwa hivyo kwa maisha yake yote. Baba yake akasema, 'Ninaamini; nisaidie kutokuamini kwangu!' Tunaweza kuelewa namna Petro na baba yule walivyojisikia. Tunayo imani kwa Mungu na kumwamini yeye, lakini bado hali zetu inashusha imani na kuleta mashaka kuwa Yesu atafanya kile alichosema.

Hata hivyo, inawezekana hii ni shida tunakabiliana nayo kwa kuamini: kuamini siyo juu ya Mungu kufanya tunavyotaka, ni juu ya kumwamini Mungu kwa kile anachotaka! Kuamini na Imani siyo kitu tu ambacho ni uamuzi wa mara moja tunaofanya mwanzoni mwa safari yetu ya Kikristo; ni maamuzi ya kila siku tunayofanya. Kwenye Luka 9:23 Yesu alisema, 'Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwikemsalaba wake kila siku anifuate'. Imani ni uamuzi wa kusema kila siku, 'Leo Yesu nakuamini kwa kila kitu'.

Katikati ya kujaribu mazingira imani inasema, 'Bwana naweka imani yangu kwako' na kufikiri hilo na kulifanyia kazi. Chini ya Mlima wa Mumpu kwenye historia, tunaweza kusema, 'Bwana naweka imani yangu kwako!' Mara zote napenda kusoma Yoshua 24 kwa wakati huo kwa sababu kwenye kifungu 15 Yoshua anasema, 'Chagueni hivi leo mtakayemtumikia'. (Unaweza kusoma historia baadaye ukitaka.) Tunapaswa kuamua hilo kila

siku. Imani yetu huanza kujengeka na kukua tunapopata ujuzi wa matokeo ya imani ya kila siku na kuamini. Tukimkabidhi yeye mapenzi yetu tutauona uaminifu wa Mungu na kukuza imani zaidi kwa jaribio lingine. Uzima ambao ameweka ndani yetu huanza kukua tunapiweka kwenye matendo.

Hata kushindwa kwetu, ikifanana na ujuzi wa Petro kwenye kifungu, itajenga imani yetu kwa mambo ya baadaye. Petro alijenga imani yake kwa Yesu kwa kumwamini na kutoka nje ya boti. Baadaye Yesu alimwita Petro 'mwamba' wa kanisa (Matayo 16:18). Mwamba niktu kilichoi maranahakitingishiki. Mwamba ni ktu kilicho imara na hakitingishiki, kama mwamba ambao sisi, na wengine, tunaweza kusimama.


Petro alijua tabia ya muhimu ya Yesu ambayo kwa kawaida inaonekana kushindwa kwa wengi, kwamba wakati tunaposhuka kwenye boti na kumwamini yeye, siku zote atakuwa hapo kutufikia sisi na kututoa. Hiyo ndiyo asili ya Yesu. Matamanio yake ni kuwa mioyo yetu isisumbuke, kuwa tunapaswa kumwamini Mungu na kumwamini yeye (Yohana 14:1). Matamanio ya Yesu kumwamini yeye ni kila kitu kwetu. Bado, kumwamini huku siyo jambo analotulazimisha; inatakiwa kuwa maamuzi yetu na kwa hili ndivyo uhusiano unavyojengwa juu ya upendo wa kazi. Tunaitikia wito wake kwa kumwamini yeye kila siku, Yesu hutujibu sisi na upendo uliyotunzwa wa milele na kututia moyo sisi kutokuwa na mashaka naye. Tunaweza kumwamini, kwa uaminifu wake.

10
Dakika


**Shughuli**

Njia nzuri ya kudhihirisha namna kuamini inavyokuza na kujenga ni mduara wa kuaminika.


Waambie watu kuunda vikundi vya watu 6, 7 au 8 kwenye kikundi. Kila kikundi inapaswa kuunda mduara kwa kusimama bega kwa began a moja kwa mwingine.



Mtu moja anapaswa kusimama katikati ya kila mduara. Mtu aliyeko katikati anapaswa kukunja mikono yao kifuani na kusimama wima kama ubao wa mbao.



Wengine kwenye mduara waweke mikono yao miwili mbele yao na kuweka mguu moja mbele (bado bega kwa bega kwa mduara uliyobaki). Mtu aliyeko katikati, wakinyoosha miguu yao kama ubao wa mbao, ukiegemea juu ya mikono ya watu walioko kwenye mduara. Watu walioko kwenye mduara kwa polepole wamsukume mtu aliye katikati kuzunguka mduara. Wazo SIYO kumfanya mtu aliyeko kwenye mduara kuanguka, siku zote wasaidie.



Hii hujenga imani kwa mtu aliyeko katikati kwamba atawaamini wengine kwenye mduara na wengine kwenye mduara kudhibitisha uaminifu wao!

- Muulize mtu aliyeko katikati walijisikiaje?
- Ilikuwa ni rahisi kuamini?
- Shughuli hii inahusianaje na sisi kumwamini Mungu?

?

15 Dakika

**Maswali**

Kwenye vikundi vya watu 3 au 4 mjadili maswali haya na vifungu ndani ya Biblia. Baada ya majadiliano, ruhusu muda kwa vikundi kutoa mrejesho kwenye kikundi chote.

- Luka 17:1-10 Tunajengaje uaminifu wetu na imani? Ufunguo ni upi?
- Marko 9:14-29 Maelezo yaliyotolewa na baba kwenye kifungu 24 inaonyesha kujipinga wenyewe. Tutaaminije (kuamini) na bado tunataka kushinda kutokuamini (upungufu wa kuamini)? Unayo mifano ya jambo hili kwenye maisha yako mwenyewe?
- Ni hali zipi zinasababisha mashaka na kushindwa kumwamini Mungu?
- Majibu yetu yanapaswa kuwaje?
- Kushindwa kwetu inajengaje imani yetu?

- Ina maana gani kujikataa wenyewe na kuchukua msalaba kila siku?

**Maombi**

10 Dakika

Kwenye kikundi chako kidogo, tumia mawazo hapo chini kumshirikisha Mungu kwa ukweli juu ya kuamini kwako na imani. Chukua muda kuomba na kuombea wengine pia, kuwatia moyo wengine kujenga kuamini na imani yao.

Hapa kuna baadhi ya mawazo ya namna ya kuomba:

- Bwana nakuamini; nisaidie kushinda mashaka na kukosa kuamini.
- Tubia maeneo ya mashaka, hofu na kukosa kuamini.
- Mwombe Mungu akusaidie kushinda maeneo hayo, kwa nguvu na uwezo kupitia Roho Mtakatifu wake.
- Mwombe Mungu kwa hali yeyote maalum unayokabiliana nayo sasa ambayo inahitaji imani na kuamini zaidi ya kawaida. Omba akutie nguvu.
- Waombe wengine wakuombee kwenye hali hizo pia.
- Omba uweze kutumia kushindwa (weka wazi kama unataka) kwenye maisha yako kujenga imani yako.

**Kufanya wiki hii**

Kila wiki kuna kazi ya nyumbani sisi kufanya. Wiki hii soma Waebrania 11. Chukua tabia moja kwenye listi ya watu wa imani. Andika chini au kumbuka mifano 5 ya namna walivyomwamini Mungu. Halafu kutana na mtu mwingine kwenye kikundi na kujadili maswali haya pamoja.

- Unaweza kuingiza moja ya mifano hii kwenye maisha yako wiki hii?
- Unawezaje kumwamini Mungu zaidikwenye maisha yako?
- Unawezaje kushinda kupungukiwa kwa kuamini?
- Unawezaje kumtia mtu mwingine moyo wiki hii kumwamini Mungu?

**Shahidi**

Uzima wa Mungu ndani yetu ina maana kuwa tumebadilishwa ndani inayoongoza mabadiliko kwenye matendo yetu ya utendaji pia. Watu wanaotuzunguka wataona haya mabadiliko ndani yetu.

Wiki hii, fikiri juu ya hali ya kumwamini mtu fulani au kitu zaidi ya kumwamini Mungu. Ombea hali hiyo, umpe Mungu. Amua kumwamini Mungu zaidi ya mtu au vitu ulivyokuwa unaviamini. Sasa badilisha namna unavyotenda ufanane na uamuzi uliyoamua kumwamini Mungu.

Kwa mfano, labda umekuwa ukimwamini jirani au rafiki kukufanyia kazi fulani. Wakati mwingine wana mambo mengi ya kufanya. Kwa kawaida wakikuambia hawawezi kukusaidia, unapanik na kusema vitu kwa marafiki zako kujaribu kuwashawishi wao kupata muda wa kufanya kazi hiyo. Wiki hii, ikiwa rafiki yako hana muda wa kukusaidia, kumbuka kuwa unamwamini Mungu kukusaidia badala yake. Omba maombi ya haraka kwenye moyo wako, halafu unaweza kuwashukuru marafiki zako kwa wakati mwingine kukusaidia na uwaambie kuwa unaelewa kuwa hawawezi kukusaidia wiki hii. Mwombe Mungu akusaidie kufanya kazi mwenyewe au amtume mtu kukusaidia!


Mfano mwingine ni kuamini pesa badala ya kumwamini Mungu. Ukijikuta mwenyewe unaamini pesa kutatua matatizo yako zaidi ya kumwamini Mungu, omba juu yake na utoe pesa kwa mtu mwingine mwenye mahitaji zaidi yako. Mwombe Mungu akupe mahitaji yako. Mwamini yeye.

Kwa kutenda tofauti, unajiweka mwenyewe kwenye hali ya kumwamini Mungu. Unampa pia Mungu nafasi kuonyesha jinsi anavyoweza kuaminika. Watu wengine watona jambo hilo kwenye maisha yako.

# Kumbukumbu

6

# Vita vya Kiroho



'Mwizi huja tu kuiba, kuua na kuharibu; mimi nilikuja ili wawe na uzima, tena wawe nao tele.'
Yohana 10:10

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma Kifungu cha Biblia?

**Wakaribishe na Mrejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila mtu kwa kufika kwenye kikundi.
- Anza kwa maombi, mepesi mafupi.
- Waulize wanakikundi kama wamefanya 'Kufanya wiki hii' na 'Kushuhudia' kazi toka toka wiki iliyopita.
- Wakaribishe washirikieshe chochote walichokijifunza ama kupata ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kuelewa kuwa wakati tunapokea maisha mapya toka kwa Mungu, tunaingia pia kwenye vita kinyume na nguvu za kiroho zinazompinga Mungu. Mungu tayari ameshazishinda hizo nguvu; hata hivyo, bado zinaweza kuonyesha baadhi ya vizuizi ambazo tunaweza kuzishinda kwa maombi, kuabudu na metendo yanaonekana.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Tayari umekwisha jifunza sehemu ya kifungu cha kukumbuka cha leo kwenye kipindi cha kwanza ya ***Misingi 1: Maisha Huanza*** tulipojifunza kuwa Yesu alikuja kutupa sisi maisha mapya. Kifungu cha kukumbuka cha leo ongezea kwa yale uliyojifunza kabla.

Soma kifungu cha kukumbuka na marejeo ya Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Soma tena kwenye vifungu vidogo, ukiachia kikundi kurudia kila kifungu baada yako. Poleploe soma kwenye vifungu virefu kikundi kikirudia kila kipande mpaka kila mtu aweze kukariri kifungu chote. Watie baadhi ya watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

*Mwizi huja tu kuiba, kuua na kuharibu; mimi nilikuja ili wawe na uzima, tena wawe nao tele.*

*Yohana 10:10*

**Hadithi**

Wasomee hadithi inayofuata kikundi:

Kwa kadri alivyomkumbuka Marina amesikia sauti kwenye kichwa chake. Wakati mwingine anazisikia sana na kwa wakati mwingine kidogo. Alipokea matibabu kwa madaktari kwa hali hii, na ingawa imesaidia kidogo, sauti hizo hazikuondoka kabisa. Sauti hizo humwambia vitu kumhusu yeye mwenyewe, juu ya wengine na wakati mwingine humpa maagizo namna ya kutenda. Kwa nyakati nyingine wamemwambia kujiumiza mwenyewe, au wengine.

Hata hivyo hivi karibuni, Marina alipokea maisha mapya toka kwa Mungu na kuwa Mkristo ikiwa na maana kuwa ameanza kusoma Biblia. Kwenye Biblia alipata ukweli wa aina nyingi wa kuhusu yeye ni nani kama mtoto wa Mungu, na pia namna ya kutenda tunapopokea maisha mapya. Alianza kutambua kuwa sauti alizokuwa akizisikia hazikumweleza juu ya kweli ya Mungu kumhusu yeye au kuhusu hali yake. Aliamua kuandika chini baadhi ya vifungu toka kwenye Biblia na sasa akisikia sauti anazijibu kwa kweli ya Mungu, akisimama imara kwenye neno lake na kwa ahadi alizompa yeye. Hii inamsaidia yeye kila siku.

(Magonjwa ya akili yanaweza kuwa magumu sana kwa hao wanaoteseka nayo na kwa watu wanaowazunguka. Mara nyingi inakuwa vigumu na hatuwezi kubuni kuwa kilichomsaidia mtu mwingine kinaweza kuwasaidia wengine. Uponyaji unaweza kuja kwa muujiza au kwa matibabu ya kitabibu.)

**Kujifunza Biblia**

Soma Waefeso 6:10-18 kwenye kikundi:

*[10]Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika*
*uweza wa nguvu zake. [11]Vaeni silaha zote za Mungu, mpate*

*kuweza kuzipinga hila za Shetani. 12Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. 13Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama. 14Basi simameni, mkiwa mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani, 15na kama viatu vilivyofungiwa miguuni mwenu muwe tayari kutangaza Injili ya amani; 16zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. 17Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu; 18kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote.*

Biblia iko wazi kuwa shetani, ingawa ni adui mjinga, yeye ni adui aliyeshindwa. Alishindwa baada Yesu kufa msalabani na kufufuka, lakini amebaki na upuuzi mwingi mpaka Yesu atakaporudi. Jinsi tunavyozidi kumkaribia Bwana wetu Yesu Kristo, tunakuwa na ujuzi na kuwa mstari wa mbele kwenye mapambano.

Mtume Paulo, mwandishi wa nyaraka kwa Waefeso, anaandikia kusanyiko lake juu ya vita walivyomo wakitumia sura ambayo wanaweza kufanana na – hizo za askari wa Kirumi. Anawapa wasomaji wake mawazo fulani namna ambavyo wanaweza kupigana kinyume na mbinu za huyo mwovu.

Kwa njia hiyo ya askari kwenye uwanja wa vita hatadumu sana ikiwa yeye atasahau kuwa yuko vitani, hivyo hata sisi tunapaswa kuwa macho na kujiandaa kukabiliana na mwovu huyo nyakati zote.

**Maswali: Tunapigana na nani?**

Soma Waefeso 6:10-12 kwenye kikundi:

10
Dakika

> *[10]Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. [11]Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani. [12]Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.*
>
> *Waefeso 6:10-12*

Waambie kikundi wakuambie nani au nini wanachofikiri kuwa maadui zetu. Unaangalia majibu yafuatayo:

- Kanuni
- Mamlaka
- Nguvu
- Ulimwengu wa roho wa mashetani

Waulize kikundi wanafikiri nini maana ya vitu hivi. Mjadili mahali vita inapopiganwa na wanafikiri hii inaweza kuwa na maana gani.

Hatua yetu ya kwanza ya mafanikio ya kupiga maadui zetu wa kiroho ni kutambua madhaifu yetu na uwezo mkubwa wa nguvu za Yesu. Tukijiamini sisi wenyewe, tunataka kushidwa kwa sababu tuko dhaifu. Kumtegemea Yesu ni lazima. Kumwabudu Yesu na kujitoa kwake ni namna ya ufunguo wa vita vya kiroho na kupitia kuabudu tunajikumbusha wenyewe na adui kutambua Yesu ni nani na kile alichofanya.

Kifungu hiki kinarudia kutukumbusha sisi kutokuwa na uwezo kipigana wenyewe. Tunahitaji uewzo wa nguvu (kifungu 10), silaha (kifungu 11 na 14-17) na kuunganisha mawasiliano na Mungu kutusaidia sisi (kifungu 18-20). Bila vitu hivi hatutaweza kusimama kinyume na adui. Kuachiwa sisi wenyewe mapema tutafikicha kwenye joto la vita. Kwa urahisi hatutatosha kwa kazi hiyo. Hata

hivyo, Mungu anawapenda watu wake na kamwe hatawaacha bila ulinzi.

Kwenye kifungu cha 10, Paulo anatambua kuwa tuko dhaifu na wakati maisha yanapokuwa magumu tunataka kuachana nayo. Vita hivi vya kiroho siyo vita rahisi lakini kama tulivyosema kabla tayari Yesu alishashinda. Yeye ndiye nguvu yetu na tunapaswa kumtegemea yeye na nguvu zake.

Picha ya askari hutusaidia sisi kuelewa silaha gani tutatumia kupigana nayo. Askari havai kama raia, lakini huvaa magwanda na kubeba silaha kujinda kinyume na adui. Kifungu cha 11 kinatuambia kuwa kama Wakristo tunapaswa kuvaa kama askari, kuvaa ‘silaha zote za Mungu’ kuwa tayari kupigana. Tunapaswa kusimama na Mungu na tusishindwe na mbinu za adui.

Tunapoona au kufikiri kuwa tuko kwenye hatari, haraka sana tunakuwa kwenye ulinzi wetu; kifungu hiki kinatuambia sisi namna ya kujilinda wenyewe na pia inatoa mapendekezo namna tunavyoweza kupigana kinyume na kazi za shetani. Tunayo mamlaka kufanya hivyo. Wakati mwingine vita hivyo vinaweza kuwa wazi, wakati mwingine vita vinaweza kuendelea ndani ya mioyo yetu au akili zetu. Kifungu 13 inatutia moyo sisi kwa kutukumbusha sisi kuwa Mungu hakutuacha kupigana wenyewe; badala yake ametupa sisi ulinzi na silaha tunazohitaji kutusaidia sisi kusimama imara ndani yake. Tunaenda Kuangalia kila moja sasa.



15 Dakika

**Shughuli – Silaha za Mungu**

Unapozungumzia kila kipande cha silaha ambazo Mungu ametupa, inatia watu moyo kufanya tendo itakayowasaidia kukumbuka. Kwa mfano, unapozungumzia juu ya mkanda wa kweli, kila moja anatakiwa kusimama na kujifanya kufunga mkanda kuzunguka kiuno. Waambie kutumia mawazo yao!

**Mkanda wa kweli**

Mkanda hufanya nini? Inashika suruali yako. Inatoa sura kwa vazi lako. Kwenye kesi ya askari wa Kirumi, inamruhusu yeye kubeba silaha – hanjari. Kwa kuamini ukweli kuwa Yesu alikufa msalabani na kuwa hai tena siku ya 3 kulingana na msingi wa imani yetu. Adui shetani anataka kutudanganya juu ya kweli ya Yesu. Kuamini na kushikilia kweli aliyotupa Yesu huipa maisha yetu sura na sababu ya kufanya vile tunavyofanya.

**Dirii ya haki**

Dirii hutumika kulinda kifua chako, ambayo hutunza moyo wako. Haki husimamia uhusiano wetu na Mungu na sisi kwa sisi. Shetani anataka kuharibu uhusiano wetu na Mungu na sisi kwa sisi ili tujisikie wapweke kwenye safari yetu ya maisha. Tunaweza kutunza mioyo yetu kwa kulinda uhusiano wetu na Mungu. Hii ina maana ya kuwa na muda wa kuzungumza naye kwa maombi, kusoma neno lake na kutiana moyo sisi kwa sisi.

**Miguu iliyovikwa utayari tupatao kwa Injili ya amani**

Miguu yetu hutupeleka tunakotaka kwenda. Mungu ametuagiza kupeleka habari njema hadi miisho ya dunia. Tuhakikishe kuwa tuko tayari kwa kufanya mazoezi kusema historia yetu wenyewe namna tunavyomjua Yesu na kujiandaa kueleza jinsi Mungu alivyobadilisha maisha yetu. Wakati mwingine ushuhuda wetu unaweza kuwa ushuhuda kimya wakati watu wanaangalia maisha yetu. Injili ya amani ni injili ya umoja na kukaa pamoja. Adui shetani anataka kuleta faraka na mabishano. Kwa kutembea karibu na Yesu, tunaweza kuleta umoja na kuwa pamoja kila

tunakoenda na kueneza habari yake njema. Tunaweza kuwa na sehemu kwa matendo ya upendo ambayo itageuza kazi za shetani.

**Ngao ya Imani**

Kubeba ngao inatueleza kuwa tunashambuliwa. Mashambulizi yanaweza kutokea upande wowote – juu, katikati, chini, pande zote – na tunaweza kutumia ngao kujilinda. Askari wa Kirumi waliunganisha ngao zao pamoja kujenga ukuta na kujilinda wenyewe na wengine.

Adui shetani atafanya kila analoliweza kutufanya kuwa na mashaka na kweli ya Mungu, lakini imani yetu katika Mungu itatulinda na wengine, kwa hali yeyote tutakayo jikuta ndani yake. Maana ya imani ni kufanya maamuzi ya kumwamini Mungu.

**Chepeo ya wokovu**

Chepeo, inaongeza kulinda kichwa chako, husaidia kutambua uko kwenye jeshi lipi. Ni kitu cha kwanza kutambua wakati unalindwa. Chepeo yetu ya wokovu huonyesha dunia kuwa sisi ni jeshi la Mungu. Adui shetani anataka kutuangusha chini kama Wakristo, lakini wokuvu wetu uko salama ndani ya msalaba wa Yesu. Haijalishi tunapambana na nini, hakuna kitakachotutenga na upendo wa Mungu na kuchukua wokovu wetu.

**Upanga wa Roho**

2 Timoteo 3:16 inasema, 'Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadabisha katika haki'. Tunaweza kutumia neno la Mungu kumshambulia adui kama tunavyoweza kutumia upanga kumshambulia adui.

Hiki ndicho kinachotokea kwenye historia yetu kwa Marina kutumia kweli ya neno la Mungu kuja kinyume na zile sauti. Ni silaha ambayo Yesu alitumia alipojaribiwa na shetani. Unaweza kusoma zaidi juu ya haya kwenye Luka 14:1-12.

**Maombi**

Kifungu kinamalizia kwa kutuambia kuomba wakati wote. Mahali popote ulipo, kile unachokifanya au kufikiri, maombi ni silaha yenye nguvu ya yote. Tunaweza kuzungumzia juu ya ushindi wetu na mapambano yetu kwa Mungu anayeelewa. Yesu siku zote hutuombea kwenye uwepo wa Baba yetu Mungu.

**Maswali**

10 Dakika

Kwenye kikundi cha watu 3 au 4 jadilini njia ambayo tunaweza kutambua adui yetu na kujadili njia ya kutumia silaha za Mungu kwa kujilinda. Maswali yafuatayo yanaweza kusaidia:

- Unaweza kufikiri juu ya mfano wa uongo umeleta shida?
- Unaweza ukafikiri muda ambao uhusiano ulivunjika na ikaleta maumivu?
- Unaweza kufikiri wakati ambao umejikuta kuwa na mashaka kusema je Mungu ni mzuri?
- Katika kila hali hizi, fikiri kama kulikuwa na hali ya kiroho iliyoelekeza mateso na maumivu.
- Katika kila hali hizi, ni sehemu gani ya silaha ingeweza kusaidia?
- Ni tendo gani tunaweza kuchukua 'kuvaa silaha zote za Mungu'?

**Shughuli**

5 Dakika

Mwambie mtu fulani asome Waefeso 6:14-18 kwenye kikundi. Wakati inasomwa, mwambie kila mtu kusimama na matendo yote tofauti yaliyofanywa kuwakilisha sehemu tofauti ya silaha.

**Maombi**

10 Dakika

Soma maombi haya haya, na kuambia kikundi kurudia baada yako. Unaweza kuwatia moyo kufanya matendo yanayoonekana toka kwenye kifungu cha kukumbuka kama ishara ya kuvaa silaha.

> Baba yetu wa Mbinguni, najua kutoka kwa kazi za Yesu Kristo kwamba shetani na wafuasi wake ni maadui walioshindwa. Najua pia kutoka kwa neno lako, Biblia, kuwa adui anaendelea kunguruma kwenye dunia na kutushambulia. Yesu, naomba msaada wako kwa kuvaa silaha zako – chepeo ya wakovu, dirii ya haki, ngao ya imani, utayari tupatao kwa injili ya amani, mkanda wa kweli, na upanga wa Roho ili kuweza kumpinga adui aweze kukimbia.
>
> Nakusifu Yesu, kwa ushindi wako juu ya adui, maana ameshindwa, nadai huo ushindi kwangu mwenyewe wakati nabaki kwako. Amen.

Baada ya kuvaa silaha zote za Mungu tunapaswa pia kugeuka kwa kila kinachotufunga au uhusiano wowote tuliokuwa na shetani, kwa kujua au kwa kutojua. Mfano wa hizi ni kuapiza, laana, kwenda kwa waganga wa kienyeji au kujihusisha na dini za uongo. Ni muhimu sana kumwomba Mungu akusaidie uwe huru na kutembea huru. Hii inaweza kuhusisha toba ya hofu, toka kwenye kifungo hadi kwenye nguvu ya asili au toka kwenye roho chafu ambayo siyo Roho Mtakatifu.

Sasa tutaenda kuwa na nafasi ya kugeuka mbali na kitu chochote kilichoshika maisha yetu. Tutaenda kufanya haya kwenye vikundi vyetu. Kama kuna kitu ambacho huwezi kushirikisha kwenye kikundi chako lakini amini Mungu anataka kukuweka huru, unaweza kusema vitu hivyo kimya ndani ya moyo wako (badala ya kutamka kwa sauti) au unaweza kuongea na kiongozi wa kikundi baada ya kipindi.

Pamoja na watu kwenye kikundi, ongoza kila mtu kwenye maombi ambayo itamgeuza kutoka kwenye kitu kilichomfunga kwenye maisha.

> Bwana Yesu, ninatamka mambo yafuatayo:

(Waalike watu kusema kwa sauti au kimya ndani ya mioyo yao kitu chochote wanachokijua kwenye maisha yao ya kishetani au makosa.)
Ninakupa vitu hivi, Bwana.
Aksante kwa kuniweka huru.
Amen.

Wakati kikundi kinafanya haya, unaweza kugundua kuwa baadhi ya watu wana ugumu mkubwa kugeuka toka maeneo tofauti, kama hawawezi kutamka maneno toka kwenye midomo yao. Wengine wanaweza kuwa na hisia kali. Unaweza kuona baadhi ya watu wakianza kuonyesha tabia za kawaida; ni kama roho anajidhihirisha ndani yao. Kila kinachotokea, kumbuka kuwa Yesu Kristo ndiye mtawala. Usiogopeshwe wala usitishwe. Mkemee pepo atulie na kutoka nje ya mtu kwa jina la Bwana Yesu. Hatuwezi kufanya mambo haya kwa uwezo zetu; ni kwa nguvu za Yesu tu.

Baada ya roho kuondoka au mtu aliyevunjika moyo akapata utulivu, ni wakati wa kumwomba Roho Mtakatifu kuja na kumjaza mtu huyo afurike. Hii ni muhimu na itatoa uhakika kuwa mtu huyu atatembea na uhusiano na Yesu.

**Kufanya wiki hii**

Wiki hii rudia matendo uliyofanya juu ya silaha kila asubuhi mara unapoamka. Mwombe Yesu akusaidie kuona kila shambulizi toka kwa adui na utumie silaha ulizovaa. Hapa kuna mifano ya hii ina maana gani:

- Unaposikia uongo, ongea kweli.
- Ukiwa na mashaka juu ya uzuri wa Mungu, soma kifungu kwenye Biblia inayokukumbusha juu ya kweli.
- Kama uhusiano wako na Mungu au na mtu mwingine siyo mzuri, uwe na muda wa kusema samahani naurekebishe iwe sawa.
- Ukijisikia kuogopeshwa, omba.

**Shahidi**

Wingi wa silaha tunazopewa na Mungu ni za kujilinda wenyewe kutokana na mashambulizi. Kuna moja ambayo ni tofauti. Tumeambiwa kuhakikisha tumevikwa utayari tupatao kwa injili ya amani. Hii ni juu ya kutoka kushuhudia habari njema za Yesu na wengine.

Wiki hii panga muda kuomwombea mtu asiyemjua Yesu, mazingira ambapo amani ya injili haipo au mahali ushetani ni dhahiri. Mwombee mtu huyo na mazingira na mwombe Mungu abadilishe. Baada ya kuomba, nenda na kuongea na mtu huyo au tafuta kuleta amani kwenye mazingira hayo. Nenda na amani na ushirikishe amani.

Kumbuka KUMWAMINI Mungu unapofanya hayo. Huwezi kufanya haya kwa uwezo wako. Unatakiwa kumtegemea Mungu – Hivi ni vita vya kiroho!

**Kuchagua Kuendelea Kusoma**

Ikiwa watu wana muda na wanayo Biblia (au rafiki na Biblia) hapa kuna vifungu vya ziada wanaweza kusoma kuwasaidia kutambua kazi za shetani na za Mungu:

**Kazi za shetani**[2]

- Yohana 10:10 Uharibufu na kifo
- Luka 22:31; Ufunuo 2:10-11 Mateso
- Matayo 4:1; 1 Wakorintho 7:5 Majaribu

**Kazi za Mungu**

- Yohana 10:10 Uzima tele
- Zaburi 9:9 Ngome wakati wa shida
- Yakobo 1:13 Mungu hajaribu

---

[2] Shule ya Theologia ya Brisbane (2013). *Siri ya vita vya kiroho: Namna ya kuangamiza mwili, kushinda dunia, na kukemea mapepo!* [kwa mtandao] inapatikana: http//bst.gld.edu.au/wp-content/uploads/2013/08/SpiritualWarfare%20PowerPoingt.pdf [Accessed 6 July 2018]

- Yohana 13:2; Luka 22:3 Kumsaliti Yesu au Wakristo
- Mwanzo 3; Matendo 5:3; 2 Wakorintho 2:9-11; Waefeso 6:11 Mbinu na Udanganyifu
- Matayo 16:22-23 Kupinga na kukataa msalaba, kuchukua njia rahisi
- Matayo 4:8-10 Kuabudu vitu vingine pamoja na shetani
- 2 Wakorintho 11:14; 2 Wathesalonike 2:9 Akionekana kama malaika wa nuru (tabia ya uongo, ushawishi)
- 1 Wathesalonike 2:18 Kuaribu kazi za injili
- (Historia ya) Ayubu Kusaliti na kuangamiza

- Kumbukumbu la Torati 7:9 Mungu ni mwaminifu
- Yohana 14:6 Yesu ndiye kweli
- Matayo 7:13 Kuchukua njia nyembamba, njia ngumu, na kumpokea Yesu aongoze maisha
- 1 Mambo ya nyakati 16:25; Kutoka 20:2-3 Mwabudu Mungu peke yake.
- 1 Yohana 4:7-21; 1 Wakorintho 13:4-8 Mungu ni pendo.
- Warumi 1:16 Injili ni nguvu ya Mungu.
- (Historia ya) Ayubu Uaminifu Uumbaji, na Mungu wa Baraka.

# Kumbukumbu

7

# Kuombea Jumuia yetu



'Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote.'

1 Timotheo 2:1

**Maandalizi**

Unachohitaji kwenye kipindi hiki:

- Kipande cha karatasi pana, au baadhi ya vipande vidogo unavyoweza kugundisha pamoja.
- Kalamu ya alama au kalamu nene.

Uwe na:

- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma Kifungu cha Biblia?

**Wakaribishe na Mrejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila mtu kwa kufika kwenye kikundi.
- Anza kwa maombi, mepesi mafupi.
- Waulize wanakikundi kama wamefanya 'Kufanya wiki hii' na 'Kushuhudia' kazi toka toka wiki iliyopita.
- Wakaribishe washirikieshe chochote walichokijifunza ama kupata ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kujifunza namna ya kuomba siyo kujiombea wenyewe, lakini kwa jumuia zetu, hivyo mahitaji ya hao wanaotuzunguka yanapelekwa kwa Mungu na maisha yake mapya yanaweza kuja.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na marejeo ya Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Soma tena kwenye vifungu vidogo, ukiachia kikundi kurudia kila kifungu baada yako. Poleploe soma kwenye vifungu virefu kikundi kikirudia kila kipande mpaka kila mtu aweze kukariri kifungu chote. Watie baadhi ya watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

> *Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote.*
>
> *1 Timotheo 2:1*

**Hadithi**

Wasomee hadithi inayofuata kikundi:

Tokea Pete na familia yake walipohamia kwa majirani zao, amekuwa akiwakusanya watu pamoja kwa ajili ya kuomba kwa mahitaji ya marafiki na majirani. Wakati mwingine wanaombea mtu 1 au 2 au hali fulani wanayojua. Wakati mwingine wanaombea vitu tofauti, wakimwomba Mungu kuwafunulia vitu vingine ambavyo pengine wala wasingevielewa juu yake.

Jambo moja mara nyingi wanapenda kufanya ni kutembea kuzunguka jumuia huku wakiomba (hii inaitwa maombi ya kutembea). Wakati mwingine huomba kwa sauti, wakati mwingine polepole. Mara zote, wakati wakienda hukutana na watu ambao hawajawaona kwa muda au huona vitu ambavyo wasingevijua kabla na kuanza kuviombea.

Wiki chache zilizopita Pete na baadhi ya marafiki walitoka wakati wa joto la mchana. Waliwaona vijana wengi wakianza kukusanyika mahali, wengine juu ya pikipiki, wengine juu ya baiskeli, na wengi wao wakiwa wamebeba aina silaha. Imekuwa wazi kuwa kulikuwepo na vikundi 2 vikikusanyika na kuonekana kuwa walikuwa wanaenda kupigana.

Pete na marafiki zake wakaamua kuelekea kule ambako vijana wameanza kuksanyika. Walisimama na kuchukua muda kumwomba Mungu kuwatawanya watu na kuleta amani kwa majirani. Kwa haraka maombi yao yalijibiwa: mwonekano wa wengi pale ulianza kubadilika. Kwa kweli wale ambao hawakuondoka waliishia kuzungumza na Pete na marafiki zake juu ya imani yao ambayo imeumba nafasi ya kushuhudia habari ya maisha mapya ambayo wamekuwa na ujuzi nayo na Mungu aletaye amani siyo kwa maisha yetu tu ya binafsi, lakini kwa jumuia yetu yote.

**Kujifunza Biblia**

Soma 1 Timoteo 2:1-8 kwenye kikundi:

> *1Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na
> maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote;
> 2kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi
> maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na
> ustahivu. 3Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za Mungu
> Mwokozi wetu; 4ambaye hutaka watu wote waokolewe, na
> kupata kujua yaliyo kweli. 5Kwa sababu Mungu ni mmoja, na
> mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja,
> Mwanadamu Kristo Yesu; 6ambaye alijitoa mwenyewe kuwa
> ukombozi kwa ajili ya wote, utakaoshuhudiwa kwa majira
> yake. 7Nami kwa ajili ya huo niliwekwa niwe mhubiri na
> mtume, (nasema kweli, sisemi uongo), mwalimu wa Mataifa
> katika imani na kweli.*
>
> *8Basi, nataka wanaume waombe kila mahali, huku wakiinua
> mikono iliyotakata pasipo hasira wala majadiliano.*

Kwenye kifungu cha Biblia, mtume Paulo alimwandikia kiongozi kijana wa kanisa Timoteo kumwongoza na kumtia moyo kwenye huduma yake kwa kanisa lenye changamoto ya mazingira magumu. Anatumia neno 'wote', akitukumbusha sisi kuwa tumeitwa kwa ajili ya kuwaombea watu wote kwa sababu Mungu anawataka wote waokoke na kwamba Yesu alikufa msalabani ili haya yatokee. Wote ni kila moja: wa juu na wa chini; wenye elimu na wale hawajaenda shule; tajiri na maskini; wazuri na wabaya; mtesaji na anyeteswa. Kwa awaye yote haileti tofauti kwa Mungu maana anataka wote wapokee kile alichonacho kwa ajili yao. Anawapenda nasi tunapaswa kuwapenda pia. Ni nini kilicho na upendo zaidi ya kuja kwa Mungu kwa maombi na kuomba kwa niaba yao?

Pamoja na kuwaombea wale walioko kwenye jumuia, Paulo anatutia moyo kuwaombea viongozi na serikali iliyo juu yetu, hata

kama hatukubaliani nao au wako kinyume nasi. **Tukiomba kwa ajili ya amani na hekima kwa hao walioko madarakani, wafikie kumjua Mungu na kubadilishwa naye, ni kwa kiwango gani tutaweza kuona mabadiliko?** Siyo kwenye maisha yetu tu, au maisha ya wana jumuia wetu lakini kwenye taifa letu, mabara yetu, na dunia yote.

Yetu pia ametufundisha kuwaombea maadui zetu, kwa hao wanaotutesa. Hii ni ngumu kufanya ila tukumbuke udhamani wa ushauri wa Paulo wa kuwaombea watu 'wote'. Mungu atakusaidia kuwaombea hao unaona vigumu kuwaombea. Unaweza pia kutumia karama zako za kiroho kukusaidia kuomba, kwa mfano ukijua kuwa huna maneno sahihi unaweza ukaomba kwa lugha auunaweza kutoa unabii wa maandiko kwa watu na hali.

Ukitembea ukiomba ndani ya jumuia zetu pia inaweza kuwa ni ushuhuda wenye nguvu kwa hao wanaotuzunguka, na udhihirisho wa nguvu za Mungu kwenye eneo. Wiki iliyopita tulizungumzia juu ya vita vya kiroho na adui yetu shetani. Adui huyo anapenda kuwadanganya siyo tu watu binafsi lakini pia jumuiazao na majirani. Hata hivyo, tunataka Mungu awepo na kubariki maeneo yote ambayo tunakanyaga na miguu yetu (Yoshua 1:3, Kumbukumbu la Torati 11:24) pamoja na watu wote tunaokutana nao njiani.

**Shughuli**


15 Dakika

Tafuta kipande cha karatasi pana, au tumia vipande vya karatasi. Unaenda kuchora ramani rahisi juu ya karatasi hiyo.

Anza ukizungumza juu ya yale unayoyafahamu kwenye jumuia yako; anza na majumbani na maeneo yanayozunguka ambayo wanachama wa kikundi wanaishi na uchore juu ya karatasi unachoona kuwa ni muhimu na pia kile ambacho kinaonekana siyo muhimu!

Jenga ramani hiyo na usiogope ikionekana kuwa siyo nzuri kama inavyoonekana kwako kama kikundi kusaidia kuombea jumuia yako.

Huu ni mfano wa karatasi yako itakavyoonekana. Unapaswa kuwa msingi kwenye jumuia yako.




Kama unaweza kutunza ramani uliyochora pamoja unaweza kutumia kuomba kwa ajili ya jumuia yako wakati mwingine.

Kama ambavyo tayari tumekwisha kujifunza, kuna Mungu moja tu, na tunaweza kumwomba kupitia Mwana ye Yesu aliyeonyesha upendo wake kwa kufa kwa ajili yetu. Tumeunganishwa kama kaka na dada haijalishi tunatokea kwenye makanisa gani, hivyo sote tunaweza kwenda kwake kwa maombi. Maombi hayapaswi

kuwa ya kitu cha muundo fulani; ni juu ya kuja mbele za Mungu, kuongea naye na kusikiliza kwa kile anachosema.

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake namna ya kuomba na sehemu ya hiyo ni ‘ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, duniani kama ilivyo huko mbinguni’ (Matayo 5:10). Kuombea jumuia zetu na watu wanotengeneza hayo ni kumwomba Mungu kuleta mbingu karibu na dunia.

Wacha ufalme wake uje kwenye jumuia yako.

20 Dakika

**Shughuli**

Sasa ni wakati mzuri kufanya mazoezi ya maombi ya kutembea. Ingia kwenye kikundi cha watu 3 au 4.

Ombeni kwa pamoja kabla ya kuondoka, kumwomba Mungu kuonyesha hali yeyote au mtu ambaye angetaka kipekee umwombea na kuongea naye.

Halafu utoke na kufanya – hata hivyo unaweza kuomba jinsi unavyojisikia kuwa sawa, ndani ya kichwa chako au kwa sauti. Kumbuka kama unazungumza na mtu fulani kumuuliza kwanza kama wangependa uwaombee.

Njooni kwa pamoja tena baada ya dakika 15-20.

10 Dakika

**Maombi**

Ikiwa wote mmerudi pamoja waambie watu wawaeleze kikundi kilichobaki kile kilichotokea wakiwa kwenye maombi ya kutembea. Tumia ramani, na historia yako ya maombi ya kutembea, kukusaidia wewe kuomba kwa pamoja kwa watu tofauti, maeneo na vitu kwenye jumuia yako. Wakati ukiomba, ikiwa Mungu amemweka mtu yeyote, kitu chochote au sehemu yeyote kwenye moyo wako, unapaswa kuongeza kwenye ramani.

Inawezekana, watie watu moyo kuchukua picha ya ramani wakitumia simu zao ili waweze kutumia ramani kwa kazi ya nyumbani ya wiki hii.

**Kufanya wiki hii**

Wiki hii, kwenye kikundi cha watu 3 au 4, tufuta muda wa ziada kuzungukia hapo unapoishi na uwaombee watu na hali inayokuzunguka. Kama umeweza kupiga picha ya ramani unaweza kutumia hiyo kama ya kukukumbusha mambo ambayo mliyoombea kwa pamoja. Andika chini kile ambacho Mungu ameweka ndani ya moyo wako na uongeze kwenye ramani hadi mtakapokutana tena.

Ikiwa hujui cha kuombea kwa urahisi ombea watu baraka na maeneo.

Usiombee maeneo ukiwa mbali, tembelea uombee. Unaweza kumwona mtu au kitu kipya au Mungu anaweza kukupa picha, neno au kifungu cha Biblia.

Vitu vinapobadilika na maisha ya watu yameguswa na Mungu, weka alama kwenye ramani kama kutia moyo na kwa historia ya wakati ujao ya yale Mungu anayoyafanya kwenye jumuia yako.

**Shahidi**

Ukikutana na mtu na ukawa na nafasi, basi waambie kile unachokifanya na uwaulize kama wangependa uwaombee nini. Jitoe kuwaombea na uwe na maombi rahisi na kile walichotaka uwaombee. Na kama wanaonekana hawako tayari kuombewa, jitoe kuombea baraka rahisi.

Wakiuliza kujua zaidi na wakawa na maswali mengi unaweza kutoa ushauri wa kupanga muda wa kukutana pamoja kuwaeleza maisha aliyokupa Mungu wako kwa usahihi zaidi na namna hiyo ilivyokufanya kuwaombea wao na maeneo yao.

8

# Ushahidi – Kwa nini na Namna gani?



'Maana ufalme wa Mungu hauwi katika neno, bali katika nguvu.'
1 Wakorintho 4:20

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma Kifungu cha Biblia?

Unachohitaji:

- Viberiti au jagi la maji

**Wakaribishe na Mrejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila mtu kwa kufika kwenye kikundi.
- Anza kwa maombi, mepesi mafupi.
- Waulize wanakikundi kama wamefanya ‘Kufanya wiki hii’ na ‘Kushuhudia’ kazi toka toka wiki iliyopita.
- Wakaribishe washirikieshe chochote walichokijifunza ama kupata ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kuelewa kuwa kila moja wetu anayo historia ya pekee kueleza juu ya maisha yetu mapya ndani ya Yesu, na kazi yake kwenye jumuia. Sisi ni mashahidi wa kazi zake na kupitia kushuhudia historia zetu na ujuzi, tunapogundua maisha haya mapya, watu zaidi na zaidi watagundua maisha haya wenyewe pia.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na dondoo za Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Rudia tena kusoma na kuambia kikundi kurudia baada yako mpaka kila moja aweze kukariri kifungu chote. Watie moyo baadhi ya watu kujaribu na kurudia tena wenyewe.

> *Maana ufalme wa Mungu hauwi katika neno, bali katika nguvu.*
>
> *1 Wakorintho 4:20*

**Hadithi**

Wasomee hadithi inayofuata kikundi:

Mwezi wa kumi 2011 ulitokea ugonjwa mbaya kule Kambwali, Kaskazini mwa Zambia. Watoto walikuwa wakifariki mfululizo. 17 tayari wameshakufa. Hakuna mtu aliyejua chanzo cha ugonjwa huo. Ilionekana kama aina fulani ya ugonjwa ilyosababisha kuharisha na maumivu makali ya tumbo na ikawa kitu cha kutisha kwa kila aliyeteseka nayo.

Watu wengi kwenye eneo waliamini kuwa Chifu wa eneao alikuwa akitaka nguvu zaidi na aliwaloga watoto kuonyesha nguvu zake. Kikosi kiliinuka kinyume na Chifu na wakaenda eneo lake kumpiga.

Kikosi pia kikainuka kinyume na Kikundi cha Uzima cha Dignity kwenye eneo. Kikundi cha Uzima kilikuwa kikijifunza Biblia, wakiomba na kufanya kazi pamoja kwa faida ya jumuia kwa kujenga umoja na kuwajali wale wenye mahitaji. Kikundi cha Uzima kilipokuwa, watu wakaanza kukipinga wakidhani kikundi hicho kitakuwa na nguvu. Uvumi ukaenea kuwa kikundi kilikuwa cha Shetani na ghafla kikundi pia kikalaumiwa kwa kifo cha mfululizo cha watoto.

Kwa wakati huo, mwana kikundi cha Dignity alikitembelae Kikundi cha Uzima kukitia moyo. Alipokuwa hapo Kikundi cha Uzima kikakutanika kuomba kwa pamoja na kuwaalika idadi ya watu wengine toka kwenye jumuia. Walikutana kuomba asubuhi kwenye shule ya mahali.

Baada ya kuomba pamoja hakuna tena watoto waliofariki kwa ugonjwa huo!

Watu kwenye eneo walishangazwa zidi na zaidi walipoona maombi ya Kikundi cha Uzima yakijibiwa kwa siku zilizofuata. Kila

mtu alijua kuwa Wakristo waliomba pamoja na wakashuhudia kuwa ugonjwa ulizuiwa baada ya Wakristo kuomba.
Kikosi kichoinuka juu ya Chifu na Kikundi cha Uzima waliona kilichotokea na wakaacha matendo yao.

Chifu alipumua alipoona watoto hawafi tena na kuona watu wakirejeshwa kwenye jumuia. Alitoa agizo kwa viongozi wawkilishi kuzungumza na Kikundi cha Uzima kule Kambwali na kuanzisha vikundi kama hivyo kwenye maeneo mengi mengine ili watu waweze kujifunza juu ya Mungu mwenye nguvu walizoziona.

Mungu kwa nguvu zake aliwatetea watu wake na heshima yake na kusimamisha vifo visivyotakiwa vya watoto kwa ugonjwa usiokuwa na huruma. Matokeo ya Mungu kufanya kazi kwa sababu ya maombi ya watu wake jumuia, kikosi na Chifu walishuhudia nguvu za Mungu. Wakawaambia watu wengi zaidi, na jumuia zingine nyingi zilizowazunguka zilifunguka kwa habari njema za Yesu.

**Kujifunza Biblia**

Soma Matendo 1:8 kwenye kikundi:

> *Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na kote katika Yudea, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.*

**Kushuhudia ni nini?**

Kuwa shahidi maana yake ni kuwa umeona au umepata ujuzi wa kitu kinachotokea ambacho unaambiwa kuzungumzia juu yake. Mara nyingi tunazungumzia mashahidi wanaohusiana na kosa lililotendwa; hao walioona tukio wanaitwa mahakamani kuelezea kile walichokiona. Kila shahidi anao mtazamo wake wa kipekee wa kile kilichotokea, kama jinsi ilivyo kwetu kila moja anayo historia ya pekee wa namna Mungu anavyofanya kazi ndani ya

maisha yetu. Sisi sote tunalo la kusema kuhusu maisha mapya tunayo pata ujuzi kupitia Mungu na tunaposhuhudia kile tunachokijua, Mungu atatengeneza nafasi kwa wengine kuja na kulijua pia.

Yesu alisema,

> *'14 Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji ukiwa juu ya mlima hauwezi kusitirika. 15 Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani. 16 Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.'*
>
> *Matayo 5:14-16*

Wote tunayo nuru ndani yetu, hata hivyo wakati mwingine tunaona aibu, kusumbuliwa au hofu kueleza kile alichotufanyia. Bado tunakumbushwa kuwa tunapaswa kuwa tayari na kujiandaa kutoa jibu kwa hao wanaotuuliza juu ya tumaini tulilonalo (1 Petro 3:15). Kenye kipindi hiki tutaenda kutazama baadhi ya njia zingine ambazo tutakuwa tayari kushuhudia yale ambayo Mungu amefanya. Hii inahusisha maneno yetu na metendo yetuna kifungu chetu cha kukumbuka kinatuonyesha sisi – siyo tu maneno (ingawa maneno yetu ni ya muhimu), inahusu pia juu ya nguvu, inayodhihirishwa kwenye Ufalme wa Mungu ujao.

Kusudi la maisha yetu ni kumfanana Kristo, ili tuweze kuona namna Yesu alivyoshuhudia watu kama mfano. Yesu alikuja kutafuta na kuokoa hao waliopotea. Aliwafikia kwa njia tofauti kwa nyakati tofauti.

Ushahidi huhusisha matendo na maneno. Yesu alionyesha hili. Kwenye mwanzo wa kitabu cha Matendo, mwandishi Luka alitaja kuwa kwenye kitabu chake cha kwanza aliandika juu ya yale 'yote aliyoanaz Yesu kufanya na kufundisha' (Matendo 1:1). Tunafahamu toka kwenye kitabu cha Yakobo kuwa imani pasipo matendoimekufa (Yakobo 2:17).

Kitabu cha Ufunuo pia kinafundisha kuwa Wakristo wanao ushindi dhidi ya shetani kupitia ‘damu ya mwana kondoo na kwa ushuhuda’ (Ufunuo 12:11). Hii ina maana kuwa ushuhuda wetu, historia yetu, nguvu yake ya kubadilisha maisha. Wakristo wengi wanakadiria pungufu ya nguvu ya historia yao wenyewe.

**Kwa nini tunshuhudia?**
Mungu anatutuma nje kuwafikia watu wote ili tuwe mashahidi wake. Hatufanyi kwa sababu kwa sababu maisha yetu mbinguni inategemea hiyo; badala yake, tumepewa kazi ya kushuhudia maisha ya Yesu na Ufalme wake kwa kila mtu. Mungu ni muumbaji na siku zote hutafuta nafasi kuumba maisha mapya ndani ya watu na jumuia, na huwa naushirika nasi kufanya haya yatokee.

**Unashuhudiaje?**
Kila wiki kama sehemu ya ***Misingi*** tunayo sehemu ya kushuhudia. Siku zote hili ni wazo la kufanyia kazi juu ya namna ya kushuhudia kupitia maneno yako au matendo kitu cha maisha mapya uliyopokea kwa Mungu. Kupitia kipindi kilichopita tulipendekeza njia nyingi za kushuhudia kwa imani yako mpya.

Kitu kimoja cha kipekee kinachofaa kufanyika ni kufanyia mazoezi ushuhuda wako ili iwe rahisi, na haraka, kuwaambia watu wanaouliza kuwa imani yako ni juu ya nini.

Ushuhuda wako kwa urahisi ni historia ya namna ulivyokutana na Yesu na ni nini amefanya kwenye maisha yako tokea hapo.

**Shughuli**

15
Dakika

Wiki hii tunaenda kufanya mazoezi ya kutoa kwa kifupi mtazamo wa ushuhuda wetu. Mara nyingi watu hawapendi kusikiliza historia ndefu, kwa ajili hiyo tutaenda kutazama pointi za maana juu ya historia yetu ili kuweza kupata taarifa zilizo za muhimu ndani yake.

Fikiri juu ya namana utakavyojibu maswa matatu yafuatayo:

- Maisha yako yalikuwaje kabla hujakutana na Yesu?
- Ulikutanaje naye?
- Nini kilichobadilika kama matokeoya maisha mapya aliyokupa Yesu?

Kwenye kikundi cha watu 3 au 4, kila moja afanye mazoezi ya kujibu maswali haya 3 kwenye nafasi ya muda itakayochukua pengine kuungua kwa kiberiti au jagi la maji kumiminwa taratibu. Kama huna kiberiti au jagi la maji, unaweza kutumia saa ya muda kwenye simu ambayo itasetiwa kwa dakika 2 au pungufu.

Njia nyingine za kushuhudia ni kupitia vipawa vyetu vyetu vya kiroho, kupitia kudhihirisha nguvu za Mungu na kuendelea kuishi tofauti na wale walioko duniani. Maisha yetu kama maneno yetu yanazungumza kwa sauti kuhusu kazi za Yesu ndani yetu.

Wakati Yesu anaishi ndani yetu kwa Roho wake Mtakatifu, anaweza kutusaidia na kutuongoza kwa sauti yake. Tunaweza kusikiliza sauti yake kwa makini na kuwa na uhakika kuwa atatoa nguvu inayohitajika kudhihirisha uhalisi wa maneno yetu.

**Maswali**

Kwenye kikundi cha 3 au 4 jadilini maswali yafuatayo:

10 Dakika

- Kwa nini unakuta kuwa ni vigumu kushuhudia imani yako?
- Utawezaje kushinda baadhi ya sababu hizi?
- Mungu amebadilisha maisha yako tokea umpe maisha yako?
- Ni maeneo gani kwenye maisha yako unafikiri kuwa bado unahitaji kumwomba Mungu kubadilisha?

**Maombi**

Waambie kikundi kusimama na kuunda mduara na kushikana mikono. Wakati wamesimama pamoja, waambie warudie maombi haya mepesi baada yako.

5 Dakika


Mungu ndani yangu,
nisaidie niwe shahidi wako;
badilisha maisha yangu, maneno yangu na matendo yangu
ili kwamba watu wakiniangalia mimi, wanaweza kukuona wewe.
Amen.

**Kufanya wiki hii**

Wiki hii endelea kufanya mazoezi kushuhudia ushuhuda wako na wanachama wengine wachache wa kikundi. Endelea kujaribu mpaka uweze kukumbuka bila kutazama na unaweza kuielezea haraka.

**Shahidi**

Shughuli zote za tofauti tulizozifanya ni namna ya ushuhuda! Wiki iliyopita tulikuwa waombaji wa kutembea na kuzungumza na watu kila tulikoenda. Tembea ukiomba tena. Mwombe Mungu akupe nafasi ya kumweleza mtu mwingine ushuhuda wako mtu anayependa kusikiliza namna Mungu alivyo mzuri na kupenda maisha yetu. Kumbuka kuwa hauko peke yako – Roho wa Mungu mwenye nguvunyuko ndani yako ya kuwashuhudia watu, waulize kama kuna wangehitaji Mungu awatendee na uombe hilo litokee.



9

# Nenda Uwaambie Wengine

'Akawaambia, Mavuno ni mengi, lakini wafanya kazi ni wachache; basi mwombeni Bwana wa mavuno apeleke wafanya kazi katika mavuno yake.'

Luka 10:2

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma Kifungu cha Biblia?

**Wakaribishe na Mrejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila mtu kwa kufika kwenye kikundi.
- Anza kwa maombi, mepesi mafupi.
- Waulize wanakikundi kama wamefanya ‘Kufanya wiki hii’ na ‘Kushuhudia’ kazi toka toka wiki iliyopita.
- Wakaribishe washirikieshe chochote walichokijifunza ama kupata ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi hiki ni kuchunguza utaenda kwa nani kumweleza juu ya maisha haya mapya kuwa Yesu anakuwa ndani yako. Iwapo hapo ni mbali au karibu kwa kila siku au njia zingine za ziada, sisi sote tumeitwa kuwaambia watu wengine juu ya imani tuliyonayo.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na marejeo ya Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Soma tena kwenye vifungu vidogo, ukiachia kikundi kurudia kila kifungu baada yako. Poleploe soma kwenye vifungu virefu kikundi kikirudia kila kipande mpaka kila mtu aweze kukariri kifungu chote. Watie baadhi ya watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

> *Akawaambia, Mavuno ni mengi, lakini wafanya kazi ni wachache; basi mwombeni Bwana wa mavuno apeleke wafanya kazi katika mavuno yake.*
>
> *Luka 10:2*

**Hadithi**

Wasomee hadithi inayofuata kikundi:

Kulikuwa na mtu anayeitwa Mr Nat ambaye, kwa huzuni, alitengana na mke wake kwa miaka mingi alipoanza kupata dalili za ugonjwa wa Parkinson. Aliacha pia kazi yake kama wakili na kuwa monk kiongozi wa dini ya Kibudha, akisafiri maeneo mengi mbali na nyumbani.

Kwa miaka mingi, Nat hakuona mafanikio yeyote kwenye mazoezi makali ya hekalu la Kibudha. Baadaye aliamua kufuata Ukristo badala ya Ubudha. Mapema akaanza kupata ujuzi wa maisha mapya katika Mungu katika moyo wake, huruma ikakua ndani yake kwa mke wake walioachana, Mrs Sonjay. Aliamua kuzungumza na mchungaji wa kanisa lake, Mchungaji Pitak, na akamwomba mchungaji amtembelee na kumwombea.

Mchungaji Pitak akaenda na Nat nyumbani kwao na Sonjay kwenye ukingo wa kisiwa kizuri cha bahari. Sonjay sasa amekuwa maskini kabisa kwa sababu ugonjwa wa Parkinson ulizidi kuwa mbaya kwa nyakati. Nat alimtambulisha mchungaji na wakaongea kwa kifupi pamoja. Wakati mchungaji alipomwambia Sonjay kuwa amekuja kumwombea, aliweka macho yake wazi na akaanza kutazama kwa shauku. Nat na mchungaji waliimba wimbo juu ya nguvu za Yesu na Nat akamwambia Sonjay juu ya imani yake mpya ndani ya Yesu. Mchungaji Pitak akamwambia historia rahisi ya kuzaliwa kwa Yesu, kifo chake na kufufuka. Alimwambia ainue mkono wake kama ameelewa na pia kama anataka kumfungulia Mungu moyo wake. Aliinua mkono wake mara mbili na Pitak akamwongoza sala ya toba na kuweka agano na Yesu.

Sonjay akainuka kwenye kiti chake na kutembea kwa shida kwenye varanda akiwaonyesha sehemu nzuri ya kutazama bahari. Aliwaonyesha ukaribu mkubwa. Mchungaji Pitak sasa anajua kuwa atarudi kumtembelea tena na kumsaidia kuelewa zaidi juu ya imani katika Yesu. Ukaribisho wake mzuri ulimfungulia mlango wa Mungu kutembea ndani yake.

**Kujifunza Biblia**

Soma Luka 10:1-20 kwenye kikundi:

*1Basi, baada ya hayo Bwana aliweka na wengine, sabini,*
*akawatuma wawili wawili wamtangulie kwenda katika kila*
*mji na kila mahali alipokusudia kwenda mwenyewe.*
*2Akawaambia, Mavuno ni mengi, lakini wafanya kazi ni*
*wachache; basi mwombeni Bwana wa mavuno apeleke*
*wafanya kazi katika mavuno yake. 3Nendeni, angalieni,*
*nawatuma kama wana-kondoo kati ya mbwamwitu.*
*4Msichukue mfuko, wala mkoba, wala viatu; wala*
*msimwamkie mtu njiani.*

*5Na nyumba yoyote mtakayoingia, semeni kwanza, Amani*
*iwemo nyumbani humu; 6na akiwamo mwana wa amani,*
*amani yenu itamkalia; lakini kama hamna, amani yenu*
*itarudi kwenu. 7Basi, kaeni katika nyumba iyo hiyo, mkila na*
*kunywa vya kwao; maana, mfanya kazi amestahili kupewa*
*ujira wake. Msihamahame kutoka nyumba hii kwenda*
*nyumba hii.*

*8Na mji wowote mtakaouingia, wakiwakaribisha, vileni*
*vyakula viwekwavyo mbele yenu; 9waponyeni wagonjwa*
*waliomo, waambieni, Ufalme wa Mungu umewakaribia.*
*10Na mji wowote mtakaouingia, nao hawawakaribishi,*
*tokeni humo, nanyi mkipita katika njia zake semeni, 11hata*
*mavumbi ya mji wenu yaliyogandamana na miguu yetu*
*tunayakung'uta juu yenu. Lakini jueni hili, ya kuwa Ufalme*
*wa Mungu umekaribia. 12Nawaambia ya kwamba siku ile*
*itakuwa rahisi zaidi Sodoma kuistahimili adhabu yake kuliko*
*mji huo.*

*13Ole wako Korazini! Ole wako, Bethsaida! Kwa kuwa kama*
*miujiza hiyo iliyofanyika kwenu ingalifanyika katika Tiro na*
*Sidoni, wangalitubu tangu hapo, huku wakikaa katika nguo*
*za magunia na majivu. 14Lakini, siku ya hukumu itakuwa*

*rahisi Tiro na Sidoni kustahimili adhabu zake kuliko ninyi.*
*[15]Nawe Kapernaumu, je! Utakuzwa hata mbinguni?*
*Utashushwa hata kuzimu.*

*[16]Awasikilizaye ninyi anisikiliza mimi, naye awakataaye ninyi anikataa mimi; naye anikataaye mimi amkataa yeye aliyenituma.*

*[17]Ndipo wale sabini waliporudi kwa furaha, wakisema, Bwana, hata pepo wanatutii kwa jina lako.*

*[18]Akawaambia, Nilimwona Shetani, akianguka kutoka*
*mbinguni kama umeme. [19]Tazama, nimewapa amri ya*
*kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala*
*hakuna kitu kitakachowadhuru. [20]Lakini, msifurahi kwa vile*
*pepo wanavyowatii; bali furahini kwa sababu majina yenu*
*yameandikwa mbinguni.*

Wakati Yesu akiishi duniani alichukua muda akitembelea miji na vijiji vingi. Alikuwa na maono makubwa na mipango rahisi. Maono yake ni juu ya mashamba yaliyo iva, yaliyo tayari kwa mavuno. Mpango wake ilikuwa kuwatuma wafuasi wake kukutana na watu na kuwaambia juu yake. Hawakutakiwa kuwa na wasiwasi au kujiamini wao wenyewe hivyo aliwaambia wasibebe kitu chochote pamoja nao. Walitakiwa kumtafuta mtu ambaye angewakaribisha wao. Kama wangekutana na upinzani mwingi wangehamia mji mwingine.

Kama wafuasi katika Yesu tunayo nafasi na wajibu ya kuwa mashahidi wa Yesu kwenye maisha yetu ya siku kwa siku. Sisi sote tunao marafiki, majirani na familia na wote wanataka kumwona Yesu kazini ndani ya maisha yetu.

Kuna pia nyakati ambazo Yesu anatuita kwenda zaidi ya hayo na kufikia maeneo fulani ambazo yeye mwenyewe anataka kwenda. Hatuwezi kufanya hayo wenyewe. Pengine Mungu anaongoza kanisa lako, kikundi cha kujifunza Biblia au Kikundi cha Uzima

kutembelea majirani au kikundi cha vijiji. Kama kuna makubaliano ndani yako kuwa Mungu anakuongoza, sasa utafanyaje hayo?

Kitu cha kwanza unapaswa kutazama nje na Yesu na kuona kuwa kuna 'mavuno'. Inaweza kuonekana kuwa hakuna mtu yuko tayari au hafurahii ujumbe wako wa matumaini lakini kuna watu ambao wako tayari na hutayajua hayo mpaka utoke nje na kuwatafuta. Hiyo ndiyo maana 'Nenda!' (kifungu 3). Ina maana ya nenda nje na kuunganika na waamini wengine watakaoenda na wewe. Usivunjike moyo au kukata tama kama waumini wengine hawataki kuungana na wewe moja kwa moja. Unahitaji tu timu ndogo na Yesu mwenyewe alisema kuwapata watenda kazi wa aina hiyo (wafanyakazi) itakuwa ni vigumu. Pia, usiogope: Yesu alisema atakuwa pamoja nasi katika mambo yote.

Usiwe na wasiwasi. Panga muda wa kwenda na usiruhusu matukio ya dunia yakugeuze. Usibebe vitabu vingi au vitu pamoja nawe. Weka mtazamo wako mahali Mungu amekuonyesha kutembelea. Kumbuka kuweka imani yako kwa Mungu; atafanya njia kwako.

Uwe na mpango rahisi. Huchukui mwaliko kwenye mkutano lakini unaenda kuingia kwenye majadiliano yatakayokuongoza kushuhudia historia yako ya maisha ya Yesu mapya na mtu kwenye eneo hilo. Kwenye kifungu inazungumzia juu ya kumtafuta mtu wa amani, mtu ambaye atakukaribisha na ujumbe wako na hata kutengeneza nafasi yaw ewe kushuhudia ujumbe wako kwa upana zaidi kwenye familia au jumuia. Hakikisha unaomba na kumwomba Mungu kukuonyesha hawa ni watu gani.

Tumia mwelekeo mzuri wa kumfikia. Unaweza kuanza kwa kuwauliza watu uliokutana nao kama wana jambo lolote wanalotaka uwaombee. Ama mahali ambapo Wakristo hawajawahi kufika unaweza kuwauliza kwa urahisi kama waliwahi kusikia habari za Yesu.

Unaweza kuadhirika kwa pointi hiyo. Yesu alisema unaweza kujisikia kama kondoo ndani ya mbwa mwitu hivyo usishangae

unapokuwa na hali kama hiyo! Hata hivyo, Mungu anazo njia za kufungua milango na ikiwa utakutana na mtu ambaye anao mwitikio mizuri basi utakuwa umekutana na mtu wa amani ambaye Mungu amekuongoza kwake. Mwitikio wao utakuwa wa amani na utakuwa na uhuru wa kuendelea kuwashuhudia. Kumbuka kanuni ya miduara 3 ya kushirikisha tuliyoangalia kwenye kipindi cha kwanza cha ***Misingi 1: Maisha Huanza***? Unaweza kutumia hiyo kusaidia kuwasilisha ujumbe wako (tutarudia hili baadaye kwenye kipindi). Au unaweza kutumia kanuni tuliyofanyia mazoezi wiki iliyopita.

Usiondoke tu bila kufikiri namna Mungu anavyotaka uondoke. Kama wakikukaribisha kwa sababu ya ukarimu basi kubali tu bila kusita. Mungu anafungua mioyo yao. Uchowashuhudia ni cha muhimu sana na utarajie mwitikio. Hii inaweza kuwa kuwakusanya watu wengine kwenye vikundi vyao vya familia au marafiki kusoma moja ya mifano ya Yesu na ufikiri juu ya itakavyogusa maisha yao na watakavyo shuhudia hilo kwa wengine. Pia uwe radhi kuwaombea na kuleta uponyaji wa Mungu kwenye maisha yao. Kuwa tayari kwa jambo lolote na usiweke na kiwango kwa yale ambayo Mungu atafanya.

Utakuwa umefungua kijiji au kikundi cha majirani; hivi ndivyo Yesu alivyoona alipowatuma wale 72. Na walirudi huku wameshangaa na kuwa na furaha kuwa Mungu amefungua milango. Utaanza kuona hayo mpango huu wa kazi. Kwa nini isiwe hivyo? Ilikuwa ni mpango rahisi aliyotumia Yesu. Wanaoweka kiwango ni sisi wenyewe, ikiwa hatuamini kuwa itafanya kazi au tunajitoa wenyewe bila kujaribu. Hivyo, uwe jasiri na utiwe moyo – Yesu amekuambia uende, ataenda pamoja na wewe, na anayo mavuno yanayokusubiri!

**Maswali**

15 Dakika

Waambie watu wajadili maswali haya kwenye kikundi cha watu 3 au 4. Soma swali 1, ruhusu dakika chache ya majadiliano halafu waambie watu kushuhudia majibu yao. Baadhi ya majibu yanayofanana yametolewa baada ya kila swali. Mnaweza kuweka

pamoja maswali hayo na majibu haya kabla ya kwenda kwenye swali linalofuata.

- Mungu anaweza kukuambia uende wapi?

  Jibu linalofanana: Inaonekana kuwa Mungu anaweza kukuambia uende sehemu au kwenye kikundi cha watu mahali watu hawamjui yeye.

- Unafikirije kuwa utamtambua mtu wa amani?

  Jibu linalofanana: Mtu wa amani ni mtu ambaye hakupingi au ni mtu ambaye hataki mabishano ya muda mrefu yanayo husiana na imani. Inawezekana wakafurahia unaposhuhudia historia ya maisha mapya ndani ya Yesu. Inawezekana wasiwe tayari haraka unapokuwa nao kwa mara ya kwanza.

- Utashuhudiaje habari njema juu ya Yesu? Unajua namna ya kushuhudia kifupi kwa namna ambayo inaweka wazi uamuzi wa kumpokea Yesu?

  Jibu linayofanana: Itasaidia sana kushuhudia habari njema wazi kwa dakika 5 (au pungufu) kwa sababu watu wanaweza kukereka au kupoteza kile unachokisema. Jambo la muhimu kwa pointi ya ujumbe ni: tumetenganishwa na Mungu kwa kugeuka na kumwacha sisi wenyewe (dhambi); majaribio yetu ya kupona kuvunjika kwetu haifanyi kazi (toa mifano mifupi); Mungu alimtuma Yesu kuchukua adhabu yetu kwa makosa yetu na kufungua njia; ili tugeuke na kupokea hili ikiwa tunataka kurejeshwa na Mungu.

- Utawaambia nini watu waliosema walikuwa tayari kumpokea Kristo?


  Jibu linalofanana: Unapaswa kuomba pamoja nao na kuwaongoza wao kujua msamaha kamili wa Mungu.

Unapaswa kuwasaidia kuelewa kuwa wao ni viumbe vipya ndani ya Kristo (2 Wakorintho 5:17). Unapaswa kubaki nao na kufurahia ukaribisho wao kwa muda mrefu au ufanye mpango wa kurudi mapema na ikiwezekana isizidi muda wa siku 1.

15
Dakika

**Shughuli**

Unakumbuka mchoro tuliochora wa miduara 3[3] kwenye kipindi cha kwanza ya ***Misingi 1: Maisha Huumba***? Tunaenda kutumia tena.




[3] Miduara 3 inatokana na Kanisa la Familia kule Palm Beach ya Mangaribi, Florida. Inafungua chanzo cha vifaa inayoweza kutengenezwa bila gharama yeyote.

Kwa kutumia mchoro huu, onyesha jinsi utakavyoweza kushuhudia injili kwa dakika 5.

Jaribu kuanza na mduara ukionyesha Usanifu wa Mungu. Halafu jaribu kuanza na mduara kuonyesha kuvunjika kwetu. Ni njia ipi ndiyo bora?

10 Dakika

**Maombi**

Soma maombi yafuatayo kwenye kikundi. Soma kwa vifungu vifupi na kumuuliza kila mtu kurudia kila sehemu baada yako ikiwa watataka kuitikia kwenye kipindi cha leo kwa kumwomba Yesu kuwatuma watoke.

> Bwana Yesu,
> Aksante kunikumbusha mimi kuwa mavuno yako tayari.
> Nisaidie nione wakati naenda.
> Tuma watenda kazi waende na mimi, wanisaidie na kunitia moyo,
> na utusaidie sisi kwenda kwa ujasiri na mtazamo.
> Tuonyeshe pa kwenda na utufungulie sisi milango.
> Tusaidie tuendelee kwenda tunapotafuta kumweleza kila mtu kuwa tunamjali.
> Amen.

**Kufanya wiki hii**

Wiki hii weka alam kwenye simu yako au saa ya ukutani saa 10:02 kila asubuhi. Wakati ikizima, omba kupitia kifungu chako cha kukumbuka, Luka 10:2. (Kama huna simu au saa ya alam waza juu ya kitu cha kufanya kila siku halafu ukifanya kila siku wiki hii, acha na omba maombi haya.)

- Omba juu ya kuhusika mwenyewe kama mtenda kazi kwenye mavuno Yesu aliyozungumzia.
- Fanya mazoezi kwa ile michoro ya miduara 3 tena.
- Mwombe Mungu akuonyeshe anataka kukutuma wapi, na kukuunganisha na watu utakaoenda nao.

**Shahidi**

Tayari tumekuwa tukizungumza na watu ndani ya jumuia zetu. Leo tumeona kuwa Yesu anatutuma mbele zaidi. Nenda kwenye jumia ya jirani na ushuhudie yale unayoyafanya. Kama unamfahamu mtu hapo, panga kukutana nao na uwaeleze juu ya Kikundi cha Uzima chako. Unaweza kuwasaidia kuanzisha moja kwenye jumuia yao. Kama humjui mtu yeyote, kwa urahisi nenda ufanye maombi ya kutembea kwenye jumuia. Wakati unaomba mwombe Mungu akulete kwa watu aliyowaweka kwenye jumuia hiyo watakaosaidia wengine kumjua Yesu.

# Kumbukumbu

10

# Haki



'Lakini hukumu na iteremke kama maji, na haki kama maji makuu.'

Amosi 5:24

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma Kifungu cha Biblia?

**Wakaribishe na Mrejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila mtu kwa kufika kwenye kikundi.
- Anza kwa maombi, mepesi mafupi.
- Waulize wanakikundi kama wamefanya ‘Kufanya wiki hii’ na ‘Kushuhudia’ kazi toka toka wiki iliyopita.
- Wakaribishe washirikieshe chochote walichokijifunza ama kupata ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kuelewa maswali, ‘Haki ni nini?’ Jinsi tunavyofahamu kuwa Mungu ni pendo, Biblia inatuambia kuwa Mungu ni mwenye haki, na anatafuta kuleta haki duniani.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na marejeo ya Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Soma tena kwenye vifungu vidogo, ukiachia kikundi kurudia kila kifungu baada yako. Poleploe soma kwenye vifungu virefu kikundi kikirudia kila kipande mpaka kila mtu aweze kukariri kifungu chote. Watie baadhi ya watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

> *Lakini hukumu na iteremke kama maji, na haki kama maji makuu.*
>
> *Amosi 5:24*

**Hadithi**

Soma historia inayofuata iliyochukuliwa toka *Gazeti la Zambia* kwenye kikundi. Eleza kuwa ni historia ya binti mdogo, mtoto wa

pekee, aliyetumwa Lusaka, mji mkuu wa Zambia. Kabla ya kwenda Lusaka hakuwai kuwa mbali nje na kijiji chao.

> Wakati Tomaida Tembo alipopokea habari ya safari yake ya kwenda Lusaka, alikuwa umbali wa km 500 kule Katete kijiji cha Kathumba kule kweny Mkoa wa Mashariki wa Zambia. Binti wa miaka 11 hakujua namna ya kufurahia.
>
> Lusaka kwake imekuwa sehemu ya visasili na kulingana na hao ambao tayari wameshakuwa mjini, ilikuwa ni sehemu ya 'agebenga' (majambazi) na 'akapenta' (makahaba) waliofanya doria na kudhalilisha mitaa ya mji wa 'mwanga'.
>
> Kilichokuwa mahali pa visasili kwa Tomaida karibu itakuwa kitu cha halisi.
>
> Kufanya safari yake kuwa rahisi, binamu wake wa mbali alikuwa ametuma fedha za kutosha kugharamia safari yake na zaidi kumsaidia mama yake kutulia baada ya kuondoka. Imekuwa miaka mitano ilyopita tokea Tomaida aacha makazi ya mama yake kwenye safari iliyobadilisha maisha yake daima.
>
> Akishangaa mitaa ya baridi za Lusaka, Tomaida anasubiri mteja wake mwingine kwenye barabara ya Addis Ababa.[4]

Ikielezwa kuwa Tomaida alitumwa Lusaka na familia yake, akauzwa kwenye maisha ya kutengeneza pesa kwa familia yake kwa kufanya kazi na binamu wake huko Lusaka. Hata hivyo, baada ya kufika Lusaka, binamu wake alimlazimisha kwenye maisha ya utumwa wa ngono na ukahaba. Tomaida huwahi kujua kama kitu chochote kingeweza kubadilika na kuwa tofauti; aliwekwa utumwani, akiuzwa na familia yake mwenyewe.

---

[4] (2003) 'Historia ya Tomaida Tembo' Gazeti la Zambia, July 11th

Historia hii ingekuwa inatisha kama ingekuwa ya uongo. Hata inatisha zaidi kwa sababu ni ya kweli. Tomaida ni mtu halisi nah ii ni historia yake ya kweli: utoto wake na maisha yake ya baadaye ilichukuliwa toka kwake kwa kuuzwa akiwa na umri wa miaka 11 tu. Kwenye taarifa iliyotolewa na Serikali ya Marekani, hali – ambayo ni ya kipekee Zambia – iliachwa uchi:

> Zambia ni chanzo, kivuko, na nchi ya kufikia kwa wanawake na watoto kwa biashara kwa kusudi la kulazimishwa kazi na unyonyaji wa kingono. Kafara ya wototo, biashara ya kwanza ndani ya nchi kwa kazi na unyonyaji wa kingono, inaonekana kuwa ya kike, umri mchanga, na yatima. Kwa kubadilishana na fedha au zawadi, ndugu na jamaa huondoka hata kurahisisha biashara ya mtoto kwenye kituo cha mji kwa ajili ya ukahaba. Watoto wakati mwingine hufanyiwa biashara kama matokeo ya kupokea msaada toka kwa wageni kama madereva wa malori. Wafanyakazi watoto wengi wa Zambia, hasa hao walioko kwenye ukulima, huduma za ufugaji na secta ya uvuvi ni waadhirika pia wa biashara ya kibinaadamu. Wafanya biashara wengi hufanya kazi kwa kunasa, mawasiliano mepesi ya ndugu na jamii, madereva wa malori, watu wa biashara, wafanyabiashara wa mipakani, na viongozi wa kidini.[5]

**Kujifunza Biblia**

Soma <u>Isaya 42:1-9</u> kwenye kikundi:

> *1 Tazama mtumishi wangu nimtegemezaye; mteule wangu,*
> *ambaye nafsi yangu imependezwa naye; nimetia roho yangu*
> *juu yake; naye atawatolea mataifa hukumu. 2 Hatalia, wala*
> *hatapaza sauti yake, wala kuifanya isikiwe katika njia kuu.*
> *3 Mwanzi uliopondeka hatauvunja, wala utambi utokao*
> *moshi hatauzima; atatoa hukumu kwa uaminifu. 4 Hatazimia,*

---

[5] Idara ya Kimarekani (2009). *Taarifa ya biashara ya binadamu 2009, Simulizi ya Nchi – Nchi Q hadi Z* [Mtandaoni] Iko: https//www.state.gov/j/tip/ris/tiprpt/2009/123139.htm [Iliangaliwa 19 July 2018.

*wala hatakata tamaa, hata atakapoweka hukumu duniani;*
*na visiwa vitaingojea sheria yake.* 5 *Mungu BWANA anena,*
*yeye aliyeziumba mbingu, na kuzitanda; yeye aliyeitandaza*
*nchi na mazao yake; yeye awapaye pumzi watu walio juu*
*yake; yeye awapaye roho wao waendao ndani yake.* 6 *Mimi,*
*BWANA, nimekuita katika haki, nami nitakushika mkono, na*
*kukulinda, na kukutoa uwe agano la watu, na nuru ya*
*mataifa;* 7 *kuyafunua macho ya vipofu, kuwatoa gerezani*
*waliofungwa, kuwatoa wale walioketi gizani katika nyumba*
*ya kufungwa.* 8 *Mimi ni BWANA; ndilo jina langu; na utukufu*
*wangu sitampa mwingine, wala sitawapa sanamu sifa*
*zangu. =Tazama, mambo ya kwanza yamekuwa, nami*
*nayahubiri mambo mapya; kabla hayajatokea nawapasheni*
*habari zake.*

Uliwahi kuwa kwenye hali ya kujisikia umetosheka na kila kitu kiko sawa kwenye maisha yako? Kila kitu ilikuwa ni amani wala hukuogopa jambo lolote? Hiyo hali uliyokuwa nayo, kuna neno la Kiebrania inayo itwa ‘Shalom’. Shalom siyo kitu kiurahisi tu tunayosema kwa kiingereza ‘amani’. Ni ile hali ya kujisikia kuwa kila kitu kiko sawa kwa kila mtu duniani. Kwa hiyo, hali hiyo uliokuwa nayo wakati kila kitu kilikuwa kwenye amani ni Shalom.

Shida ni kuwa hatuishi kwenye dunia iliyojaa ‘Shalom’. Watu wanakutana na shida mateso na kutotendewa haki. Shida, biashara ya binadamu na kupigana imeenea kila mahali. Hakuna siku hata moja kwenye dunia yetu ambayo kila kitu kiko kwenye amani au shalom. Mtu sehemu fulani anaweza kuwa mkali au mhanga.

Kuna neno lingine la Kiebrania linaloelezea kitu ambacho dunia hii inahitaji. Neno ni, ‘tsedeqah’. Mamlaka ya ‘kisheria’ au ‘haki’. Kwenye Biblia, mahali popote unapoona neno haki au mamlaka ya kisheria kwa kawaida hili wazo la Kiebrania linalenga hayo. Mungu anataka shalom kwa dunia yetu: amani, furaha, upendo na mamlaka ya kisheria. Hii ina maana kuwa haki ya Mungu na mamlaka ya kisheria ni lazima yatokee katika kila hali.

Kwa hiyo hii inatuhusu nini sisi?

Kama watu wanaotaka kumfuata Yesu, tumeitwa kuwa watu wa mamlaka ya kisheria na haki na kushikilia mawazo hayo kwenye maisha yetu, kwenye biashara na kwa kila hali tunayokutana nayo. Haitoshi tu kusema tunamfuata Kristo na bado kudharau vitu ambavyo siyo sawa kwenye dunia yetu. Hivyo viwili haviwezi kwenda kwa pamoja.

**Yesu huleta mamlaka ya kisheria**

Kifungu chetu cha Biblia wiki hii imechukuliwa toka kwenye kitabu cha Isaya: alikuwa ni nabii aliyeishi miaka 700 kabla ya Kristo. Hata hivyo, kwenye kifungu hiki anazungumzia juu ya Yesu, akitabiri kuwa Yesu ni nani. Anatuambia kuwa Yesu ni moja aliyechaguliwa na Mungu, atakayeleta 'mamlaka ya kisheria kwa mataifa'. Mungu anataka kila mtu kupata ujuzi wake wa mamlaka ya kisheria na haki ambayo ndiyo moja ya sababu aliweka Roho wake pamoja na Yesu na kuwatuma kwetu. Leo mamlaka ya kisheria inaletwa na Roho wa Mungu akifanya kazi duniani, kupitia maisha ya hao waliyo na Roho ndani yao.

Hatuwezi kupuuza hili.

**Mamlaka ya kisherea au haki huokoa walio dhaifu na kuwatia moyo waliyo kata tamaa**

Kuna picha kwenye kifungu cha 2-4 kwa hao waliyo dhaifu na kukata tamaa. Picha ni ya mshumaa au moto ambao karibu kuzimika. Utahudumia hii kwa uangalifu mkubwa, na uvumilivu na uelewa. Kwa nyakati, miali hubembelezwa kurejea kwenye uzima. Siyo tu kwamba tunajifunza kupitia picha hii ya kushangaza, pia inatufundisha namna ya kuwahudumia walio dhaifu, waliodidimizwa, maskini na waliokata tama.

Hao wanaoteseka, au waliofanya maamuzi mabaya, au walionyonywa na watu hawahitaji laana yetu, wanahitaji msaada wetu. Tumeitwa kama wafuasi wa Yesu kuja pembeni ya hao wanaohitaji mamlaka ya kisheria na haki na kuwabembeleza

kurudi kwenye uzima. Kifungu cha 4 kinasema kuwa Mungu kwa uaminifu wake, bila kuchoka, anataka kuleta mamlaka ya kisheria katika dunia.

Fikiri juu ya historia yetu. Hii ina maana kuwa Tomaida atasaidiwa kutoka kwenye hali hiyo mbaya aliyojikuta ndani yake.

**Mamlaka ya kisheria inahitaji kuwa hali ibadilishwe**
Kutokuwa na mamlaka ya kisheria au haki ni wakati kitu ambacho siyo sawa na siyo halali kimetokea kwa mtu. Hii inaweza kuwa kitu kidogo kama kumwambia mtu mwingine uongo. Inaweza kuwa kitu kibaya kama mtu aliyetekwa, kunyimwa uhuru wao na kuuzwa kama mtumwa. Vyote siyo haki.

Tunaweza kuangalia hali hizi na kuamua kuwa hatuwezi au hatutafanya kitu chochote juu yake. Hii inaweza kuwa rahisi lakini pia siyo sawa na haiwezi kufanya kazi kwa Mungu shalom kwenye dunia hii. Kifungu 5-7 kinatuambia kuwa ni Mungu anayetoa Roho wake na kutupumulia uzima. Hii ni kwa kazi maalum. Ni kuleta mamlaka ya kisheria au haki kwa watu. Tunapaswa kuwaweka wafungwa huru, kuwafungua macho ya vipofu na kuleta uponyaji na tumaini kwenye hali hizo ambazo siyo za haki.

Hii ni moja ya makusudi kwa Roho kwenye maisha yetu. Hatuwezi kupuuza.

**Mamlaka ya kisheia au haki inamwitaji Mungu**
Mamlaka ya kisheria au haki ya kweli ina maana kuwa tunahitaji kufanya kazi na muumbaji wetu kwa kuleta haki kwenye maisha yetu, jumuia zetu, kazi zetu au hali zetu. Mamlaka ya kisheria na haki huenda pamoja; huwezi kuwa na moja bila nyingine. Kwenye kifungu cha 8 kifungu kinamzungumzia Mungu kutotaka kushirikiana utukufu wake na sanamu yeyote. Tunaishi kwenye dunia ambayo watu wengine wanafuata sanamu za aina nyingi. Kutoka kwa miungu ya mawe yaliyochongwa, pesa, watu, kuna miungu mingi ya uongo yanayofuatwa. Kwa kawaida kufuata

miungu hii inasababisha kutokuwepo na haki mahali. Ubinafsi inaongoza kuweka pesa mbele zaidi ya watu kwa mfano.

Kama tunataka kuwawezesha watu kuwa na ujuzi wa mamlaka ya kisheria na haki, basi maisha yetu yajazwe na mamlaka ya kisheria na haki ya muumbaji, Mungu mwenyewe. Bila hili, mamlaka yetu ya kisheria inaweza tu kubadilisha mamlaka moja ya kisheria kwa nyingine. Tunamuitaji Mungu kuleta mamlaka ya kisheria na haki kwenye dunia hii.

Haya ni majaribio ya uzima wa milele. Hao wanaomfuata Mungu kwa kweli, mamlaka ya kisheria na haki itaumba dunia ambayo inakuja kwenye maisha yao ya kila, kila siku kila mahali. Hiyo ni shalom.

**Maswali**

15 Dakika

Kuna idadi ya maswali ya kujadili wiki hii. Swali la kwanza linaweza kujadiliwa kama kikundi chote na swali la mwisho kujadiliwa ndani ya kikundi kidogo.

Maswali ya kikundi chote:

- Uliwahi kuwa mhanga wa kotokuwa na haki? Nini kilichotokea na kujisikiaje? Kuna mtu yeyote aliyekusaidia?
- Kwa nini unafikiri kuwa haki ya Mungu na mamlaka ya kisheria huenda kwa pamoja? Kwa nini tu usiseme unampenda Mungu mpaka pia umpende ndugu au dada yako na hao wanaokuzunguka?

Maswali ya kikundi kidogo (watu wanapaswa kujibu maswali hayakwa pamoja kwenye vikundi vya watu 3 au 4):

- Sisi ni watu ambao ni ‘watumwa’ na walio kata ‘tamaa’, wahanga wa kusosa mamlaka ya kisheria kwenye maisha yetu na pale tunapoishi?
- Tutawafanyia nini?
- Shalom ina maana/kila kitu kiwe kwenye amani humaanisha nini kwenye kijiji chako?

Kwa maswali haya yote, hakikisha kuwa kila mtu anasikiliza na kuelewa wazo la kila mtu na majibu.

10 Dakika

**Shughuli**

Kwa kawaida, kutokuwa na mamlaka ya kisheria au haki huanza kwenye kutokubaliana na magomvi tunayokuwa nayo kwenye maisha yetu wenyewe.

Chukua dakika tano kufikiri nani umekuwa na ugomvi naye, humpendi, hata umemtendea vibaya na hukumtendea vema. Inawezekana kuna mtu umemdanganya au hujamfanyia haki. Inawezekana kuna cha kitu ziada umechukua sehemu na hiyo ikaleta uadui kwenye maisha yenu huko nyuma.

Kwenye kikundi cha watu 3 au 4, kuwa jasiri na kukiri moja kwa mwingine kwenye hali yeyote iliyosababisha ugomvi. Kila mtu amwambie mwezake kile amcho umekifanya kwa kukusudia au kwa bahati mbaya.

Ya pili, mjadili namna ya kuboresha hali hiyo au kurekebisha hali hiyo. Kama mtaweza kufanya, andika hili kwenye kipande cha karatasi: utahitaji baadaye.

10 Dakika

**Maombi**

Kwenye vikundi vyao, mtie moyo kila mtu kujifikiria wenyewe na hali amabyo wamekuwa wakizungumzia juu yake.

- Je tumewaletea watu mamlaka isiyo ya kisheria? Kama ni hivyo tunapaswa kuomba msamaha na kubadilisha njia zetu.
- Mwombe Mungu atusaidie sisi kuona hali na watu wanaohusika na anawaona.
- Mwombe Mungu namna tunavyoweza kufanya marekebisho kwenye kila hali. Kama watu wataweza, watie moyo kuandika chini kile anachosema Mungu.

Maliza kwa kuomba ili mamlaka ya kisheria na haki ije na kumwambia kila mtu kusema kifungu cha kukumbuka kwa pamoja.

**Kufanya wiki hii**

Wiki hii peleka nyumbani kipande cha karatasi ulichoandika wakati wa shughuli na maombi. Ni muhimu kuwa tunatendea kazi yale tunayosikia kuwa Mungu anatuonyesha. Tusiache bila kutenda.

Endelea kuombea hali ilyopo na kumwomba Mungu atukuzwe kwenye hali hiyo, haijalishi kuonekana ngumu namna gani.

**Shahidi**

Wiki hii panga muda kwenda na rafiki 1 au 2 na kurekebisha hali iliyopo. Chochote kile ulichoandika kwenye kipande chako cha karatasi, hakikisha inatokea halisi. Lete mabadiliko ya Mungu kwenye hali.

Nafasi ikipatikana, hakikisha unaeleza kwa nini unarekebisha hali hiyo na vitu ulivyojifunza kwenye kikundi chako wiki hii.

11

# Kuleta Mamlaka ya Kisheria



'Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi.'

Mathayo 25:40

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma Kifungu cha Biblia?

**Wakaribishe na Mrejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila mtu kwa kufika kwenye kikundi.
- Anza kwa maombi, mepesi mafupi.
- Waulize wanakikundi kama wamefanya 'Kufanya wiki hii' na 'Kushuhudia' kazi toka toka wiki iliyopita.
- Wakaribishe washirikieshe chochote walichokijifunza ama kupata ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kutambua hali au mazingira ya kutokuwa na mamlaka ya kisheria au haki kwenye jumuia zetu na kujifunza namna ya kuanza kuwashughulikia wao. Mungu ametuita kupenda familia zetu, na kudhihirisha maisha yetu mapya ndani yake kupitia kuleta mamlakaya kisheria kwa hao walio dhaifu, maskini na kudidimizwa.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na marejeo ya Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Soma tena kwenye vifungu vidogo, ukiachia kikundi kurudia kila kifungu baada yako. Poleploe soma kwenye vifungu virefu kikundi kikirudia kila kipande mpaka kila mtu aweze kukariri kifungu chote. Watie baadhi ya watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

> *Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi.*
>
> *Mathayo 25:40*

Kwenye kipindi cha mwisho tulijifunza juu 'Shalom' (amani anayotoa Mungu mahali kila kitu kiko sawa kwa kila mtu). Tunatambua kuwa vitu haviko kama ilivyopaswa kuwa kwenye jumuia zetu na kwa dunia pana. Tumejifunza juu ya mamlaka ya kisheria na haki na walivyo sehemu ya Mungu ni nani na kwa nini wanahitajika kwenye jumuia zetu.

**Maswali**

Waambie watu washuhudiwe kitu wanachokumbuka toka kwenye kipindi cha wiki iliyopita.

Kwa wiki yote iliyopita tumekuwa tukifikiri juu ya hali kwenye maisha yetu wenyewe na jumuia mahali ambapo hatusikii amani ya Mungu ya ndani (shalom) na Mungu ametuonyesha sisi kuwa mamlaka ya kisheria inatakiwa.

Kutokuwa na mamlaka ya kisheria inaweza kusababishwa na kitu kidogo kama uongo au inaweza kuwa kitu kinachotokea kuwa kubwa, kama mtu kutekwa. Kwa sababu yeyote, mahali pasipokuwa na mamlaka ya kisheria na watu wanateseka.

Kipindi chetu leo kitatusaidia sisi kufikiri namna ya kukabiliana na hali inayotuzunguka mahali watu wanapoteseka kwa sababu ya kutokuwa na mamlaka ya kisheria au haki.

**Hadithi**

Eleza hilo wiki hii tunayo historia 4 za kweli toka Vikundi vya Uzima kule Zambia na Namibia. Soma historia zifuatazo kwenye kikundi:

**Historia 1:** Kikundi cha Uzima kimekuwa kikikutana kwa pamoja kwa muda. Wamekuwa wakishirikisha mawazo juu ya namna ya kuonyesha upendo wa Yesu kwenye jumuia. Wanaposhirikisha mawazo, watu wanakumbuka kona iliyo kali sana kwenye moja ya barabara za vichakani mahali ambapo ajali zimekuwa zikitokea na watu kujeruhiwa. Walihisi kuwa Kikundi cha Uzima kitajaribu

kufanya kitu juu ya jambo hili na kikundi cha watu 12 walitengeneza barabara na kutengeneza njia pembeni. Kuanzia hapo ajali hazikutokea tena!

**Historia 2:** Kikundi cha Uzima kimekuwa kikiombea jumuia yao iliyokuwa ikijulikana kama kanda ya maasi kwa miaka mingi. Kwa mwaka moja Kikundi cha Uzima kimekuwa kikiomba maalum kwa watu waliojulikana kusababisha matatizo na siku moja wakawaalika kuhudhuria kwenye kikundi. Hao wanaosababisha matatizo walikuja na kwa muda walijenga urafiki na washirika wa Kikundi cha Uzima na wakakutana na Yesu. Waliyatoa maisha yao kwa Yesu na wakabadilisha namna walivyokuwa wakiishi. Matokeo yake kiwango cha makosa kikapungua na mtazamo wa kijiji chao kikabadilika kabisa!

**Historia 3:** Binti aliyekuwa na ukimwi alilazimishwa kuishi ukingoni mwa jumuia yao kwa sababu watu walifikiri ni mtu mbaya na hatari. Alisema, 'Nimekuwa nikifikiri kuwa nikiwa, na ukimwi naweza kuwa mtoto wa Mungu.' Watu hawakutaka kumfanyia jambo lolote. Kikundi cha Uzima kwenye jumuia yao walichagua kufanya kitu cha tofauti wakamwalika kuhudhuria kwenye mkutano wao. Alianza kuhudhuria na kujisikia kukaribishwa na kupendwa na akaweza kuzungumzia juu ya vita vyake na ugonjwa. Akawa Mkristo na akampa Yesu maisha yake. Kwa sasa anasema, 'Najisikia furaha ndani yangu ambayo sikuwa nayo huko nyuma.' Kwa sasa anatoka kuwafuatilia hao wanaoteseka na ukimwi na ameunda kikundi cha kusaidia. Wengi wanapata msaada wa matendo na wanafikia kumjua Yesu.

**Historia 4:** Baadhi ya vijana walikuwa walevi wa kupindukia na kusababisha matatizo kwenye familia zao. Walikaribishwa na Kikundi cha Uzima cha mahali na walipojiunga na kikundi kujifunza Biblia waligundua amani na kumpokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yao. Waliacha kunywa na hii imeleta amani kwenye maboma na familia zao. Washirika wa Kikundi cha Uzima chao wamekuwa wakichangia kiasi kidogo cha fedha kwa utaratibu wa kawaida mpaka kufikia kununua nguruwe

kwa pamoja. Baadaye nguruwe alizaa vitoto na Kikundi cha Uzima kikawagawaanyia kwa hao waliokuwa wakiteseka kulipa ada na gharama zingine. Kwa kipindi kirefu nguruwe watazalishana na kuanza kuwapatia kipato familia hizo.

**Kujifunza Biblia**

Soma <u>Yakobo 1:19-27</u> kwenye kikundi:

> *[19]Hayo mnajua, ndugu zangu wapenzi. Basi kila mtu na awe*
> *mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala*
> *kukasirika; [20]kwa maana hasira ya mwanadamu haiitendi*
> *haki ya Mungu. [21]Kwa hiyo wekeeni mbali uchafu wote na*
> *ubaya uzidio, na kupokea kwa upole neno lile lililopandwa*
> *ndani, liwezalo kuziokoa roho zenu.*
>
> *[22]Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali*
> *mkijidanganya nafsi zenu. [23]Kwa sababu mtu akiwa ni*
> *msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu*
> *anayejiangalia uso wake katika kioo. [24]Maana hujiangalia,*
> *kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo. [25]Lakini*
> *aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo,*
> *asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo*
> *atakuwa heri katika kutenda kwake.*
>
> *[26]Mtu akidhani ya kuwa anayo dini, wala hauzuii ulimi wake*
> *kwa hatamu, ili hali akijidanganya moyo wake, dini yake*
> *mtu huyo haifai. [27]Dini iliyo safi, isiyo na dosari mbele za*
> *Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane*
> *katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.*

**Maswali**

5
Dakika

Kwenye kikundi cha watu 3 au 4, mwambie kila moja kujibu maswali yafuatayo kuhusu kifungu cha Biblia:

- Tunajifunza nini kuhusu Mungu?
- Tunajifunza nini kuhusu sisi wenyewe?

- Kifungu hiki kinatuambia nini cha kufany?

Kirudishe kikundi kwa pamoja na uulize kila kikundi kushirikisha jibu moja kwa kila swali.

3
Dakika

**Shughuli**

Waulize kikundi kama kuna mtu yeyote aliyewahi kujiangalia kwenye kioo au picha hivi karibuni.

Mchukue mtu aliyewahi kufanya hivyo halafu waambie waeleze wanaonekanaje. Muulize kila mtu kwenye kikundi kama wametoa maelezo mazuri. Rudia mazoezi haya na mwingine aliyejitolea.

Kifungu cha Biblia tulichokisoma na kujadili pamoja inatupa mfano wa mtu anayejiangalia kwenye kioo na kusahau anavyoonekana. Hii itaonekana kuwa ni jambo la kipuuzi kwetu! Lakini hivyo ndivyo tunavyokuwa tunaposoma Biblia; tunaitazama, ghafla tunasahau au kupuuza kinachosema, na kile kilichotuuliza. Kifungu kinaweka wazi kuwa Mungu anataka maisha mapya aliyotupa ituhusishe kuchukua hatua.

Kifungu kinaanza kwa kusema tunapaswa kuachana na kila kitu kilicho kibaya kwenye maisha yetu na kwa unyenyekevu kukubali kile ambacho Mungu amepanda ndani yetu (kifungu 19 -20). Kumbuka siyo matendo yetu ndiyo yalimetuokoa. Mungu amepanda maisha mapya ndani yetu kupitia kwa Yesu. Hata hivyo, baada ya kupokea zawadi hii kutoka kwa Mungu, tunapaswa kuhakikisha ‘kusafisha’ kila kitu kisicho safi kwenye maisha yetu.

Kifungu kinaendelea kuelekeza kufanya yale aliyosema Mungu kwenye neno lake (kifungu 22 -25). Kwa kufurahisha, kuna ahadi 2 kwenye kifungu 25. Kwanza, tumeambiwa kuwa neno la Mungu linatoa uhuru. Ya pili, tumeambiwa kuwa kila anayelisikia neno na kuchukua haatua kwa kile alichokisikia atabarikiwa kwa kila

nalolifanya. Iko wazi kuwa Mungu anatutaka kujifunza neno lake na kuliweka kwenye mazoezi.

Mwishoni tunasoma kuwa dini ya kweli inaonekana kama kitu fulani: kuwa mwangalifu katika kile tunachokisema, kuwajali yatima na wajane na kuwa tofauti kwa jamii inayotuzunguka (kifungu 26 27). Mungu anatuambia kuishi maisha tofauti ya namna fulani kwa watu wengi wanaotuzunguka. Anatuambia kusimama kwa hao ambao hawawezi kusimama wenyewe, kufanya kazi kuleta mamlaka ya kisheria.

Tunaenda kutumia historia tuliyosoma mapema kutusaidia kufikiri hii inaweza kuwa na maana gani kwetu na kwa jumuia zetu.

20 Dakika

**Shughuli**

Gawanya kikundi kwenye vikundi 4 vidogo. Kipatie kila kikundi 1 ya historia tuliyosoma juu ya Kikundi cha Uzima. Kila kikundi kinapaswa kuwa na historia tofauti.

Vikundi vinaweza kutaka kusoma historia hiyo tena. Wanaweza kuandaa mchezo wa kuigiza fupi (urefu wa dakika 1 au 2) kueleza historia. Mpe kila moja dakika 5 kuandaa mchezo wa kuigiza.

Moja baada moja, kiambie kila kikundi kuigiza igizo kwa kila mtu. Baada ya kila historia kufanywa, jibu maswali yafuatayo:

- Kwenye historia hii, ni nani aliyekuwa akiteseka kwa sababu ya kukosa haki kwenye jumuia?
- Tunajisikiaje na tunafikirije Mungu anajisikiaje juu ya kukosa haki?
- Kikundi cha Uzima kilichukua hatua gani?
- Matokeo yake ni nini?

Baada ya kila kikundi kufanya historia yao na maswali kujadiiwa, kusanya pointi za muhimu ambazo zimerudiwa mara kwa mara.

?

20
Dakika

**Maswali — Nini inatokea kwenye jumuia yetu?**

Waulize watu wote kama kuna kukosa haki na kudidimizwa kwenye jumuia zao.

Baadhi ya mifano ni:

- Mtu anayetenda tendo ambalo ni rahisi kuadhirika
- Kuna mtu anayewadanganya watu juu ya fedha
- Watu wananyanyaswa
- Mtu hatimizi wajibu wake kwenye jumuia kamili
- Afisa mpenda rushwa na mwenye kuanzisha matatizo
- Mtu mwenye ujuzi wa vurugu za ndani
- Mzee aliyeachwa na familia yake

Mjadili maswali haya wazi. Inawezekana kuwa unahitaji kuchochea na kuwasaidia watu kujadili haya. Unahitajika kuwa mvumilivu na kuwatia watu moyo kuwa waaminifu na majasiri.

Ikiwa hali fulani imewekwa wazi, mjadili kama kikundi chote. Ikiwa idadi ya hali tofauti zimesemwa, unaweza kuganya vikundi vidogo ili waweze kujadili.

Mjibu maswali haya kwa pamoja:

- Tunajisikiaje juu ya hali hii na tunafikiri Mungu anajisikiaje juu ya hali hii?
- Nini kitatokea ikiwa hatufanyi lolote?
- Ni hatua gani tunawe kuchukua kufanya jambo juu ya hayo pamoja? Kwa mfano, itasaidia kuzungumza na kumpa changamoto mtu mwingine? Ni lazima kufanya jambo kuwazuia wao wasinyonywe? Je kuna mtu kwenye mamlaka anayeweza kusaidia?

Panga mpango wa kufanya kitu Fulani juu ya hali hiyo na ujitoe kufanya kwa pamoja. Ni jambo la muhimu kuwa tendo hili halikufanyi kuwa mzembe au kumweka mtu yeyote kwenye hatari. Kwa mfano, usiende na kumkabili mtu mwenye makosa ya

jinai; ni bora kuwahusisha wenye mamlaka. Jambo la muhimu la kukumbuka ni kwamba tulete mamlaka ya kisheria Mungu na haki na kubadilisha maisha ya watu.

**Maombi**

15 Dakika

Leo tuanenda kuomba kwa hali tuliyozungumzia na kwa mipango tuliyopanga. Tunaweza kumwomba Mungu atutangulie, na kwamba atatupa ujasiri na kwamba ataleta mamlaka yake ya kisheria na haki kwenye hali tuliyojadili.

Ikiwa umetengeneza mpango kama kikundi, basi omba namna hii:

- Simameni kwenye mduara na umgeukie mtu kushoto kwako.
- Mwombee mtu huyo wakati wanatafuta kuleta mamlaka ya kisheria Mungu na haki kwenye jumuia yako.

Ikiwa umetengeneza idadi ya mipango kama vikundi kidogo, omba namna hii:

- Kila kikundi kinapaswa kusimama, kikundi kimoja kwa wakati, na kushirikisha mipango yao kwa kifupi. Watu wote wengine wasimame wakiwazunguka na kuwaombea wakati wanaweka mipango yao kwenye matendo. Fanya haya kwa kila kikundi.

**Kufanya wiki hii**

Katika siku 2 au 3 zinazofuata, kutana na watu kwenye kikundi chako cha mwisho leo na kuomba tena kwa hali ambayo Mungu ameweka kwenye moyo wako. Chukueni muda kwa pamoja mkiangalia mipango yenu na kuanza kuchukua hatua kufanya kitu kwa ajili ya hayo. Pengine utahitaji kuwasiliana na mtu fulani au weka vitu vingine kuwa tayari.

**Shahidi**


Shahidi wiki hii ni kuweka mipango yetu kwenye matendo. Kuwa mwangalifu na makini kwa mahitaji ya watu na hisia zao na kuwaweka na wewe mwenyewe sehemu salama. Kumbuka kuwa


ni muhimu tendo hili lisikuweke wewe au mtu mwingine kwa uzembe kwenye hatari.

Jambo la kufanya wiki hii linaweza kuwa ni mwanzo tu. Unaweza kuwa unahitaji kuendelea kuwajali wale ambao Mungu amewaweka ndani ya moyo wako.

**Nyongezo ya Vifaa**

Kifaa kizuri cha kukusaidia kuleta haki kwenye jumuia yako ni ***Penda Kijiji Chako***. Ni kozi yenye mafundisho 10 ambayo mnaweza kufanya kama kikundi na inapatikana Dignity au Timu yenye Mvuto ya Mwanachama wa Dignity (www.dignityonline.org.uk/love-your-village).





12

# Kuwasaidia Wengine Kukua

'Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho.'
Wagalatia 6:9

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma Kifungu cha Biblia?

**Wakaribishe na Mrejesho**

5
Dakika

- Mshukuru kila mtu kwa kufika kwenye kikundi.
- Anza kwa maombi, mepesi mafupi.
- Waulize wanakikundi kama wamefanya 'Kufanya wiki hii' na 'Kushuhudia' kazi toka toka wiki iliyopita.
- Wakaribishe washirikieshe chochote walichokijifunza ama kupata ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kujifunza kuwa tunaweza kuwasaidia wengine kukua, watu binafsi na ndani ya jumuia. Kama Mungu anavyofanya kukuza maisha yake mapya ndani yetu, anatutumia pia sisi kusaidia kukuza maisha mapya ndani ya wengine.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5
Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na marejeo ya Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Soma tena kwenye vifungu vidogo, ukiachia kikundi kurudia kila kifungu baada yako. Polepole soma kwenye vifungu virefu kikundi kikirudia kila kipande mpaka kila mtu aweze kukariri kifungu chote. Watie baadhi ya watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

> *Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho.*
>
> *Wagalatia 6:9*

**Hadithi**

Wasomee hadithi inayofuata kikundi:

Mkulima alimpa kijana wake mdogo kipande cha ardhi na kiasi cha mbegu. Kijana alifurahi sana! Alijiambia mwenyewe, ‘Mbegu zangu ni za dhamani na sitaki kuzipoteza hivyo nitatafuta boksi nitunze ndani yake.’

Kijana alipata boksi na kuweka mbegu zake ndani na kuzitunza kwenye kipande cha ardhi yake. Kila siku alizitazama mbegu zake za dhamani lakini hazikuwa zinakuwa. Hivyo alienda kwa baba yake na kumwonyesha mbegu zake. Baba yake alitabasamu na kusema, ‘Mbegu yako inahitaji mwanga kukua. Ukitunza ndani ya boksi, haziwezi kuona jua na hazitaweza kukua.’ Hivyo kijana akachukua mbegu nje ya boksi na kuweka kwenye udongo kwenye jua na kuzitazama kama zitakuwa.

Lakini ndege wakubwa na wanyama wadogo wakaja na kujaribu kuiba mbegu. Kijana akapiga kelele na kupunga mikono yake kwa wezi na kuwafanya kuondoka. Baba yake aliona jambo hilo na kusema, ‘Mbegu zako zinaonekana kupandwa kwenye udongo wa kukua. Udongo utalisha na ndege hawataweza kuziiba.’ Hivyo kijana akaotesha mbegu kwenye udongo, mbali mbali. Baba yake alimwangalia na kumwambia kwa upole, ‘Panda mbegu karibu na zingine ili zinapokuwa ziweze kusaidiana wakati upepo ukivuma.’ Hivyo kijana akaotesha mbegu zake karibu na zingine na kuzisubiri kukua. Lakini hazikukua!

Alikuwa na huzuni akaenda kwa baba yake na kumwuuliza kwa nini mbegu hazikui. Baba yake akajibu, ‘Unapaswa kuzipa mbegu zako maji kila siku.’ Hivyo kijana akamwagia mbegu zake maji kila siku. Lakini baada ya wiki chache, hakuna kilichotokea! Kijana akawa na huzuni. ‘Mbegu zangu hazikui,’ kijana alilia. ‘Ah, lakini unapaswa kuwa mvumilivu, inachukua muda kwa mbegu kukua.’

Baada ya muda mbegu kwa kweli zilianza kukua. Kijana akawa na furaha. Lakini wadudu wakaja na kuanza kudonoa majani na kijana akapiga kelele. Baba yake akaja na kumwambia, ‘Unapaswa kuhudumia mbegu zako na kuwaondoa wadudu juu ya majani au sote zitaliwa.’ Hivyo kijana akawaondoa wadudu juu ya majani na

mimea ikaendelea kukua. Zilikuwa zikiwa na nguvu na kurefuka kwenye mwangaza wa jua na kijana akamwagia maji kila siku. Upepo ulipovuma mimea ikaelea kwa pamoja na kupeana msaada.

Halafu siku moja matunda yakatokea. Baba wa kijana akamwambia, ‘Umeona matunda kijana wangu. Hapa kuna mbegu zaidi. Unaweza kuziotesha wakati mwingine na utakuwa na mimea mingi.’ Kijana alifurahi kwa kweli! Akamwambia baba yake, ‘Ndiyo nitafanya. Na kwa sasa nimejua kuwa mbegu zangu zinahitaji mwanga zing’are juu yake na udongo wa kuzirutubisha. Zinapaswa kuwa karibu ili kupeana kivuli kutokana na upepo na napaswa kuhakikisha majani yako safi wadudu wasidonoe. Na lazima niwe mvumilivu na mbegu zangu zinazochukua muda kukua. Sasa najua namna ya kukuza mbegu zangu ziwe na nguvu na kurefuka na siku zote nitakuwa na mbegu za ziada.’ ‘Kijana wangu,’ alisema baba yake mwema, ‘sasa uko na hekima na mbegu zako zitakua na kuwa na nguvu na kurefuka.’

Historia hii inaelezea namna mbegu zinavyohitaji mazingira sahihi ziweze kukua vizuri. Kama Wakristo tunakuwa vizuri wakati tunapokuwa na ushirika pamoja na Yesu. Tunafanikiwa kwenye mwanga wa kweli ya Mungu, na kulishwa na Mungu na kuhudumiana.

**Kujifunza Biblia**

Soma Matendo 2:42-47 kwenye kikundi:

> [42]*Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika*
> *ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.* [43]*Kila*
> *mtu akaingiwa na hofu; ajabu nyingi na ishara zikafanywa*
> *na mitume.* [44]*Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja,*
> *na kuwa na vitu vyote kishirika,* [45]*wakiuza mali zao, na vitu*
> *vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote*
> *kulingana na haja ya kila mmoja.* [46]*Na siku zote kwa moyo*

*mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe, [47]wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.*

10 Dakika

**Shughuli**

Tengeneza matendo fulani ambazo zitaelezea shughuli tanao zilizoorodheshwa hapo chini. Kwa mfano, kuabudu ni kusimama na kuinua mikono juu na kuabudu. Halafu ziweke zote pamoja kuonyesha kile walichokifanya waumini wa kwanza kwenye kifungu cha Biblia kwenye kitabu cha Matendo.

- Kusoma Biblia pamoja
- Kushuhudia maisha yetu
- Ukarimu na kuwahudumia wengine
- Maombi
- Kuabudu

Sasa soma kifungu tena na kumwambia kila mtu kutenda tendo walilolitengeneza kwa wakati muafaka kwenye kifungu.

Tuliangalia kifungu hiki kabla kwenye Kipindi cha 1 ya ***Maisha Huumba***. Inatupa picha ya jumuia. Wakati kifungu hiki kikiandikwa, Yesu tayari alishachukuliwa mbinguni na wafuasi wa Yesu walijazwa nguvu za Roho Mtakatifu kwa nguvu ya namna ya pekee. Moja wa wafuasi wa Yesu, Petro, alihutubia mkusanyiko na watu kama 3,000 walibatizwa kwa matokeo ya kusikiliza ujumbe wake. Kwenye kifungu hiki katika kitabu cha Matendo tunaona jinsi hawa Wakristo wapya **walivyokuwa pamoja** kwa upendo wao wa kumpenda Yesu na kupendana wao kwa wao.

Waamini walitambua kuwa waliunganishwa kiroho moja kwa mwingine na kwa Mungu, hivyo walihakikisha kuwa wanakutana pamoja kila siku kuimba na kumwabudu Mungu, wakisikiliza mafundisho ya neno la Mungu, wakiomba, wakihudumiana,

wakila pamoja na kushuhudiana juu ya maisha wao kwa wao. Walielewa kuwa kuunganika kwao ni kwa kipitia Yesu Kristo. Walishuhudiana maisha yaliyojengwa juu ya mahusiano yao na Yesu, wakishirikiana pamoja kwa kuleta njia za mbinguni za Mungu hapa duniani. Wote walizaliwa mara ya pili kwenye familia ya Mungu. Walijawa na furaha na kuwa wakarimu kwa wengine. Miujiza ilitendeka! Kila siku watu zaidi waliamua kumfuata Yesu na kuungana na kikundi chenye furaha.

**Mafundisho**

Kwenye kifungu cha 42 tunasoma kuwa Wakristo wapya walisikiliza kwa uangalifu mafundisho ya hao waliokuwa pamoja na Yesu. Tunapokutana pamoja kama waamini tunasikiliza mafundisho ya Yesu na mitume kupitia kusoma Biblia kwa pamoja na kumwomba Roho Mtakatifu wa Mungu kuzungumza na mioyo yetu na akili zetu kupitia maandiko. Halafu tunakuwa kwenye uelewa wetu. Mungu anafungua macho yetu na mioyo yetu kwake zaidi na zaidi na tunaanza kusikia sauti yake sisi wenyewe.

**Kukutana na kula**

Kama waamini wa mwanzo, tutafungua maboma yetu ili tuweze kukutana pamoja kumwabudu Mungu, kula pamoja, na kumega mkate pamoja (kifungu cha 42) kama jinsi alivyotuelekeza Yesu wakati wa chakula cha mwisho kabla ya kuteswa (Luka 22:19-20). Chakula cha waaminio wapya ilikuwa sherehe, iliyojaa furaha badala ya kuwa wajibu (kifungu cha 46). Furaha hutfanya kuwa na nguvu na kutusaidia kumfuata Yesu sehemu zote za maisha yetu.

Tunapokutana na wengine na kukumbushana yale ambayo Mungu anayafanya kwenye maisha yetu, tunatiwa moyo na imani yetu kukua. Tunajifunza kuwapenda ndugu na dada zetu ndani ya Kristo. Wakati mwingine hiyo inaweza kuwa changamoto kwa sababu watu wengine wanaweza kusumbua au kubatilisha kama kwenye familia zingine za watu! Lakini Mungu ametuita tuwe waungwana na wavumilivu maana yeye yupo pamoja nasi. Tunapojifunza haya tunakua zaidi na kufanana na Yesu.

**Maombi**
Waaminio walijitoa pia kwa ajili ya maombi (kifungu cha 42). Yesu aliomba na tunaomba. Tunaongea na Mungu, ambaye ni Baba yetu mzuri, tukimsifu yeye, kumshukuru na kumwomba kutusaidia. Tunapoomba, urafiki wetu na Mungu unakua na tunapoomba pamoja kama waaminio, tunakua pamoja na tunafurahi wakati tunapoona majibu ya maombi yetu. Maombi ya waaminio pamoja yana nguvu kutubadilisha na hali tunayokabiliana nayo.

**Kuabudu**
Wakristo waliabudu pamoja kila siku. Walikutana mahali pa kuabudu na pia kwenye maboma yao. Tunapoabudu, tunapata ujuzi zaidi wa uwepo wa Yesu wa ajabu ambaye siku zote yuko pamoja nasi. Mungu anapenda kuabudu kwetu na anajua ni vizuri kwetu pia! Tunapohisi uwepo wake, tunatiwa nguvu, imani yetu inaongezeka na tunafahamu kuwa tunapendwa. Tunafunikwa na utukufu wa Yesu (kifungu cha 43) kwenye muktadha huo tunaona ishara kutoka kwa Mungu na miujiza inatendeka (kifungu cha 43).

**Ukarimu na kutumikia**
Waaminio walijulikana kwa kuwa wakarimu (kifungu cha 45-46). Tafsiri zingine za Biblia zinaandika kuwa waamini walikuwa na mioyo ya safi. Moyo msafi ni ule wa kweli na uko wazi. Tunapenda kuwa wa kweli kwa ndugu na dada zetu katika Kristo na kutoa kwa moyo wa kupenda. Waamini wa kwanza walishiriki maisha yao, chakula chao, maboma yao na mali zao. Waliwasaidia waliokuwa na shida. Waliwasaidia waaminio ambao hata hawajawahi kuktana nao. Ikiwa tunacho kingi au kidogo, tunaweza kushirikiana na wengine. Tunaweza kuwa wakarimu pia kwa muda wetu, uvumilivu wetu, na upendo wetu. Tunakuwa wakarimu kwa wengine kwa sababu Yesu alikuwa mkarimu sana kwetu. Tunapowatumikia wengine, kama alivyofanya Yesu, tunaweza kusahau juu ya shida zetu na tuanapowabariki wengine, Mungu hutubariki kwa njia nyingi. Kwa kurudishiwa, tunapokea msaada na kutiwa moyo toka kwa ndugu na dada zetu na tunabarikiwa tena.

Kifungu hiki kwenye kitabu cha Matendo kinatuonyesha sisi kila moja anamuhitaji mwingine ili kukua na kuwa na afya njema. Halafu tunakua pia kama watu binafsi na jumuia zetu zitakuwa wakati watu zaidi wanapounganika na sisi. Upendo ndiyo ufunguo. Yesu alisema, ‘Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi’ (Yohana 13:35).

**Utume na Wajibu**

Nidhamu inahitajika kuwa kwenye jumuia ya namna hii. Wakati mwingine hatutaki kukutana pamoja, tabia ambayo kifungu chetu cha kukumbuka kinatuonya kinyume. Kwa nyakati zingine tunaweza kuwa ‘tumechoka kwa kutenda mema’ kama inavyosema kwenye kitabu cha Wagalatia 6:9. Kwa nyakati kama hizi tunapojisikia kuchoka na kuvunjika moyo, inaweza kutujaribu kujiweka mbali na jumuia yetu mpya na hata kuwa na mashaka na maisha yetu mapya. Ni katika nyakati hizi maalumtunawahitaji waamini wenzetu kutusaidia sisi, kutupa msaada, kututia moyo na hata wakati mwingine inakuwa changamoto tunapokuwa kwenye makosa. Ni jambo la muhimu kuwa vitu hivi vyote vinafanyika kwa upendo na siyo toka kwa moyo mbaya. Kwa njia hiyo ambayo Yesu alitumia muda mwingi na kikundi kidogo cha watu aliyowapenda mno, akiwafundisha na kuwapa changamoto, hivyo tunapaswa kulenga kufanya hivyo. Ni muhimu kuwa sehemu ya kikundi, kama kikundi hiki, tunapoweza kusoma na kujifunza pamoja, kuabudu pamoja, kukua katika upendo na kuwa na matendo mema pamoja, na kusaidia na kutiana changamoto wakati mambo ni magumu. Kama kijana kwenye historia yetu alivyotakiwa kuwa na udongo, maji na jua kwa kuotesha mbegu zake, hivyo tunapaswa kusaidiana kukua katika Yesu. Kupitia kuangalia mazingira na maendeleo yetu na ya wengine, tunaweza kusaidia na kutoa msaada kwa kadri tunavyoweza.

?

**Maswali**

15 Dakika

Kwenye kikundi cha watu 3 au 4 jadilini maswali yafuatayo. Mara watu watakapokuwa na wakati wa kujadili maswali haya, rudisha

kikundi pamoja na kuwaambia watu kushirikisha baadhi ya majibu yao.

- Roho Mtakatifu wa Mungu anakuambia nini kuhusu kifungu hiki cha Biblia?
- Ni kwa njia zipi jumuia yako ya waaminio inafanana na ile ya Wakristo wa Kanisa la kwanza? Mnawezaje kupendana zaidi?
- Ni vitu vya aina gani vinakuzuia kukua kwenye imani yako? Mnaweza kusaidiana namna gani ilimkushinda vitu hivyo?

**Maombi**

15 Dakika

Soma maombi haya kwa sauti:

> ‘Mungu mkuu sana, Baba yetu wa Mbinguni, wewe ni mkarimu sana na mvumilivu kwetu kwa sababu wewe ni Baba mzuri na sisi ni watoto wapendwao. Aksante kwa sababu Roho wako Mtakatifu anafanya kazi ndini yetu kutukuza kuwa Wakristo waliokomaa. Aksante kwa sababu umetupa kaka na dada katika Kristo kusaidia na kututia moyo tuweze kukua. Tafadhali tuasidie tuweze kukua pamoja: kukutana pamoja, kusoma maandiko pamoja, kutumikia na kuwa wakarimu na kuabudu na kuomba pamoja. Tusaidie kutina moyo kwa kupendana na kuwa na matendo mema. Tunaomba haya kwa jina la Yesu, aksante.’

Sasa kitie moyo kikundi kuomba kwa pamoja juu ya vitu ambavyo mmekuwa mkizungumzia juu yake leo. Watie moyo kuomba kuelekea jambo lolote lililosemwa.

**Kufanya wiki hii**

Kila wiki kuna kazi ya nyumbani sisi kufanya. Wiki hii, panga kukutana na mtu 1 au 2 toka kwenye kikundi chako na fikiri juu ya maswali haya kwa pamoja:

- Ni sehemu zipi za maisha yangu natakiwa kukua zaidi?

- Nitafanya nini kusaidia haya kutokea?
- Tunaweza kusaidiana namna gani kukua kwenye maeneo haya wiki hii?

Shirikisha majibu yako wengine, waombee na kujitoa kuchukua hatua. Fuatilia kwa kusaidiana na kulizana kama mmefanya vitu vile mlivyopaswa kujitoa kufanya.



**Shahidi**

Fikiria juu ya baadhi ya watu ambao ulizungumza nao huko nyuma au mmeunganika kama sehemu ya shughuli ambayo tumekuwa tukifanya. Waombee na wakati unaomba mwombe Mungu akuonyeshe ni yupi kati yao anahitaji kutiwa moyo na wewe wiki hii. Nenda kutana na mtu huyo, uwe na muda nao, wasikilize na kuwatia moyo – utakuwa unawasaidia kukua.



13

# Ufupisho wa Kipindi

'Dini iliyo safi, isiyo na dosari mbele za Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.'

Yakobo 1:27

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu yeyote kwenye kikundi kusoma Kifungu cha Biblia?

**Wakaribishe na Mrejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila mtu kwa kufika kwenye kikundi.
- Anza kwa maombi, mepesi mafupi.
- Waulize wanakikundi kama wamefanya 'Kufanya wiki hii' na 'Kushuhudia' kazi toka toka wiki iliyopita.
- Wakaribishe washirikieshe chochote walichokijifunza ama kupata ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kujikumbusha juu ya mawazo makuu ambayo tayari tumekwisha jifunza kwenye ***Misingi 3: Maisha Huumba***. Tutatazama pia mbele kwa kile kitakachotokea kwenye ***Misingi 4: Maisha Hukomaa***.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na marejeo ya Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Soma tena kwenye vifungu vidogo, ukiachia kikundi kurudia kila kifungu baada yako. Poleploe soma kwenye vifungu virefu kikundi kikirudia kila kipande mpaka kila mtu aweze kukariri kifungu chote. Watie baadhi ya watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

> *Dini iliyo safi, isiyo na dosari mbele za Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.*
>
> *Yakobo 1:27*

**Hadithi**

Kuna historia ya zamani inaitwa 'Kijana aliyelia kuwa kuna mbwa mwitu.'

Miaka mingi ilyopita kwenye kijiji kidogo milimani aliishi kijana mdogo. Alikuwa akichunga, akiwatazama kondoo wa baba yake. Wanakijiji wote walikuwa wakielekea kwenye shughuli zao za kawaida siku moja wakati huyo kijana alipokuja akikimbia huko kijijini akipiga kelele, “Mbwa mwitu! Mbwa mwitu!”

Watu wa kijiji hicho kwa haraka sana waliacha kile walichokuwa wakifanya na kukimbia kwa pamoja kule mashambani walikokuwa wakilisha kondoo, ili waweze kumfukuza mbwa mwitu na kuokoa kondoo. Hata hivyo walipofika hapo hawakuona ishara yeyote ya kuwepo kwa mbwa mwitu, na kondoo walikuwa wakilisha kwa furaha.

Kijana huyo mdogo alipendezwa kuwa kilio chake chepesi kiliweza kuwa sababisha wanakijiji wote kukimbia kuzunguka na kuacha kile walichokuwa wakifanya.

Siku chache baadaye alikuwa mashambani tena. Akijisikia kidogo kuwa mpweke na kutaka kitu cha kumfurahisha tena alijaribu mtego ule tena. Alikimbilia kule kijijini akilia, “Mbwa mwitu! Mbwa mwitu!”

Wakati huu ni wanakijiji wachache tu ndiyo waliyoitikia wakakimbilia kule kulikokuwa na mifugo pamoja naye kumsaidia kufukuza mbwa mwitu. Baada ya kugundua kuwa waliingizwa kwenye mtego tena, wanakijiji hawakuwa na furaha tena na kijana. Siku chache tena zikapita; muda huu, wakati kijana akichunga kondoo kijana kweli akawaona mbwa mwitu wakiwafuata kundi la kondoo. Kwa mshutuko mkubwa alikimbilia kijijini, akipiga kelel na kulia, “Mbwa mwitu! Mbwa mwitu!”

Wanakijiji wote walimtazama bila kumwamini.

“Unategemea sisi kukuamini tena wakati huu – hapana! Hatutaangukia kwenye mtego wako tena.”

Kijana alikubali na kuomba lakini hakuna mtu aliyemwamini, hivyo alikimbia kurudi kwenye mifugo lakini alikuwa amechelewa. Kondoo wote walishambuliwa na mbwa mwitu: mifugo hawakuwepo tena.

Kwa vile kijana alidanganya mara nyingi kwa kuwaingiza watu kwenye mtego, hawakuweza kumwamini wakati kweli aliwaambia ukweli.

**Kujifunza Biblia**

Soma Yakobo 2:14-18 kwenye kikundi:

> *[14]Ndugu zangu, yafaa nini, mtu akisema ya kwamba anayo imani, lakini hana matendo? Je! Ile imani yaweza kumwokoa? [15]Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki, [16]na mmoja wenu akawaambia, Nendeni zenu kwa amani, mkaote moto na kushiba, lakini asiwape mahitaji ya kimwili, yafaa nini? [17]Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake.*
>
> *[18]Lakini mtu atasema, Wewe unayo imani, nami ninayo matendo.*
>
> *Nionyshe imani yako pasipo matendo, nami nitakuonesha imani yangu kwa njia ya matendo yangu.*

Imani yetu siyo ya maneno tu, lakini ni ya matendo pia. Kifungu chetu leo kinatukumbusha kuwa maneno yetu na matendo yakubaliane, ama ziwe, kama historia ya yule kijana, inawezekana watu wasiamini maisha yetu katika Yesu. Kama tukisema kitu na hatufanyi lolote, hilo linaleta swali kusema ni kwa kiasi gani tunaamini kile tunachokisema, na ni kwa kiwango gani tunataka Mungu atubadilishe na kututumia kubadilisha jumuia yetu.

15 Dakika

**Shughuli: Kweli 2 na Uongo 1**

Unawafahamu kwa kiwango gani hasa hao walioko kwenye kikundi chako? Chezeni mchezo mfupi wa kuigiza kujua!

Mwambie kila mtu kufikiri mambo 2 kwao wenyewe ambayo ni kweli halafu ufanye kitu 1 juu yao wenyewe ambayo siyo kweli (hii inaweza kuwa kitu sirias au kitu kibaya).

Kigawanye kikundi kwenye vikundi vidogo vya watu 3 au 4. Wazungumze kwa kugeukiana, kila moja anapaswa kumweleza mwingine kwenye kikundi mambo 3 yanayomhusu. Watu wengine kwenye kikundi wanapaswa kujaribu na kujua lipi lililo kweli na lipi la uongo.

Kwenye kitabu hiki chote, ***Maisha Huumba,*** tumekuwa tukitazama njia ambazo imani yetu itabadilkisha maisha yetu kwa uhalisi na jumuia zetu pia. Kwenye kifungu chetu cha kukumbuka Yakobo anatuambia kuwa 'dini ya kweli' ni hiyo inayofanya jambo fulani; kwa mawazo yake inawasaidia watu maskini na walioadhirika kwenye jamii zetu. Imani yetu siyo kitu cha kibinafsi cha kutunza kwa ajili yetu wenyewe. Siyo kitu cha akili kwamba itakaa ndani ya fahamu zetu. Ni kitu cha kutenda inayopasa kutuongoza kufuata mifano ya Yesu aliyodhihirisha, kutusaidia sisi kutoka nje kuwafuata hao walioko kwenye jamii zetu hao hasa wanaohitaji maisha mapya anayopeana Yesu. Kwa njia hiyo Yesu anaweza kutubadilisha na siyo sisi tu, lakini pia hao wanaotuzunguka.

**Kutazama nyuma *Misingi 3: Maisha Huumba***

Kwenye kitabu hiki cha tatu kwenye mtiririko wa ***Misingi*** tumetazama ukweli kuwa Mungu yupo kwenye jumuia, na ametuita kuungana naye kama sehemu ya jumuia. Tunapopokea maisha yake mapya tunaunganika na familia yake; tunakuwa ni sehemu ya hiyo anayosema mwili wake. Familia hii na mwili ni sura ya kanisa. Hii ina maana kuwa sote tuko tofauti, tuanataka wote kufanikiwa na kukua. Kila moja wetu amepewa karama, na anayo nafasi ya kupokea kipawa cha kiroho kusaidia mwili kukua

na kupanuka na pia kusaidia jumuia zetu na hao tunaotumia muda pamoja. Hii inatuhitaji sisi kufanyia mazoezi imani, ambayo wakati tunatumia, inakua zaidi na zaidi.

Wakati mwingine tunatumia muda kutazama Vita vya Kiroho na namna ya kujitetea wenyewe na pia kupigana kinyume na mipango ya adui, shetani. Kama sehemu ya kipindi hiki tunatumia wakati mwingine muda kuombea wengine kugeuka na kuacha vifungo vya kiroho vilivyowafunga ambavyo siyo vya Mungu, na kumwamini kutuweka huru. Tulijifunza pia namna ya kuombea jumuia zetu, kwa hao tunaokutana nao tunapotoka. Tulifanya mazoezi ya kushirikishana historia zetu ili tuweze kuwa mashahidi wa Mungu katikati ya marafiki zetu, familia na hata zaidi mashambani.

Kufikia mwishoni mwa kitabu tulifafanua pia fikra ya mamlaka ya kisheria ya Mungu, tukitazama namna ya kunyang'anya tabia ya kisicho haki pamoja na mamlaka yetu ya kisheria isiyo sawa tunayoona ikituzunguka mahali na zaidi mashambani. Mwishoni, tumetazama namna ya kucheza sehemu yetu kwa kuwasaidia wengine kukua kwenye maisha yao mapya, kwa vile tumepata ujuzi wa kukua pia.

20 Dakika

**Maswali**

Sasa tutatazama nyuma kwenye vipindi 12 vilivyopita kwenye ***Misingi 3: Maisha Huumba*** na kuchukua muda fulani kujadili kwenye vikundi vidogo mafundisho yaliyo makuu uliyojifunza.

Kwenye kikundi cha watu 3 au 4, shirikisha baadhi ya ujuzi uliyonayo wa kushuhudia hao walioko kwenye jumuia yako ukijumlisha ujuzi huo wa yaliyokuwa na changamoto.

Mwishowe, mjaribiane kwenye vifungu vya kukukumbuka 13 (ukinganisha na ya leo) na uone kama utaweza kusaidia mwingine kukukumbuka maandiko ambayo tayari tumekwisha jifunza.

Ikiwa kutakuwepo na muda, mjadili ni ipi kwenye vifungu hivi umepata kuwa inasaidia au imeongea na wewe kwa njia fulani kwa wiki 12 zilizopita.

**Kutazama mbele *Misingi 4: Maisha Hukomaa***

Kwenye ***Misingi 4,*** kitabu cha mwisho kwenye mtiririko wa Uzima tutatazama namna ***Maisha Hukomaa.*** Tutatazama kwa ndani zaidi maisha yetu yanavyobadilika tunapopevuka kwenye imani yetu. Kama ilivyo kwenye maisha mtoto hukua na baadaye kufikia utu uzima, hivyo kwenye maisha yetu ya kiroho tunakua na kupevuka. Tunajifunza juu ya ishara ya kupevuka huku ikijumlisha kutaka mabadiliko, kile Biblia inachoita, 'kufa kwa nafsi.' Tutajifunza zaidi juu ya namna ya kusikia kutoka kwa Mungu na kumtii, na kusikiliza namna Mungu alivyowaongoza watu wake kupitia historia yote, na namna anavyoendelea kuwaongoza leo.

Tutatazama kwa undani zaidi namna ya kushirikisha kile ambacho Mungu ametupa – maisha yetu, muda na pesa – tukielewa kuwa kila tulicho nacho ni Mungu ametupa, na tunatumia kwa ubora tunapomkabidhi yeye. Hii inabadilisha namna tunavyoona dunia, namna tunavyoona eneo letu, na matamanio yetu ya baadaye. Kwa kumaliza tunatazama namna tunavyoweza kuvumilia kwenye imani yetu na kumaliza mbio ya imani vizuri, mpaka mwishoni tuende kuwa pamoja na Yesu milele.

**Maombi**

15 Dakika

Kweny vikundi vidogo chukua muda kidogo kushirikisha mahitaji ya maombi yaliyotokana na kipindi hiki. Pengine unaweza kushirikisha baadhi ya pointi za sifa kwa vitu ambavyo umemwona Mungu akifanya na kupitia kwako kwa sababu umefanyia kazi kifaa hiki. Unaweza pia kushirikisha baadhi ya pointi za maombi kwenye maeneo ambayo bado unasikia inahitaji kazi zaidi, au upenyo kabla hujaingia kwenye kitabu kingine.

Baada ya kushirikisha alama hizi za sifa na maombi, chukua muda kiasi kwenye kikundi chako kuombeana.

Mwishowe, kama kikundi chote, ombeni maombi yafuatayo:

> Bwana Yesu,
> Aksante kwa sababu umeumba maisha mapya ndani yangu, na kupitia mimi unataka kuumba maisha mapya kwenye familia yangu na jumuia yangu. Naomba kuwa unisaidie kuendelea kuweka imani yangu kwenye matendo, ili uweze kufanya kazi ndani na kupitia mimi, kuwafikia hao wanaokuhitaji zaidi.
> Amen.

p

**Kufanya wiki hii**

Kila wiki kuna kazi ya nyumbani sisi kufanya. Wiki hii uwe na muda wa kutafakari juu ya kifungu chetu cha kukumbuka. Pengine kutana na wanakikundi wengine 1-2 na kujadili pamoja:

- ‘Dini ya kweli’ ni ipi?
- Ina maana gani kujiweka mbali usiadhiriwe na dunia?
- Je kuna yatima au mjane au watu wengine walioadhirika kwenye jumuia yako ambao unaweza kuwasaidia?

**Shahidi**

Tumewafikia watu wengi tofauti wakati tumejifunza kitabu hiki pamoja. Matendo yetu yangewawagusa maisha ya watu wengi, ikileta mabadiliko. Haya ndiyo Mungu ametuagiza kufanya. Wiki hii tunaenda kumfikia mtu moja kwenye jumuia aliyeadhirika.

Mfikirie mtu moja anayeteseka, huyu anaweza kuwa yatima, mjane, aliliyeadhirika au watu wenye mahitaji kwenye jumuia yako. Fikiri namna utakavyo mbariki na kuwasaidia wiki hii halafu uende na kufanya jambo fulani juu ya hilo. Hii inaweza kuwa kushiriki chakula, kuwapa nguo, kuwasaidia kazi inayoonekana kuwa ngumu au kuwasaidia wao kupata vyanzo vingine vya msaada.

Ikiwezekana, washirikishe kwa nini umevuviwa kuwasaidia, wao ukiwaeleza uhusiano uliopo baina ya imani yako na matendo yako mema.

# Kifungu cha Kukumbukas

‘Sikiliza, ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja.’

*Kumbukumbu la Torati 6:4*

‘Hata walipokwisha kuziegesha mashua zao pwani, wakaacha vyote wakamfuata.’

*Luka 5:11*

‘Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana.’

*1 Wakorintho 12:7*

‘Ufuatilieni upendo, na kutaka sana karama za rohoni, lakini zaidi kwamba mpate kutoa unabii.’

*1 Wakorintho 14:1*

‘Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyosha mapito yako.’

*Mithali 3:5-6*

‘Mwizi huja tu kuiba, kuua na kuharibu; mimi nilikuja ili wawe na uzima, tena wawe nao tele.’

*Yohana 10:10*

‘Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote.’

*1 Timotheo 2:1*

‘Maana ufalme wa Mungu hauwi katika neno, bali katika nguvu.’

*1 Wakorintho 4:20*

‘Akawaambia, Mavuno ni mengi, lakini wafanya kazi ni wachache; basi mwombeni Bwana wa mavuno apeleke wafanya kazi katika mavuno yake.’

*Luka 10:2*

‘Lakini hukumu na iteremke kama maji, na haki kama maji makuu!’

*Amosi 5:24*

‘Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi.’

*Mathayo 25:40*

‘Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho.’

*Wagalatia 6:9*

‘Dini iliyo safi, isiyo na dosari mbele za Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.’

*Yakobo 1:27*

# Kumbukumbu

# Mpangilio wa Picha

| **Picha** | **Undani wa Picha** |
|---|---|
| Jalada la mbele | Imepigwa picha na Bill Williams siku ya Unsplash |
| Kikao cha 1 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Danielle Barnes siku ya Unsplash |
| Kikao cha 2 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Mega Caesaria siku ya Unsplash |
| Kikao cha 3 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Ullash Borah siku ya Unsplash |
| Kikao cha 4 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Clem Onojeghuo siku ya Unsplash |
| Kikao cha 5 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Richard Thompson, imetumika kwa ruhusa |
| Kikao cha 6 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Savas Kazantzides siku ya Unsplash |
| Roman soldier | Image by macrysstina siku ya Pixabay |
| Kikao cha 7 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Nathan Dumlao siku ya Unsplash |
| Kikao cha 8 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Samuel Zeller siku ya Unsplash |
| Kikao cha 9 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Capturing the Human Heart siku ya Unsplash |
| Kikao cha 10 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Karthikeyan K siku ya Unsplash |
| Kikao cha 11 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Atlas Green siku ya Unsplash |
| Kikao cha 12 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Francesco Gallarotti siku ya Unsplash |
| Kikao cha 13 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Avel Chuklanov siku ya Unsplash |

MISINGI 3:

# Maisha Huumba

***Misingi*** ni mafundisho inayowasaidia watu kugundua na kukua ndani ya mahusiano yao na Mungu na kuwatia moyo kuhudumia jumuiya zao. Iliandikwa ili iweze kutoa vifaa vilivyo bora ambavyo vingeweza kutumika kwenye maeneo mengi ya kijiografia na kwenye vikundi vya kitamaduni duniani pote. Misingi ni mkusanyiko wa seti ya vitabu vine, na kila kimoja kinayo vipindi kumi na vitatu ya mafundisho kwenye vikundi.

***Misingi*** imeandikwa na waandishi wageni waliojitolea toka duniani kote na kukusanywa na kuandaliwa na Dignity.

***Misingi 3: Maisha Huumba*** umakini namna mitume walivyoishi ndani ya jumia walivyoleta mabadiliko kwa kila kilchowazunguka wao. Mkristo mwenye afya kwa kawaida huumba maisha waliyopewa kwenye jumuia zao na kwa watu wengine.

**Wasiliana nasi kwa hello@dignityonline.org.uk au +44(0)7340 573 937. Kwa majina ya vitabu vyetu vyote na gharama tembelea tovuti yetu: www.dignityonline.org.uk/publications.**

Swahili Toleo la kwanza
Aliyeandaa jalada: The Message Trust
Picha ya jalada: Bill Williams/Unsplash

DIGNITY

www.dignityonline.org.uk